# MNYAMBULIKO WA VITENZI KATIKA LUGHA YA KIMAASAI CHA ENEO LA SUSWA, MOSIRO NA ILKERIN-LOITA (NAROK, KENYA).

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

ACQUISITION SECTION
EGERTON UNIVERSITY LIBRARY
19 SEP 2013
P.O. BOX 536, EGERTON

ALEXANDER S. MEITAMEI

Tasnifu Hii Imewasilishwa Ili Kutosheleza Baadhi Ya Mahitaji Ya Shahada Ya Uzamili (M.A) Ya Isimu Ya Lugha Ya Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Egerton.

CHUO KIKUU CHA EGERTON

EULIB
041 002

2013/96618

## UNGAMO NA IDHINI

### UNGAMO

Hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote ile katika chuo chochote kile.

Alexander S. Meitamei: Sahihi ........................ Tarehe 27/10/08
**AM12/1313/04**

### IDHINI

Tasnifu hii ya shahada ya uzamili imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Egerton.

1. Dkt. Furaha Chai : Sahihi ........................ Tarehe 27-10-08

2. Dkt. Onyango Ogola: Sahihi ........................ Tarehe 27-10-08

**© HATILINZI**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kuhifadhi kwa mfumo wowote ule au kutoa hata sehemu ndogo ya tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

Alexander s. Meitamei © 2008

**© HATILINZI**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kuhifadhi kwa mfumo wowote ule au kutoa hata sehemu ndogo ya tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

## TABARUKU

Kwa Rabuka aloziumba lugha zote,
Kisha kazigawanya kwa mataifa yote.
Kwa nyanyangu alonifunza Kimaasai chote,
N'kaweza kuzibaini mofimuze zote.

# SHUKRANI

Shukrani zangu za kwanza zimwendee Maulana kwa kuyaongoza mema yote tutendayo chini ya jua. Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu, Dkt. Furaha Chai pamoja na Dkt. Onyango Ogola ambao kwanza kabisa, walinielekeza katika kuikuza dhana na kuipevusha iwe suala la utafiti. Baadaye waliikosoa kazi yangu bila kukawia wala kuchoka na kunipa mwongozo mwema wakati wote wa maandalizi, utekelezaji wa utafiti na uandishi wa tasnifu hii. Aidha hawakukosa kunijibu nilipowapigia simu katika saa zisizokuwa rasmi au nilipotaka kuwaona bila miadi. Rahimu awape maisha marefu waweze kuwapevusha wengine kama walivyonipevusha mimi.

Shukrani zangu za kipekee ziwaendee Dkt. Mwenda Mukuthuria, Dkt. Aswani Buliba, Dkt. Mutiti na Bw. Ngwachi Mayaka kwa hoja muhimu walizochangia wakati wa utafiti huu.

Sikosi kutabasamu niwakumbukapo wahudumu wa maktaba ya FASS, Chuoni Egerton; hawa walinilakabu Bwana TUKI! Jambo hili lilitokana na uzoefu wangu wa kuitumia kamusi ya pekee ya TUKI ya Kiingereza - Kiswahili iliyokuwepo, hasa nilipokuwa nikiliandaa pendekezo langu. Hao wote walinitakia heri na fanaka katika usomi wangu. Wahudumu hawa, pomoja na wale wa maktaba za vyuo vikuu vya Nairobi na Dar es Salaam walinihudumia kwa moyo mweupe nilipokuwa nikipitia maandishi; mimi pia nawaombea baraka za Maulana.

Nawezaje kusahau kuishukuru familia yangu, mke wangu Annie, na wanangu Amos, Jemima na Tabitha ambao kila mara walikuwa kisima cha liwazo baada ya uchovu na mashaka yanayoambatana na usomi wa shahada ya uzamili? Pia na babangu Philip Ole Nkobei na mamangu Damaris en Ole Nkobei ambao walinisaidia kwa hali na mali kila wakati, na kipindi chote cha kuisomea shahada hii.

Daima sitakosa kumshukuru nyanyangu Kiramatisho en Ole Nkobei aliyenilea katika mazingira mlimokuwa na fonimu na mofimu za lugha ya Kimaasai, akanifunza kuzitamka na kuzipanga ifaavyo. Ingawa sasa ni mkongwe sana bado yeye hujikakamua kunisimulia ngano na kuniimbia nyimbo za kiasili lau kwa shida.

Katika shule ya Upili ya Olasiti-Suswa, ningependa kumshukuru mwalimu mkuu Mwangi Irungu, aliyenipa tarakilishi ya shule niitumie kuichapa kazi hii. Hili pia, ni jambo ambalo sitalisahau. Kwa wale wengine wote ambao walisaidia kuifanikisha kazi hii na ambao sijawataja, hebu wafahamu kuwa nawashukuru na kuwapenda, tena sana.

# ABSTRACT

Maasai language has attracted many scholars ranging from historians, anthropologists and linguists. However, their studies did not give a detailed account of the process of verb derivation of this Language. This research therefore, was on the process of verb extensions in Maasai language. The aim of the research was to identify derivational morphemes and the accompanying formal and semantic transformations within the verb grammatical part of speech in the Maasai language. The research was founded on the premise that identifiable morphemes exist within words and that both phonological and lexical processes operate within these elements, thus giving rise to the formal and semantic changes. Two structuralist theories guided this research. *Hockett's Morphological Theory* formed the analytical framework while *Transformational Generative Grammar* (TGG) formed the descriptive framework. The method of research for this study was *content analysis*. This method was used in the collection of verb data as well as in the analysis to identify the derivational morphemes. These verbs were sampled purposively from naturally occurring discourse and from various oral literature genres such as songs, proverbs, and narratives. It is hoped that the findings of this research, which confirmed the existence of different verb extensions in Maasai language, are a major contribution to this language at the morphological level, as they described some of the principles that guide the morphology of the language, particularly in regard to the morphological process of derivation. It is also hoped that, the research will be useful to Swahili language students, teachers and language planners. This is particularly so as in East Africa where, apart from Swahili and Nyamwezi, other available works on verb extensions in our libraries were done by foreign scholars and have tended to concentrate on equally alien languages such as German, Hungarian or even Russian. It is one study that investigates the concept of morphology of East African languages.

## IKISIRI

Lugha ya Kimaasai imewavutia wasomi wengi wa kihistoria, anthropolojia na wanaisimu. Hata hivyo, tafiti hizi hazikuchunguza kwa kina swala la mfanyiko wa mnyambuliko wa vitenzi. Kwa mintarafu hii, utafiti huu ulihusu mfanyiko wa mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kimaasai. Dhamira ya utafiti huu ilikuwa ni kutambulisha mofimu nyambulishi pamoja na mabadiliko ya kimaumbo na kisemantiki yanayoziandama katika kundi la kisarufi la vitenzi. Utafiti huu ulijikita katika msingi kwamba mofimu hupatikana katika maneno na kwamba mifanyiko ya kifonolojia na kileksia hutenda kazi miongoni mwa vipengele hivi na kusababisha mabadiliko ya kimaumbo na kisemantiki. Nadharia mbili za Wanamuundo ziliuongoza utafiti huu ambapo *Nadharia ya Mofolojia ya Hockett* ilikuwa msingi wa uchanganuzi ilihali *Nadharia ya Sarufi zalishi Geuza Umbo* ilikuwa msingi wa kutoa maelezo ya mabadiliko ya kimaumbo na kisemantiki. Mbinu ya utafiti huu ilikuwa *uchanganuzi wa yaliyomo.* Mbinu hii ilitumika katika ukusanyaji wa data ya vitenzi na pia katika uchanganuzi wa vitenzi vile ili kuzipata mofimu nyambulishi. Vitenzi hivi viliteuliwa kimaksudi kutoka katika mazungumzo ya kawaida na pia kutoka katika tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya lugha ya Kimaasai kama vile nyimbo, methali na hadithi. Inatarajiwa kuwa matokeo ya utafiti huu, ambayo yamedhihirisha kuwepo kwa minyambuliko tofauti ya vitenzi katika lugha ya Kimaasai ni hatua mbele ya kuendeleza mofolojia ya lugha hii kwa kuzielezea baadhi ya kaida zinazoitawala, hasa katika mfanyiko wa unyambuaji. Isitoshe, yatakuwa ya manufaa kwa wanafunzi, walimu na wapangaji wa lugha ya Kiswahili. Hii hasa ni kwa sababu katika Afrika Mashariki, isipokuwa Kiswahili na Kinyamwezi, tafiti zingine za kina za mnyambuliko wa vitenzi zilizopo katika maktaba zetu ni za kigeni na zimezingatia lugha za kigeni kama vile Kijerumani, Kihangari au hata Kirusi. Ni mojawapo ya tafiti zinazoichunguza dhana ya mofolojia katika lugha za Afrika Mashriki.

EGERTON UNIVERSITY LIBRA

YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI ..... ii
HATILINZI ..... iii
TABARUKU ..... iv
SHUKRANI ..... v
ABSTRACT ..... vii
IKISIRI ..... viii
YALIYOMO ..... ix
ORODHA YA MAJEDWALI ..... xi
MAELEZO YA VIFUPISHO ..... xiii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI
1.1 Usuli wa Mada ..... 1
1.2 Mada ya Utafiti ..... 2
1.3 Madhumuni Ya Utafiti ..... 2
1.4 Nadharia Tete ..... 2
1.5 Umuhimu wa Utafiti ..... 2
1.6 Upeo wa Utafiti ..... 3
1.7 Maelezo ya Istilahi ..... 3

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI
2.1 Utangulizi ..... 5
2.1.1 Dhana ya Unyambuaji kwa jumla ..... 5
2..1.2 Mnyambuliko wa Vitenzi katika lugha ya Kiswahili ..... 8
2.1.3 Tafiti kuhusu lugha ya Kimaasai ..... 10
2.2 Msingi wa Nadharia ..... 11

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI
3.1 Utangulizi ..... 17
3.2 Ukusanyaji wa Data ..... 17
3.2.1 Mahali pa Utafiti ..... 17
3.2.2 Uteuzi wa Sampuli ..... 18
3.3 Uchanganuzi wa Data ..... 21

SURA YA NNE: MUUNDO WA VITENZI VYA KIMAASAI KIFONOLOJIA NA KIMOFOLOJIA

4.1 Utangulizi....25
4.2 Fonimu za lugha ya Kimaasai....25
4.2.1Vokali....25
4.2.2 Konsonanti....27
4.3 Mofolojia ya Vitenzi vya lugha ya Kimaasai....29
4.4 Sintaksia ya Lugha ya Kimasai....35

SURA YA TANO: MNYAMBULIKO WA VITENZI KATIKA LUGHA YA KIMAASAI

5.1 Utangulizi....38
5.2 Vitenzi sahili vya lugha ya Kimaasai....38
5.3 Hali tofauti za Mnyambuliko wa Vitenzi....56
5.3.1 Mnyambuliko Ala-tendea....56
5.3.2 Mnyambuliko wa jinsi ya Kutendea....62
5.3.3 Mnyambuliko wa jinsi ya Kutendesha....61
5.3.4 Mnyambulikowa jinsi ya Kutendwa/ Kutendewa....75
5.3.5 Mnyambuliko wa jinsi ya Kutendana....82
5.3.6 Mnyambuliko wa jinsi ya Kutendeka....87
5.3.7 Mnyambuliko Geuzi/ Zalishi....81
5.3.8 Mnyambuliko Radidi....94

SURA YA SITA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

6.1 Utangulizi....97
6.2 Muhtasari....97
6.3 Mapendekezo....99
6.4 Hitimisho....99
MAREJELEO....101

# ORODHA YA MAJEDWALI

Konsonanti za lugha ya Kimaasai ............................................................................27

Alomofu za mofimu za mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kimasai ............. 97

## MAELEZO YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| KB | Kibainishi |
| NF | Nafsi |
| WK | Wakati |
| MZ | Mzizi |
| MN | Mnyambuliko |
| KNF | Kirejeshi nafsi (tenda au tendwa) |
| KI | Kiishio |
| WI | Wingi |
| R | Rai |
| MT | Mofu Tupu |
| J | Jinsia |
| UK | Ukanusho |
| SH | Shina |
| SAH | Sàhili |
| AL-EA | Ala-tedea |
| UH-EA | Uhusika- tendea |
| ESH | Tendesha |
| W/EW | Tendewa |
| AN | Tendana |
| EK | Tendeka |
| GEUZI | Geuzi/zalishi |
| RADIDI | Uradi |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa mada

Mofolojia ni tawi la isimu ambalo katika miongo ya sitini na sabini lilikuwa likichukuliwa kama sehemu ya fonolojia kwa upande mmoja na sintaksia kwa upande mwingine. Mawazo haya yaliendelezwa na wanaisimu kama vile Chomsky (1957) na Aronoff (1979). Kuanzia miongo ya themanini, dhana ya mofolojia imechukua mwelekeo mpya ambapo wanaisimu wamedhihirisha kuwa ni eneo huru la kiisimu lenye sheria na kaida zake. Kumekuwa na tafiti nyingi za kimofolojia katika lugha nyingi ambapo wanaisimu wamekuwa wakijaribu kuibua nadharia ya kijumla ya mofolojia.

Vitenzi ni mojawapo ya makundi wazi ya kisarufi. Hivi ni kusema kwamba vitenzi vina uwezo wa kuathiriwa na mifanyiko mbalimbali ya kimofolojia kama vile unyambuaji, uambishaji, uambatanishaji na mifanyiko mingine. Kwa mintarafu hii, vitenzi vinakuwa eneo mwafaka la kufanyia utafiti wowote ule wa kimofolojia. Hii ni sababu mojawapo iliyompelekea mtafiti kukichagua kikundi cha vitenzi katika utafiti huu wa kimofolojia.

Lugha ya Kimaasai ni mojawapo ya lugha za Kinailotiki inayozungumzwa katika eneo kubwa la Bonde la Ufa; sehemu za Samburu, Baringo, Nakuru, Narok, Trans-Mara na Kajiado nchini Kenya na pia katika sehemu za Arusha na Serengeti nchini Tanzania. Kuhusu lugha ya Kimaasai nimekumbana na kazi kadha wa kadha za fasihi, msamiati na maelezo ya kijumla ya sarufi. Nyingi ya tafiti hizi zilifanywa na Wazungu wamishenari na Wasafiri wa awali wakitafuta kuuelewa utamaduni wa Waafrika kwa lengo la kueneza himaya za Wazungu na dini ya Kikristu. Miongoni mwa watafiti hawa, wale walioandika makamusi ndio waliopiga hatua kubwa zaidi kuitafiti lugha hii. Mifano mizuri ya kazi hizi ni kama vile *Maasai Vocabulary* ya Shaffer (1955) na *Maa-A Dictionary of the Maasaai Language and Folklore: English–Maasai* ya Mol (1979). Kazi zingine za awali katika lugha hii ni kama zile za Meyer (1891), Hollis (1905), (Krapf (1854), Tucker na Mpaayei (1955) na zinginezo. Watafiti hawa wa awali walitoa hoja muhimu zinazohusiana na lugha hii na mtafiti alipata mshawasha wa kuendeleza kazi zile kwa kuchunguza kwa undani zaidi juu ya mfanyiko wa mnyambuliko wa vitenzi katika lugha hii.

Kuna haja ya kufanya utafiti zaidi wa mifanyiko mingine ya kimofolojia katika vitenzi na katika makundi mengine ya maneno katika lugha hii. Mofolojia ya Kimaasai ni eneo ambalo halijafanyiwa utafiti wa kutosha.

## 1.2 Mada ya Utafiti

Swala la mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kimaasai halijashughulikiwa kwa undani licha ya kuwepo tafiti kadha wa kadha za isimu ya lugha hii. Utafiti huu kwa hivyo ulishughulikia tatizo hili chini ya mada 'Mnyambuliko wa Vitenzi katika Lugha ya Kimaasai kinachozungumzwa katika eneo la Suswa, Mosiro na Ilkerin Loita'.

## 1.3 Madhumuni Ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni mawili;

1. Kutambulisha muundo wa vitenzi vya lugha ya Kimaasai kifonolojia na kimofolojia.
2. Kubanisha mofimu nyambulishi katika vitenzi vya lugha ya Kimaasai.
3. Kutambulisha maana na maumbo tofauti yanayotokana na mnyambuliko wa vitenzi vya lugha ya Kimaasai.

## 1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete mbili;

1. Vitenzi vya lugha ya Kimaasai vina muundo mahsusi kifonolojia na kimofolojia.
2. Mofimu mahsusi zinazowakilisha minyambuliko zinaweza kubainishwa katika vitenzi vya lugha ya Kimaasai.
3. Maana na maumbo tofauti yanayotokana na mnyambuliko wa vitenzi vya lugha ya Kimaasai zinaweza kutambulishwa.

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Mnyambuliko wa vitenzi ni kipengele mojawapo cha uwanja mpana wa mofolojia. Uwanja huu wa kiisimu unafaa kutafitiwa ili upanuliwe na kuendelezwa. Mathews (1974:1,19) na Anderson (1992:6) wanakubaliana kuwa hakujazuliwa nadharia moja ya kijumla ya kimofolojia inayoweza kutumiwa kuchanganulia lugha zote ulimwenguni.

Tafiti za lugha nyingi zitasaidia kuibua maelezo au nadharia ya kijumla ya mofolojia. Utafiti huu ulichangia lau kwa kiwango kidogo katika kufanikisha jambo hili.

Utafiti huu umeshughulikia mnyambuliko wa vitenzi. Vitenzi ni kikundi cha kimsingi katika sarufi ya lugha yoyote ile. Hii ni kwa sababu vitenzi huweza kujumuisha vipashio tofauti tofauti kama vile wakati, nafsi, idadi, na hali zinginezo mbali mbali. Mofolojia kamili ya lugha ya Kimaasai haijulikani licha ya kuwepo kazi nyingi za lugha hii ambazo zimetoa vidokezo muhimu kuihusu. Inatumainiwa kuwa, matokeo ya utafiti huu ambayo yamedhihirisha kuwepo kwa minyambuliko ya vitenzi katika lugha ya Kimaasai ni hatua mbele ya kuendeleza mofolojia ya lugha hii kwa kuzielezea baadhi ya kaida zinazoitawala, hasa katika mfanyiko wa unyambuaji. Isitoshe, matokeo ya utafiti huu yatakuwa ya manufaa kwa wanafunzi, walimu na wapangaji wa lugha ya Kiswahili. Hii hasa ni kwa sababu katika Afrika Mashariki, isipokuwa Kiswahili na Kinyamwezi, tafiti zingine za kina za mnyambuliko wa vitenzi zilizopo katika maktaba zetu ni za lugha za kigeni kama vile Kijerumani, Kihangari au hata Kirusi. Huu ni mojawapo ya tafiti zilizoichunguza dhana ya mofolojia katika lugha za Afrika Mashariki.

## 1.6 Upeo wa Utafiti

Kuna viwango vingi vya uchanganuzi wa kiisimu kama vile fonolojia, mofolojia au sintakisia. Utafiti huu ulishughulikia kiwango cha mofolojia. Katika mofolojia kunayo mifanyiko tofautitofauti kama vile unyambuaji, uambishaji na uambatanishaji; utafiti huu ulijihusisha na mfanyiko wa unyambuaji pekee. Katika lugha yoyote ile, kuna makundi manane ya maneno kisarufi; nomino, viwakilishi, vitenzi, vielezi, vivumishi, viunganishi, vihusishi na vihisishi. Mtafiti alishughulikia unyambuaji katika kikundi cha vitenzi vya lugha ya Kimaasai.

Utafiti huu hasa ulihusu Kimaasai kinachozungumzwa katika maeneo ya Suswa, Mosiro na Ilkerin-Loita, wilayani Narok. Koo za Wamaasai wanaoishi sehemu hii ni Ilkeek-Onyokie, Ilpurko, Ildamat na Iloitai.

Sababu za kuteuliwa kwa sehemu hizi ni kwamba hii ndiyo sehemu pana zaidi iliyo na wazungumzaji wengi wa lugha ya Kimaasai na kwamba Kimaasai kinachozungumzwa katika eneo hili kinachukuliwa kama lahaja sanifu na kutumika na Wamishenari katika uandishi wa Bibilia na vitabu kadha wa kadha alivyorejelea mtafiti.

## 1.7 Maelezo ya Istilahi

*Fonetiki:* Somo linalojihusisha na sayansi ya utamkaji wa sauti za lugha (Mathews:1991).

*Fonimu:* Kipashio kidogo zaidi cha lugha kinachoweza kuhusishwa na lugha mahsusi (Lass:1984).

*Kibadala:* Maumbo tofauti ya mofimu moja. Pia chaweza kuitwa alomofu.

*Kielezo cha maneno:* Seti ya maneno mazima yanayopangwa kulingana na kategoria za kisarufi au ruwaza ya neno inayoonyesha maumbo yake katika sarufi.

*Kielelezo cha maneno:* Seti ya maneno kamili yanayopangwa kulingana na kategoria za kisarufi au ruwaza ya maneno inayoonyesha maumbo yake tofauti katika sarufi.

*Mfanyiko:* Kuathiriana kwa mofimu au fonimu kunakoibua maana na maumbo tofauti .

*Muundo:* Mpangilio na idadi ya mofimu katika maneno.

*Mofolojia:* Muundo wa ndani wa maneno katika tungo mbalimbali (Mathews : 1974).

*Mofimu:* Vipashio vidogo zaidi vyenye maana kisarufi visivyoweza kugawika zaidi bilakupoteza maana (Mathews (1974).

*Umbo:* Sura, umbile, jinsi au mkao wa mofimu.

*Unyambuaji:* Mfanyiko mojawapo wa kimofolojia ulio na uwezo wa kubadilisha maana, umbo au kikundi cha kisarufi cha neno (Kapinga 1983).

Sura hii ya kwanza ilihusu utangulizi wa utafiti kwa kutoa maelezo ya vipengele vyake kama vile usuli wa mada, tatizo na umuhimu wa utafiti huu kwa jumla.
Sura ifuatayo nayo ilijihusisha na uchanganuzi wa kijumla wa tafiti zilizofanywa kuhusiana na mada ya mnyambuliko katika lugha kadha wa kadha na nadharia ziliouongoza utafiti.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, mwandishi amepitia maandishi yanayohusu dhana ya mfanyiko wa unyambuaji kwa jumla. Vile vile sura hii imeangazia maandishi yaliyochapishwa yanayohusu lugha ya Kimaasai. Hatimaye mtafiti ameelezea nadharia na mikabala iliyouongoza utafiti huu.

### 2.1.1 Dhana ya unyambuaji kwa jumla

Unyambuaji ni mojawapo ya mifanyiko ya Kimofolojia. Neno 'unyambuaji' linatokana na neno 'nyambua' au 'nyumbua' linalomaanisha kurefusha kitu kama mpira (Kapinga 1983:26, Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Tuki, 1993, Mbaabu 1985). Unyambuaji unahusu kufungilia kiambishi au viambishi katika shina. Hata hivyo, katika baadhi ya lugha mnyambuliko hutokea bila kuwepo kwa kufungiliwa viambishi katika shina.

Mzizi huweza kuashiria mnyambuliko katika mofolojia ya baadhi ya lugha. Katika Kiingereza huitwa, *marked base form*. Ikiwa mzizi hauashirii mnyambuliko basi huitwa '*unmarked base form*' (Adams 1973:12). Unyambuaji hujitokeza mara kwa mara pale ambapo wazungumzaji wa lugha hutumia viambishi vipya katika maneno kwa namna inayosikika kama kawaida. Lugha ya Kiingereza ina mifano kama vile *workaholic*, *radioholic* na mengine.

Maumbo ya maneno yaliyonyambuliwa na yenye mizizi au mashina yanayofanana yanaweza kupangwa katika vielelezo (*paradigms* katika Kiingereza), kama vya maneno ambishaji. Hata hivyo viambishi nyambulishi (mofimu nyambulishi) hazina ule uthabiti wa kimaana na kimaenezi. Hii ndiyo sababu tofauti hutolewa kati ya myambuliko sarufi na mnyambuliko geuzi. Myambuliko sarufi huunda neno jipya bila kubadilisha kikundi chake cha kisarufi. Kwa mfano katika Kiswahili, kitenzi *panda* kikinyambuliwa katika hali ya kutendesha linakuwa *pandisha* ambalo pia ni kitenzi. Kwa upande mwingine mnyambuliko geuzi huunda neno jipya na kulihamisha kutoka kikundi chake asilia hadi kikundi kingine cha kisarufi. Kwa mfano, neno *compute* la Kiingereza ambalo ni kitenzi likifungiliwa mofimu ya myambuliko, {*r*} linakuwa *computer* ambalo ni nomino. Katika Kiswahili kuna neno *chuja* ambalo ni kitenzi na likifungiliwa mofimu {m} na {o} huunda nomino *mchujo*.

Maalmjaer (1991: 65) ameelezea aina nyingine ya mnyambuliko geuzi anaouita '*conversion*' ambapo neno hubadilisha kikundi chake cha kisarufi bila kufungiliwa mnyambuliko wowote. Wanatoa mfano wa nomino '*a hoover*' (kifaa cha kusafisha sakafu) na kitenzi '*to hoover*' (kusafisha sakafu kwa kutumia kifaa hicho). Pia nomino '*a service*' kumanisha huduma na kitenzi '*to service*' kumaanisha 'kuhudumia'. Huu nao Maalmjaer Maalmjaer auita mnyambuliko – ndani (tafsiri yangu ya '*internal derivation*').

Unyambuaji waweza kutofautishwa na mfanyiko wa Uambishaji kwa vigezo vitatu muhimu. Kwanza ni dhima yake katika neno. Dhima ya mnyambuliko sio kuwakilisha kategoria za kimofosintaksia kama vile idadi, wakati au nafsi bali ni kuunda maneno au mashina mapya. Katika Kiswahili kwa mfano, neno *sema* linaponyambuliwa katika hali ya kutendeka linakuwa *semeka*. Neno hili ingawa bado ni kitenzi limekuwa neno jipya kwa misingi ya kubadilika kwa umbo la mzizi kuwa {*semek*} badala ya {*sem*} na pia kubadilika kwa maana.

Kigezo cha pili kinachoutofautisha unyambuaji na uambishaji ni ule uwezo wa kulitoa neno kutoka kikundi kimoja cha kisarufi hadi kingine kama ilivyotajwa hapo awali.

Kigezo cha tatu ni kile cha uthabiti wa kisemantiki na kimaenezi. Uthabiti huu haufuati utaratibu unaotarajiwa wa vielelezo katika baadhi ya lugha. Katika Kiingereza kwa mfano, mofimu '*al*' ikifungiliwa katika mzizi wa vitenzi '*arrive*' na '*dispose*' matokeo ni nomino '*arrival*' na '*disposal*', lakini mofimu hiyo inapofungiliwa katika nomino '*nose*', '*brute*' au '*doctor*' matokeo sio nomino bali ni vivumishi '*nasal*', '*brutal*' na '*doctoral*'.

Licha ya tofauti hizi, mofimu za minyambuliko pia zina uwezo wa kuzalisha maumbo mapya katika leksimu mbalimbali. Hata hivyo uzalishaji huu hutofautiana kati ya mnyambuliko mmoja na mwingine. Kwa mfano, katika Kiswahili mofimu {*e*} ya kauli ya kutendea, {*esh*} ya kutendesha au {*ek*} ya kutendeka hupatikana katika vitenzi vingi. Lakini { *at*} ya kutendata kwa mfano katika kitenzi '*fumbata*' au {*am*} ya kutendama kwa mfano katika neno '*fungama*' ni chache sana. Katika Kiingereza nomino zenye mofimu ya mnyambuliko '*-hood*' kama vile katika neno '*boyhood*' au '*neighbourhood*' ni chache ikilinganishwa na mofimu {*-ist*} na {*-ize*} katika maneno kama vile '*communist*', '*opportunist*', '*computerize*' na '*centralize.*'

Wanatoa mfano wa nomino '*a hoover*' (kifaa cha kusafisha sakafu) na kitenzi '*to hoover*' (kusafisha sakafu kwa kutumia kifaa hicho). Pia nomino '*a service*' kumanisha huduma na kitenzi '*to service*' kumaanisha 'kuhudumia'. Huu nao Maalmjaer Maalmjaer auita mnyambuliko – ndani (tafsiri yangu ya '*internal derivation*').

Unyambuaji waweza kutofautishwa na mfanyiko wa Uambishaji kwa vigezo vitatu muhimu. Kwanza ni dhima yake katika neno. Dhima ya mnyambuliko sio kuwakilisha kategoria za kimofosintaksia kama vile idadi, wakati au nafsi bali ni kuunda maneno au mashina mapya. Katika Kiswahili kwa mfano, neno *sema* linaponyambuliwa katika hali ya kutendeka linakuwa *semeka*. Neno hili ingawa bado ni kitenzi limekuwa neno jipya kwa misingi ya kubadilika kwa umbo la mzizi kuwa {*semek*} badala ya {*sem*} na pia kubadilika kwa maana.

Kigezo cha pili kinachoutofautisha unyambuaji na uambishaji ni ule uwezo wa kulitoa neno kutoka kikundi kimoja cha kisarufi hadi kingine kama ilivyotajwa hapo awali.

Kigezo cha tatu ni kile cha uthabiti wa kisemantiki na kimaenezi. Uthabiti huu haufuati utaratibu unaotarajiwa wa vielelezo katika baadhi ya lugha. Katika Kiingereza kwa mfano, mofimu '*al*' ikifungiliwa katika mzizi wa vitenzi '*arrive*' na '*dispose*' matokeo ni nomino '*arrival*' na '*disposal*', lakini mofimu hiyo inapofungiliwa katika nomino '*nose*', '*brute*' au '*doctor*' matokeo sio nomino bali ni vivumishi '*nasal*', '*brutal*' na '*doctoral*'.

Licha ya tofauti hizi, mofimu za minyambuliko pia zina uwezo wa kuzalisha maumbo mapya katika leksimu mbalimbali. Hata hivyo uzalishaji huu hutofautiana kati ya mnyambuliko mmoja na mwingine. Kwa mfano, katika Kiswahili mofimu {*e*} ya kauli ya kutendea, {*esh*} ya kutendesha au {*ek*} ya kutendeka hupatikana katika vitenzi vingi. Lakini { *at*} ya kutendata kwa mfano katika kitenzi '*fumbata*' au {*am*} ya kutendama kwa mfano katika neno '*fungama*' ni chache sana. Katika Kiingereza nomino zenye mofimu ya mnyambuliko '*-hood*' kama vile katika neno '*boyhood*' au '*neighbourhood*' ni chache ikilinganishwa na mofimu {*-ist*} na {*-ize*} katika maneno kama vile '*communist*', '*opportunist*', '*computerize*' na '*centralize.*'

### 2.1.2 Mnyambuliko wa Vitenzi katika lugha ya Kiswahili

Kumekuwa na tafiti nyingi za mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili zilizofanywa na watafiti kama vile Ashton (1944), Johnson (1939), Miehe (1989), Polome (1967), na kazi mpya kabisa iliyofanywa na Lodhi (2002). Lodhi ameelezea minyambuliko kumi na moja kwa kutumia mwongozo uliotolewa na Ashton (1944).

*Orodha Ya Ashton (1944 : 214)*

Tendea / fanyia (Applied / Propositional)

Tendeka / Fanyika (stative / Neuter)

Tendesha / Fanyiza (Causative)

Tendama / Fanyama (Static)

Tendata / Fanyata (Contactive / Tenacious)

Tendua / Fanyua (Conversive)

Tendana / Tendeana Fanyana / Fanyiana (Reciprocal / Associative)

Tendwa / Fanywa (passive)

Mnyambuliko kiwango (Augmentative)

Uradidi / Tendatenda / Fanyafanya (Subtractive)

Mnyambuliko Geuzi (Inceptive)

Mnyabuliko wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili huwakilishwa na viambishi au mofimu mahsusi, kwa mfano;

Jinsi ya *kutendea* huonyesha kuwa kitendo kimetekelezwa kwa niaba ya au kitu kimetumiwa kutendea kitendo. Mnyambuliko huu huwakilishwa na viambishi {ea}, {ia} kama vile katika maneno somea, kimbilia au lilia. Mnyambuliko huu hudhihirisha ulinganifu wa vokali ambapo vitenzi vyenye vokali {a}, {i} na {u} katika mzizi huwa na vokali {i}katika kiishio. Vitenzi vyenye vokali /e} na {o} katika mzizi huwa na vokali {e} kati ya mzizi na kiishio. Kwa mfano katika maneno yafuatayo;

Panga - pangia

Lima -limia

Chuma - chumia

Cheza - chezea

Choma - chomea

Jinsi ya *kutendesha* huleta maana ya sababisha kutenda jambo au sababisha liwe na huwakilishwa na viambishi {ish}, {esh}, {ez}, {iz} au {vy} kama vile katika maneno nawisha/navya, katisha/katiza, lewesha /levya, au tembeza.

Jinsi ya *kutendama* huwa na maana ya jambo kutendeka na kuendelea kutendeka kwa kitambo na huwakilishwa na kiambishi {am} kama vile katika maneno inama, kwama, zama au tazama.

Jinsi ya *kutendata* huwa na maana ya jambo kutendeka kwa ukamilifu na huwakilishwa na kiambishi {at} kama vile katika maneno kamata kumbatia au fumbata.

Jinsi ya *kutendua* ni mnyambuliko unaoleta maana ya kinyume na ile inayobebwa na mzizi wa kitenzi na huwakilishwa na kiambishi {u} au {o} kama vile katika maneno tegua, chomoa, tandua, tanduka au fungua.

Jinsi ya *kutendana* nayo huwa na maana ya ushirikiano, uhusiano au kutegemeana na huwakilishwa na viambishi {an}, {ian} na {ean} kama vile katika maneno imbiana, pendana, kumbatiana au tembeleana.

Jinsi ya *kutendatenda* huwa na maana ya kurudiarudia kitendo na hujitokeza kwa uradidi wa mzizi au shina la kitenzi. Mifano ni kama katika vitenzi vunjavunja pigapiga au rukaruka.

Jinsi ya *kutendwa / kutendewa* huwa na maana ya mtu/kitu kuelekezewa jambo au jambo kutendwa kwa ajili ya mwingine. Mnyambuliko huu huwakilishwa na viambishi {w}, {iw}, {ew/ {liw}, au {lew} kwa mfano katika maneno katwa, twaliwa, chekwa/chekelewa au somwa/somewa.

*Mnyambuliko geuzi* umepewa jina *inceptive form* na Ashton (1944). .Mnyambuliko huu hukibadilisha kikundi cha kisarufi cha kitenzi husika kiwe cha kikundi kingine kama vile nomino au kivumishi. Kwa mfano katika maneno yafuatayo;

Kitenzi Ogopa - nomino woga, vivumishi mwoga au mwogofu.

Kitenzi nenepa - kivumishi –nene, nomino unene

Kitenzi -la - kivumishi mlafi au nomino ulafi, ulaji.

Katika Kiswahili kuna mnyambuliko unaoelezea nguvu, ukali au jinsi kitendo kiliivyotukia na Ashton anauita *Augmentative form*. Mnyambuliko huu hauna kiambishi maalum kinachouwakilisha na hujitokeza katika hali zifwatazo;

Epa (jiondoa) ---- epua (ondoa)

Songa(bana) ---- songoa (kamua)

Sikia - hali ya kawaida ya kupokea sauti.

Sikiliza - kutega sikio ili kuipokea sauti kwa makini.

Ni kwa kufuata utaratibu huu ambapo mtafiti aliainisha mnyambuliko wa vitenzi uliyopo katika lugha ya Kimaasai. Mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili haujateuliwa kwa sababu ya kuwepo kwa uhusiano wowote kati yake na lugha ya Kimaasai bali imeteuliwa kama kigezo tu cha lugha ambayo mnyambuliko wa vitenzi umeshughulikiwa sana. Katika utafiti wowote ule ni kawaida kuanza kutoka kile kinachojulikana hadi kile kisichojulikana.

**2:1.3 Tafiti kuhusu lugha ya Kimaasai**

Kumekuwa na kazi kadha wa kadha za msamiati na maelezo ya kisarufi ya lugha ya Kimaasai. Wamishenari Ludwing Krapf na Erhardt waliandika *'Enkutuk Ooloikop'* (lugha ya Iloikop) kati ya mwaka 1854 na 1857. Kazi hii ilihusu kuorodhesha na kutoa maana ya maneno kutoka nyanja tofauti za maisha ya kila siku kama vile ufugaji, mimea, nyumbani na kadhalika.

Miongoni mwa kazi za awali ambazo zilitoa maelezo muhimu kuhusu sarufi ya lugha ya Kimaasai ni kama ile ya Hollis (1905).

Baadaye hatua kubwa ilipigwa mwaka wa 1954 wakati Tucker na Mpaayei walichapisha kazi iliyoshughulikia isimu ya lugha hii kwa undani zaidi – *'A Maasai grammer with vocabulary.'* Hii ilikuwa kazi ya sarufi iliyozingatia muundo wa sentensi na kuumudu msamiati wa lugha ya Kimaasai.

Tatizo la kazi hii ya Tucker na Mpaayei ambalo lilizua mjadala mkubwa miongoni mwa *wanaisimu wenzao wakati ule lilikuwa ni matumizi ya alama / ŋ/* ya kifonetiki badala ya ng' ya kiothografia. Kazi zilizoandikwa kuanzia mwaka wa 1955 ziliandikwa na Wamishenari waliotaka kuwasaidia wamishenari wenzao kuimudu lugha ya Kimasaai katika harakati zao za *kueneza Ukristo. Katika mwaka wa 1955 Ruth Shaffer aliandika 'Twelve lessons in Maasai'.* Kazi hii ilikuwa imepangwa kivipindi kwa namna watoto wanavyofunzwa lugha ya Kiswahili katika darasa la malezi au la kwanza.

Katika mwaka huohuo Shaffer aliandika *'Maasai Vocabulary'* kwa mtindo wa kamusi. Kazi zingine za kisarufi zilizoandikwa ni kama ile ya *'Church Missionary Society's Maasai Basic course'* ya kurasa 86 za dialojia ya kuwasaidia waliotaka kujifunza Kimaasai. Englin na Lorna (1975), waliandika *'A Maasai Grammar for Beginners'* iliyokuwa na masomo 60 ya Kimasaai na mitihani kwa kila somo sawa na kazi iliyoandikwa na Shaffer (1955).

Kasisi Frans Mol naye katika mwaka wa 1979 aliandika kamusi; *'Maa- A Dictionary of the Maasai Language and Folklore: English – Maasai* ya maneno ya Kiingereza yaliyoorodheshwa kiabjadi na visawe vyake kutolewa kwa Kimaasai. Mol pia ameonyesha mipaka ya silabi, mpumuo na vibadala vya maneno. Katika kurasa zake za utangulizi, Mol ametoa muhtasari mfupi wa viambishi vichache vya mnyambuliko wa vitenzi. Hata hivyo, katika kamusi yake hajatoa maelezo na mifano ya jinsi minyambuliko hii inavyojitokeza katika vitenzi vya lugha hii.

Kazi hizi zilikuwa msingi na kielelezo kizuri cha utafiti wa lugha kwa kutoa maelezo na vidokezo vya kijumla *kuhusu miundo na maana ya maneno* katika lugha hii. Utafiti huu unalenga kuendeleza kazi hizi za awali kwa kushughulikia kwa kina zaidi mnyambuliko wa vitenzi katika lugha hii.

**2.2 Msingi wa Nadharia**

Msingi wa nadharia wa utafiti huu ni nadharia za Wanamuundo:

Ya kwanza ikiwa ile iliyoasisiwa na Hockett (1958) na ya pili ni Sarufi Zalishi Geuza Umbo iliyoasisiwa na Chomsky (1957) na kuendelezwa na wanaisimu wengine kama vile Hockett (1958), Lees (1960), Anderson (1992) na Dressler (1990) miongoni mwa wengine.

Nadharia ya Hockett ina mikabala mitatu; kipashio na mpangilio, vielelezo vya maneno, na *kipengele na mfanyiko*. *Mkabala wa* ***kipashio na mpangilio*** huchukulia neno kama mpangilio au mfuatano wa mofimu katika mstari. Mkabala huu huchukulia mofimu kama kipashio cha kimsingi na huelezea vipashio na mpangilio kama ulivyo katika tungo. Maelezo hutolewa *kuhusu maumbo ya mofimu zinazojitokeza.*(Hockett 1958). Sentensi '*tulimfumania mwizi*' kwa mfano, itakuwa *tu/li/m/fuman/ia/ mwizi.*

Tatizo kubwa lililoukumba mkabala huu ni jinsi ya kuelezea vibadala vya mofimu au mofu zilizofungamana katika neno moja, kwa mfano, katika maneno ya kingereza, *sing - sang, take - took, sheep -sheep* (Spencer 1991:49), ambapo dhana ya wakati au wingi haziwezi zikatambulishwa kwa mofimu mahsusi. Katika lugha nyambulishi kwa 'mfano, mofimu katika *maneno mengi huadhiriana na kufungamana hivi* kwamba *ni* vigumu kuzitambulisha mojamoja katika neno. Hata hivyo mkabala huu umekuwa mwongozo mzuri kwa mtafiti katika kuzibainisha mofimu nyambulishi katika maneno.

Mkabala wa **vielelezo vya maneno** nao una misingi yake katika sarufi za jadi za Kilatini na Kiyunani. Kielelezo ni seti ya maumbo ambishi yanayotokana na neno moja. Katika mkabala huu neno ndilo kipashio cha kimsingi cha kisarufi. Mkabala huu hutambua kuwepo kwa mpaka kati ya mofolojia na sintaksia, mofolojia ikiwa ni muundo wa maneno na sintaksia ikiwa muundo wa sentensi. Neno hapa linakuwa kipashio kilicho huru na dhabiti. Maumbo ya maneno yenye mizizi au mashina yanayofanana yanawekwa katika kielelezo kimoja au zaidi.

Jamii za vielelezo ni kama zile zinazoonyesha kategoria za kimofosintaksia'kama vile idadi, uana, nyakati au hali. Mifano wa vielelezo katika Kiingereza ni kama zile za wingi wa maneno '*sea*' na '*man*';

| (1) | SEA | MAN | |
|---|---|---|---|
| Umoja | *sea* | *man* | |
| Wingi | *seas* | *men* | (Mathews 1974:38) |

Mfano wa vielelezo katika lugha ya Kihagari ni kama vile vya kuambisha kihusishi au vivumishi katika neno *'szoba'* (chumba); (Spencer 1991:57).

| (2) | Umoja | | wingi |
|---|---|---|---|
| *Szoba* | chumba | *szobak* | vyumba. |
| *Szobaban* | chumbani | *szobakban* | vyumbani. |
| *Szobam* | chumba changu | *szobaim* | vyumba vyangu |
| *Szobank* | chumba chetu | *szobaink* | vyumba vyetu |

Mnyambuliko wa vitenzi katika jinsi mbalimbali katika lugha ya Kiswahili ni mfano mzuri wa uundaji wa vielelezo vya maneno. Kwa mfano vielelezo vya neno *nawa, choma* na *pika;*

(3) *Nawa, nawia, nawisha, nawika*

*Choma, chomea, chomesha, chomeka*

*Pika , pikia , pikisha, pikika,upishi, mpishi.*

Matumizi ya maneno kama kipashio cha kimsingi huepuka matatizo ya kuelezea sifa za kimofosintaksia au tatizo la mofimu-kapa kwani sifa za kimofosintaksia huenea katika umbo la neno zima. (Malmkjaer 1991: 322).

Mkabala wa vielelezo vya maneno ni muhimu sana katika kuchunguza mnyambuliko wa vitenzi kwa kuwa umemsaidia mtafiti kupanga maumbo mbalimbali ya vitenzi yanayotokana na leksimu asilia katika vielelezo.

Mkabala wa **kipengele na mfanyiko** uliibuka kutokana na matatizo yaliyoukumba mkabala wa kipashio na mpangilio nao huhusisha vipashio na vingine kwa kurejelea mifanyiko ya kimofolojia. Mkabala huu umejikita katika misingi kwamba mofimu za lugha huathiriana kwa namna inayozifanya zibadilishe maumbo yao na umbo la neno zima.

Kwa mfano, neno *'olchani'* (mti) la Kimaasai linahusiana na *'ilkeek'* (miti) kwa mfanyiko wa *ablaut* kwa kubadilika kwa irabu na konsonanti za shina.

Neno *'man'* la Kiingereza pia hubadilika kuwa *'men'* kwa mantiki hiyohiyo. Mkabala huu pia huchukulia *mofimu (badala ya neno) kama kipashio cha kimsingi cha sarufi*. Jambo hili huondolea mbali mpaka kati ya mofolojia na sintaksia. Katika mkabala huu, kila mofimu huwa na umbo lake la kimsingi ambalo huadhiriwa na mifanyiko (Lass 1984), jambo linaloibua *miundo na maana tofauti ya neno linalohusika*. Kwa mfano, katika kielelezo cha neno la kimaasai *a-i-bung'* (kushika) linaponyambuliwa huwa hivi :

(4) (i) *I-m-bung'-a!* - Shika!

(ii) *E-m-bung'-aki* – shikieni!

(iii) *Ki-m-bung'-ie / Ki-m-bung'-akinye* - tutashikisha/ tutashikisha kwa.

(iv) *e-m-bung'-ata* - shikaneni

(v) *m-bung'umbung'-a* - shikashika

(vi) *enk-i-bung'-ata* - kushika – kitenzi-jina; ngeli ya /Ku/

Katika kielelezo hiki, (ii), (iii), na (iv) vinahusu mnyambuliko sarufi, (v) ni mnyambuliko wa uradidi na (vi) *ni mnyambuliko geuzi*.

Kulingana na mkabala huu, wakati mwingine dhana kama vile wingi au wakati huwa ni mfanyiko na wala sio umbo. *Mifanyiko* mingine *ni* kama vile uradidi wa neno *guru* (mwalimu) kuwa *guruguru* (walimu) katika lugha ya Malay, kuambatanisha katika *mwanahewa* la Kiswahili, tofauti ya mkazo katika *esho'mo* (ameenda) na *e'shomo* (wameenda) la kimaasai *na mifanyiko mingine ya uundaji wa maneno*.

Mkabala huu nao uliteuliwa kwa misingi kuwa ni jinsi mojawapo ya uundaji wa maneno na maana mpya katika lugha. Ni mkabala uliomsaidia mtafiti kuelezea maenezi, dhima na athari ya mofimu nyambulishi katika vitenzi vya lugha ya Kimaasai. **Nadharia ya Sarufi Zalishi Geuza Umbo** ni nadharia ambayo imekuwa na mabadiliko kadha wa kadha tangu kuasisiwa kwake hadi miaka ya themanini ilipopata mtazamo wa kisasa. Mwasisi wa nadharia hii ni Noam Chomsky (1957), ikaendelezwa na wataalam wengine kama vile Hockett (1958), Dressler (1990), na Spencer (1991) miongoni mwa wengine. Wanasarufi Geuza Umbo wa awali walichukulia *sintaksia kama mfululizo wa kisarufi* wa mofimu katika lugha, mofolojia haikuchukuliwa kama kiwango huru cha uchanganuzi wa kiisimu. Fonolojia na sintaksia ndivyo vilivyokuwa misingi ya uchanganuzi wa Kiisimu.

Katika miaka ya sabini dhana ya fonolojia leksia iliibuliwa, jambo lililochangia kuimarishwa kwa mofolojia kama eneo huru la uchanganuzi wa kiisimu.

Kwa mujibu wa mtazamo huu, sheria za uundaji wa maneno ndizo sheria za kuzalisha maneno *na huhifadhiwa katika kamusi kwa sababu zinapatikana katika maneno* husika. Mamkjaer (1991) anaiona kamusi kama seti ya mofimu pamoja na mifanyiko mbalimbali ya uundaji wa maneno; na kuwa uundaji wa maneno ni utendakazi katika msamiati wa lugha.

Katika miaka ya Themanini wanaisimu walijaribu kuuondoa mpaka uliopo kati ya uambishaji, unyambuaji na uambatanishaji na kuchukua hatua zaidi ya kuiweka mifanyiko hii katika eneo la kisarufi la mofolojia.

Fonolojia leksia huchukulia msamiati kama kipengele muhimu cha sarufi. Hii ni kwa sababu msamiati una sheria za uundaji wa maneno, fonolojia na pia ule upekee wa neno na mofimu (*idiosyncratic properties*). Sheria za uundaji wa maneno za kimofolojia huambatana na kutenda kazi pamoja na sheria za kifonolojia katika viwango tofauti tofauti ili kuzalisha neno. Msamiati kwa hivyo ni matokeo ya sheria za kimofolojia na kifonolojia zilizowekwa pamoja. (Spencer 1991;79-80)

Katika Sarufi Zalishi Geuza Umbo, kipengele cha kimsingi cha kisintaksia hujumuisha muundo ndani ambao hubeba maana na ambao huhusishwa na muundo nje kwa kutumia ugeuzaji. Muundo nje hapa huchukuliwa kama mfwatano wa mofimu (maumbo) ambayo hufanyiwa kazi na sheria za kifonolojia ili kuunda maumbo mapya. Kando na sheria hizi za kifonolojia pia kunahitajika msamiati (*lexicon*) ambao ni sifa za Kimaumbo na za kifonolojia ambazo haziwezi kuzalishwa kwa sheria. Maumbo huadhiriwa na mifanyiko katika miktadha mahsusi na usawiri wake kileksia lazima uwe umbo la kijumla linaloshabihi kwa kiwango maumbo ya awali. Matokeo ya utendakazi huu huchukua sifa za kimofolojia na kifonolojia na kwa hivyo ni wa kimofonemiki. Sheria hizi huchukua umbo lifwatalo;

A > B / C ---------- D

Ambapo,

A ni umbo la kipengele asilia,

B ni umbo la kipengele baada ya athari.

C na D ni mazingira.

Mstari *ni nafasi ya kipashio* A.

Kwa mfano neno la Kiingereza *bead* katika wingi huwa *beads*. Kifonetiki ni [bid]/ [bidz]. Mofimu [s] ya wingi hutamkika kama [z]; Mabadiliko haya yametokana na sheria ifuatayo;

[s] > [z] / /d/ ---------

Sauti /s/ *hubadilika na kuwa /z/ katika mazingira yanayofuata sauti ghuna.*

Neno la Kiswahili *pika* linaponyambuliwa kuwa *mpishi,* sheria inayoongoza mabadiliko *haya ni kuwa,* kwanza *tungetarajia mpishi* liwe *mpiki,* ambalo ndilo muundo ndani. Lakini, sauti /k/ ya kaakaa laini inasimilishwa na vokali /i/ ya mbele inayoitangulia na kuifuata kwa kuivuta mbele na kuilazimisha itamkike kama kikwamizo /ʃ/ cha kaakaa ngumu. Hii ndiyo sababu inayoifanya sauti /k/ kubadilika kimaeneo na kiumbo. Muhtasari wa sheria hii ni kama ifwatavyo;

[k] > [ʃ] / /i/ --------- /i/

Sauti /k/ hubadilika na kuwa / ʃ / katika mazingira kati ya irabu /i/ za mbele.

Kando na usimilisho na ubadilishaji wa faridi, mifanyiko mingine itahusu uchopekaji, uhamishaji, *udondoshi, unasalishaji na mingineyo.* Misingi ya ugeuzaji umbo upo katika sifa pambanuzi za fonimu na ule upekee wa baadhi ya maneno na mofimu katika lugha.

Umuhimu wa nadharia hii ni kuelezea yàle mabadiliko ya kimaumbo na kimaana yatakayotokea kutokana na kuwepo kwa umbo au mfanyiko wa unyambuaji katika vitenzi vya lugha ya Kimaasai.

Mapitio ya maandishi yaliopo hasa ya lugha ya Kimaasai yalidhihirisha hali ya kutokuwepo kwa *utafiti* wa kutosha katika *lugha hii na lugha za nailotiki* kwa jumla. Mojawapo ya mapengo yaliyodhihirika ni ukosefu wa maelezo ya kutosha kuhusu mnyambulikowa vitenzi. Sura ifuatayo ilitoa ruwaza au mbinu zilizotumika katika utafiti huu ili kuliziba pengo hili.

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza kwa ujumla kuhusu ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Mtafiti ameelezea jinsi alivyoikusanya data, uteuzi wa sampuli na mwisho jinsi data ilivyochanganuliwa.

### 3.2 Ukusanyaji wa data

Ili kuipata data aliyoihitaji mtafiti, ilimbidi azingatie mambo mawili; kwanza mahali pa utafiti na sampuli ambayo ingewakilisha vitenzi vyote vya lugha ya Kimaasai.

### 3.2.1 Mahali pa utafiti

Utafiti huu Kwa kiwango fulani ni utafiti wa maktaba ambapo mtafiti alichanganua matini za fasihi simulizi zilizoandikwa zinazohusu lugha ya kimaasai. Kwa upande mwingine, ilimbidi aende nyanjani na kama ilivyotajwa hapo awali kwamba utafiti ulijikita katika kimaasai kinachozungumzwa katika eneo la Suswa, Mosiro, na Ilkerin-loita wilayani Narok, mtafiti alichanganua mazungumzo mengine ya kawaida ya lahaja ya Kimaasai inayozungumzwa katika sehemu hiyo. Kwa mintarafu hii, alitumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliomo.

Yaliyomo yaliyokuwa msingi wa kupata vitenzi yalikuwa ni vipera vya fasihi simulizi kama vile nyimbo, methali na hadithi. Nyimbo kumi na tano, methali hamsini na hadithi kumi na moja zilichanganuliwa. Vipera hivi vya fasihi vilipatikana kutoka kazi za Kipury (1984) na Sankan (1971), sherehe mbili za tohara alizohudhuria mtafiti mwezi wa Disemba 2007 katika eneo la Mosiro na kutoka kumbukumbu za masimulizi na mafundisho ya tangu utotoni ya nyanya mkongwe Bi. Kiramatisho. Nyimbo zinginezo zilizokuwa msingi wa kupata vitenzi zilipatikana kutoka katika mikutano ya kisiasa ambazo ziliimbwa katika eneo lote la utafiti kusifu na kukejeli katika mikutano ya kampeni za uchaguzi kati ya Oktoba na Disemba 2007. Deta zaidi ya vitenzi ilipatikana kutoka kalimani moja, Mchungaji David Maitoyo Ole Leseyio aliyetafsiri mahubiri ya kanisa la S.D.A mwezi wa Oktoba 2007 katika soko la Olasiti suswa.

Kuhusu mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo, Schiffrin anaifananisha dhana ya 'yaliyomo' na matini anaposema;

'Nitalitumia neno 'matini' ili kutofautisha dhana za kiisimu (kwa mfano, kile *kinachosemwa katika usemi) na muktadha wa ule usemi.* Matini kwa hivyo ni yale 'yaliyomo kiisimu' Schiffrin (1994; 363) (Tafsiri yangu).

Mbinu hii hutafuta ufahamu kwa kutambulisha kwa mfumo bila upendeleo sifa bainifu za matini mbalimbali kama vile *matamshi yaliyotamkwa au taarifa zilizoandikwa* kama barua, vitabu au magazeti.

Badala ya mtafiti kutazama mienendo ya watu moja kwa moja au kuwauliza maswali kuhusu maisha yao, *mtafiti huchukua yale mawasiliano yaliyopo au* yaliyotayarishwa na watu wengine na kuuliza maswali kuhusu mawasiliano hayo. Yaliyomo katika mawasiliano hayo yanakuwa msingi wa kupata ufahamu (Nachmias 1992: 96, Holsti 1968: 601).

Uchanganuzi wa yaliyomo ni mbinu ya kuchunguza kwa kutazama na kwa sababu hiyo katika tafiti zingine hutumika kama njia ya majaribio.

Pia ni mbinu ya uchanganuzi wa data. Kwa mintarafu hii, ni mbinu ambayo ilimfaa mtafiti katika kiwango cha ukusanyaji wa data ya vitenzi kutoka katika vipera vya fasihi simulizi na pia katika kiwango cha uchaganuzi wa data ile ili kupata mofimu za mnyambuliko, maana na maumbo mbalimbali yanayotokana na mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kimaasai.

### 3.2.2 Uteuzi wa sampuli

Data ya utafiti huu ni vitenzi asilia vya lugha ya Kimaasai vilivyoteuliwa kimakusudi kutoka katika mawasiliano ya kawaida na pia kutoka vipera mbalimbali vya fasihi simulizi ya lugha hii. Jumla ya vitenzi mia sita viliteuliwa kwa misingi kuwa ni kiwakilishi mwafaka cha vitenzi vyote vilivyopo na kuwa ingewakilisha minyambuliko yote ya vitenzi vya lugha hii. Katika kutafiti, mtafiti alipata vitenzi ambavyo tayari vimenyambuliwa katika namna mbalimbali kulingana na jinsi vilivyotumika katika nyimbo, hadithi methali au mazungumzo. Utafiti huu ulijihusisha na vitenzi vikuu pekee. Hii ni kwa sababu vitenzi visaidizi haviwezi kunyambuliwa. Vitenzi vilitambulishwa kimaksudi na kuorodheshwa kufuatia vielelezo vifwatavyo.

Katika wimbo na methali zifuatazo, vitenzi vimeandikwa kwa herufi za mlazo na katika tafsiri ya Kiswahili vitenzi vile vimeandikwa kwa mnyambuliko uleule uliopo katika nakala ya lugha ya Kimaasai.

Mfano wa ukusanyaji wa data kutoka katika wimbo:

*Wimbo wa wanawake wa kumwomba Mungu awape watoto.*

| | | |
|---|---|---|
| (5) | *Kimaasai* | *Kiswahili* |
| | Parsae *tadamu* ena sile | Ee mungu *kumbuka* deni hili |
| | Esile *nemelaayu* too nkishu | Deni *lisilolipika* kwa ng'ombe |
| | *Nemelak* inkiku *nadung'u* | Matawi *nikatayo hayalilipi* |
| | *Nemelak* enkare *naoku* | Maji nimchoteayo *hayalilipi* |
| | *Nemelak* olumbwani *ladoiki* | *Kuingia* kisimani *hakulilipi* |
| | *Elaki* te Enkerai oltung'ani | Ni mwana tu *alilipaye* |

Kiitikio

| | |
|---|---|
| Hoyiayio ehoo, hoyiayio | Hoyiayio ehoo, hoyiayio |
| *Ayok* ayooki Enkai ai | *Namwendea* Mungu asubuhi |
| Enkai *nasai atasaia* | Ee Mungu *unayeombwa nakuomba* |
| *Naasai* too naishi o te kule | *Naomba* kwa pombe na maziwa |
| *Toning'u naanare* etuumate | *Sikiliza yawafaayo* wanawake |
| Enare nebarni olmasi onyil | *Wanyoe* nywele zenye mafuta |
| Osidai *obarnieki* kule | Nzuri *kunyolewa* kwa maziwa |
| | |
| Patim ai *nailejilej nemaing'ode* | Mpendwa *nimbembelezaye simkaripii* |
| Nkatambo Enkai *aimariri* | Mawinguni kwa Mungu *natazama* |
| Pee te ndorrop *aisho* nosim ai | Ili kwa kifupi *anipe* mwana |
| Nanyorr ai pee *aitotioki* . | Mpendwa wangu kwa ajili yako *nimelishwa* |
| *Atijing'a* olpul anaa ilmurran | *Nimeingia* lishe ya nyama kama vijana |
| | |
| *Aateyiang'akaki* Ololtuala sidai | *Nilichinjiwa* fahali mwenye kengele |
| *Oloseken* olopeny *neimanyie* | Mwenyewe *amthaminiye* hata *kumwapia* |

| | |
|---|---|
| Meeta *enanyorri* inkishu ang' | Hamna ng'ombe wetu *anayependwa* zaidi |
| *Aitotie* nosim ai indaiki supati. | *Nitamlisha* mpendwa vyakula bora |

(Kipury, N. 1984: 205)

Katika wimbo huu mtafiti alidondoa vitenzi vifuatavyo

(6a) *Ta-dam-u* - kumbuka.

*Ne-me-la-ayu* - lisilolipika.

*Ne-me-lak* - halilipwi.

*E-lak-i* - litalipwa.

*La-dok-i* - niingiacho.

*Na-ok-u* - nichotayo.

*Na-dung'* - nikatayo

*A-yok* - najia asubuhi.

*A-ta-sai-a* - naomba.

*E-nar-e* - yafaa.

*Ne-barn-i* - wanyolewe.

*Ne-barn-ieki* - nyolewa kwa.

*Na-ilejilej* - bembelezabembeleza.

*Ne-ma-i-ng'od-e* - nisiyekaripia.

*A-imarir-i* - natazama juu.

*A-aish-o* - anipe.

*A-i-tot-ioki* - nimelishwa.

*A-ti-jing-a* - nimeingia.

*Ol-o-seken* - amthaminiye.

*Ne-imany-ie* - Kumwapia – kuapa kwa.

*A-a-te-yang'-akaki* - nilichinjiwa.

Mfano wa ukusanyaji wa data ya vitenzi kutoka katika methali;

(6b) *Mengasunoyu* olkesen etioyo enkerai. - *Haitanguliki* nguo kabla mtoto

*Mesarunoyu* oltau *oipurupure.* - *Haunusuriki* moyo uliochafuka.

*Mikiarr* eitu *kirorie.* - *Usinipige* kabla *kunisemeza.*

*Edoorie* enkerr modooni inkuta. - *Hupata* kondoo kipofu maji*

*Misujaki* imirat entim. - *Usifuatie* ushindi mwituni.

*Mimulumulaki* osoit emodiei. - *Usifunikiefunikie* jiwe samadi.

Mijo *maipirata ilemeishiakino*. – Katu *hawalingani wasiofaana*.

(Sankan, S. 1971: 77-83)

*Orodha ya vitenzi*

(6c) *Me-ng'as-unoyu* - haitanguliki.

EGERTON UNIVERSITY LIBRA

*Me-sar-unoyu* - hainusuriki.

*O-ipurupur-e* - iliyoingia mchanga.

*E-door-ie* - hufika.

*Mi-ki-ar* - Usinipige.

*Ki-ror-ie* - Kunisemesha.

*Mi-suj-aki* - usifuatie.

*Mi-mulumul-aki* - Usifunikefunike.

*Sentensi hii sio sahihi kulingana na sintaksia ya lugha ya Kiswahili; imeandikwa kwa kufuata sintaksia ya lugha ya Kimaasai. Katika lugha hii kwa mfano, sentensi 'Meitamei *anakunywa*. maziwa' itafuata mfumo '*Anakunywa* Meitamei maziwa'* yaani '*Eokito* Meitamei kule.'

Sentensi hii ikiandikwa kwa mpangilio wa kiima – kitenzi – kiiarifa yaani 'Meitamei *eokito* kule'* basi katika Kimaasai sentensi ile sio sahihi. Tazama ukurasa wa 34 kwa maelezo zaidi ya sintaksia ya Kimaasai.

*Ma-i-pir-ata* - lingana.

*I-le-me-i-shiak-ino* -Wasiofaana.

Kutoka katika nyimbo, methali, hadithi na mazungumzo ya kawaida mtafiti aliweza kukusanya orodha ya vitenzi mia tatu ambavyo alivitumia kutimiza malengo ya utafiti huu; kwanza, *kubainisha* mofimu nyambulishi katika vitenzi vya Kimaasai, na pili, *kutambulisha* maumbo na maana zinazotokana na mnyambuliko wa vitenzi wa lugha hii.

**3.3 Uchanganuzi wa data**

Uchanganuzi wa vitenzi vilivyokusanywa ulilenga kwanza, kutambulisha muundo wa vitenzi vya lugha ya Kimaasai kifonolojia na kimofolojia.

Pili, kubainisha mofimu za mnyambuliko iliyopo katika vitenzi hivi na tatu kutambulisha maana na maumbo yanayotokana na minyambuliko hiyo.

Kama ilivyotajwa hapo awali mbinu ya uchanganuzi wa data iliyotumiwa ni *uchanganuzi wa yaliyomo* huku ikiongozwa na mikabala miwili ya wanamuundo ya Vielelezo vya Maneno na Kipengele na Mfanyiko. Mabadiliko ya umbo na maana yameelezewa kwa misingi ya nadharia ya Sarufi Zalishi Geuza Umbo. Mofimu za mnyambuliko zimeainishwa kwa kuvipanga vitenzi katika vielelezo vinavyoonyesha aina mbalimbali za mnyambuliko wa vitenzi. Utambulishaji wa maana na maumbo yanayotokana na mnyambuliko umefanywa kwa kutoa maelezo kuhusu dhima, maenezi na athari ya mofimu hii kwa muundo na maana ya kitenzi kizima. Pia sheria mbalimbali zinazotawala minyambuliko hii zimeelezewa. Muhtasari wa mofimu za Mnyambuliko umetolewa katika ukurasa wa 97. Baada ya kuvipanga vitenzi katika vielelezo, mtafiti sasa alichukua hatua ya kutambulisha zile mofimu zote zilizoambishwa katika *mizizi ya vitenzi*. Ilibainika kwamba *mizizi* ya vitenzi vya lugha ya Kimaasai ina uwezo wa kuchukua mofimu tofautitofauti ili kupanua au kubadili maana ya vitenzi vile. Mofimu zilizokuwa katika vitenzi mbalimbali zilipangwa kwa kufuata kielelezo kifuatacho kutoka Chai 2002: 87;

| -3 | -2 | -1 | 0 | +1 | +2 | +3 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kikanushi | Nafsi | wakati | Mzizi | Mnyambuliko | kiishio | |
| | | | | | | |
| - | a | te | lej | - | a | (nilimdanganya) |
| - | i | te | lej | akinot | e | (mlidanganyiana) |
| mi | ki | Φ | lej | ish | o | (hatudanganyi) |

Lengo la kuvipanga viambishi hivi ni kumwezesha mtafiti kutambulisha mofimu ya mnyambuliko miongoni mwa mofimu zingine katika kitenzi.

Kwa mfano, katika vielelezo hivi vichache, inadhihirika kuwa mofimu mahsusi zinaashiria mnyambuliko tofautitofauti: Kwa mfano, hali ya kutendea iliyo na maana mbili inawakilishwa na seti mbili za mofimu; maana ya tendea ya *niaba ya* inawakilishwa na mofimu /ki/ mwishoni mwa kitenzi ilihali *tendea kwa (ala tendea / kutumia kitu)* huwakilishwa na mofimu {ie}, {-kinye} au {ye}.

Baadhi ya minyambuliko hutokea mwanzoni na mwishoni mwa vitenzi.. Minyambuliko mingine nayo hudhihirisha *ulinganifu* wa *irabu*, *ilihali mingine ni udodndoshi* na uchopekaji. Minyambuliko hii yote na maana zinazojitokeza imeelezewa na kutolewa mifano ya kutosha katika sura ifuatayo.

Sheria za uchopekaji, *ubadilishanaji* wa *fonimu na irabu*, na *sheria* zinginezo za kimofonemiki pia zimetambulishwa na kuelezewa. Kwa mfano, katika kielelzo cha kitenzi *adung'* linalomaanisha 'kukata' na lenye kibainishi {*a*} ambacho ni kisawe cha {ku} cha Kiswahili na *mzizi –dung'*;

*a-dung'* (ku-kata)

*a-dung'-ie* (ku-kat-ia) Mofimu –ie ya kutendea inachopekwa mwishoni.

*-dung'-i* (kat-w-a) Mofimu ya kutendwa –*i* inachopekwa mwishoni.

*-dung'-okini* (kat-iw-a) Mofimu ya kutendewa –okini inachopekwa mwishoni na hufuata ulinganifu wa irabu. Huwa –*akini ikiwa mzizi* una *irabu* ya *mbele*.

*a-dung'-oyu* (kat-ik-a) Mofimu –oyu ya kutendeka huchopekwa mwishoni. Pia yaweza kuwa –ayu katika mizizi yenye irabu ya mbele.

*ntu-dung'-o* (kat-ish-a) - hali *rai*. Mnyambuliko wa *jinsi* ya kutendesha unaohusu uchopekaji awali na huwakilishwa na mofimu nt-, au mp- huku ikichukua irabu kutegemea ile ya mzizi.

*aa-dung'-o* (kukat-an-a) Mofimu -o ya jinsi ya kutendana pia huchopekwa mwishoni. Mofimu hii huwa –a katika mizizi yenye irabu za mbele.

*entu-dung'-oto!* (kat-an-eni!) – Mofimu awali entu- ni amri au rai kwa watu zaidi ya mmoja. -oto ya kutendana huchopekwa mwishoni na yaweza kuwa –ata katika mizizi yenye irabu za mbele.

*e-tu-dung'-ote* (wa-li-kat-an-a) Mofimu *e-* ni nafsi ya tatu katika wingi, *-tu-* ni wakati uliopita, ilihali -ote *ni* nafsi ya kutendana katika wakati *uliopitana* huchopekwa mwishoni.

*a-dung'udung'* (ku-katakat-a). Huu ni mnyambuliko radidi unaohusu kurudiwa kwa mzizi. Irabu inayounganisha mzizi uliorudiwa hutegemea kama ile iliopo kwenye mzizi ni ya mbele au ya nyuma.

Kitenzi *Tu-dung'udung'-o!* (katakat-a!) ni cha hali rai ambapo mofimu *–tu-* ni rai kwa nafsi ya pili (umoja).

*en-dung'-oto* (Mkato) ni mnyambuliko geuzi ambapo mofimu *en-* ya jinsia ya ukike imeambishwa. *–oto* ya tamati yaweza kuwa *–ata* ikiwa irabu ya mzizi ni ya mbele. Dhana ya mofimu za jinsia zimeshughulikiwa kwa kirefu katika sura ya tano.

Kwa muhtasari basi hatua zilizofuatwa katika uchanganuzi wa data ni vinginevyo.

ii. Kubainisha mnyambuliko katika vitenzi.hizi;

i. Kubanisha vitenzi katika nyimbo,methali, hadithi na vitanzu.

iii. Kuainisha aina za mnyambuliko.

iv. Utambulishaji wa maana na maumbo / kutambua mofimu za mfanyiko.

v. kubainisha sheria zinazotawala kila aina ya mnyambuliko.

**3.4 Vikwazo vya Utafiti**

Wamaasai wana koo zaidi ya ishirini zilizotapakaa nchini Kenya na Tanzania na kutumia lahaja zisizopungua kumi. Kiwango cha tofauti za kimsamiati huongezeka kulingana na jinsi lahaja moja ilivyo mbali na ile nyingine. Kwa sababu ya ukubwa wa eneo wanaloishi Wamaasai mtafiti hakuweza kuikusanya data kutoka lahaja zote isipokuwa tu ile ya Kimaasai kinachozungumzwa katika eneo la kati la Bonde la Ufa, ambacho ni lahaja inayozungumzwa na Ilkeek-onykie, purko, Iloitai na Ildamat. Kuna haja ya utafiti mwingine unaoelezea tofauti za kimsamiati kati ya lahaja hizi zote. Tofauti za kilahaja ni dhana iliyo nje ya upeo wa utafiti huu. Sura ifuatayo inajihusisha na utekelezaji wa madhumuni ya kwanza ya utafiti huu ya kutambulisha muundo wa vitenzi vya Kimaasai kifonolojia na kimofolojia.

# SURA YA NNE

# MUUNDO WA VITENZI VYA KIMAASAI KIFONOLOJIA NA KIMOFOLOJIA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea isimu ya Vitenzi vya lugha ya Kimaasai katika viwango vya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia na kwa hivyo ililenga kutekeleza madhumuni ya kwanza ya kutambulisha muundo wa vitenzi vya Kimaasai kifonolojia na kimofolojia. Sura yenyewe imegawika katika sehemu tatu; ya kwanza imeshughulikia vitamkwa vya lugha ya Kimaasai, ya pili inaelezea muundo wa vitenzi vya lugha ya Kimaasai na ya tatu nayo ilishughulikia sintaksia ya lugha hii. Ingawa utafiti huu ni wa kimofolojia viwango hivi vingine vya uchanganuzi vimeshughulikiwa kwa kuwa dhana ya mofolojia ni mfumo wa mahusiano kutoka maeneo tofauti tofauti ya kiisimu kama vile fonetiki, fonolojia, sintaksia, semantikia na hata pragmatiki. Katu haiwezekani kuyajadili maswala ya kimofolojia ya lugha yoyote bila kuwa na ujuzi wa fonolojia na sintaksia ya lugha ile. Mofolojia ya vitenzi imeelezewa kwa kutambulisha viambishi mbalimbali vinavyoweza kufungiliwa katika vitenzi vya lugha hii. Sura hii ina umuhimu mara mbili; kwanza ujuzi wa fonimu za lugha kunamwezesha msomaji kuzitambua sauti mahsusi (fonimu) za lugha fulani zinazohusika katika mabadiliko ya kimofofonemiki. Ujuzi wa mofolojia unamwezesha msomaji kuzitambulisha mofimu mbalimbali zinazoweza kuambishwa katika kitenzi cha lugha ya Kimaasai; na hili litamwandaa msomaji kuweza kutambua mofimu ya mnyambuliko pamoja na umbo na maana yake. Swala hili hasa, ndilo uti wa mgongo wa kazi hii. Umuhimu wa sehemu ya tatu inayoelezea sintaksia ya lugha hii ni kumwezesha msomaji kuielewa mifano michache ambayo imetolewa kwa muundo wa sentensi. Mifumo ya kisintaksia hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine na inabidi msomaji auelewe mfumo wa Kimaasai lau kwa kiwango ili kuweza kuvitambua vitenzi katika sentensi.

## 4.2 Fonimu za lugha ya Kimaasai

Lugha ya Kimaasai ina jumla ya vitamkwa ishirini na tano; konsonanti ishirini na irabu/vokali tano.

### 4.2.1 Vokali

Lugha ya Kimaasai ina vokali tano ambapo kila moja ina alofoni mbili; vokali wazi na vokali funge. Tofauti iliopo kati ya vokali wazi na vokali funge ni kuwa vokali funge hutamkwa *kwa mpumuo* ilihali vokali wazi *hazina mpumuo* ila hutamkwa kwa ulaini zaidi.

Vokali funge ni kama vile;

(7a) /i/ katika neno a-rik (kuongoza) na *a-idik* (kushikanisha) na hutamkwa kama katika neno *seat* la Kiingereza au *pipa* la Kiswahili.

b. /ɛ/ katika *a-ilep* (kukwea) inayotamkwa kama katika neno *bell* la Kiingereza au *beba* la Kiswahili.

c. /a/ katika neno *olowuaru* (simba) au *paa* la Kiswahili.

d. /o/ katika neno *a-bobol* (kufungua ngombe kinywa) na *a-lo* (kuanika) kama ile ya neno *pot* la Kiingereza au *popo* la Kiswahili.

e. /u/ katika *a-bul* (kudunga) na hutamkwa kama katika neno *fool* la Kiingereza au neno *bundi* la Kiswahili.

Vokali wazi nazo ni kama vile;

f. /i/ katika *a-itirik* (kuchafua moyo) na hutamkwa kama katika neno *sit* la Kiingereza au lipa la Kiswahili.

g. /e/ katika *a-lep* (kukama) na *ene* (hapa) na hutamkwa kama katika neno *buff'ete* la Kifaransa au neno lea la Kiswahili.

h. /a/ katika *a-wal* (kujibu) inayotamkwa kama katika neno *tawala* la Kiswahili.

i. /o/ *a-bol* (kufungua) na hutamkwa kama katika neno *Roseau* la Kifaransa au *choma* la Kiswahili .

j. /u/ katika *a-bulu* (kumea) na *arum* (kutazama au kumjulia hali mgonjwa) hutamkwa kama katika neno *full* la Kiingereza au *dhuluma* la Kiswahili.

Vokali zaweza kuwa fupi au ndefu, kwa mfano katika maneno yafuatayo,

9a. *A-itil* (kaidi) na *-aitiil* (ng'aa).

b. *Tara* - ua na *taara* - chapa.

Katika lugha ya Kimaasai wakaa ni sifa bainifu ya kimofemiki.

Vokali mbili zaweza kuungana kuunda vokali unganifu au vokali ambatani ambazo ni irabu mbili katika silabi moja.Vokali hizi huwa hazina mpaka wa moja kwa moja kati yao, kilichopo ni hali endelezi kutoka vokali moja hadi nyingine, kwa mfano katika maneno yafuatayo;

c. *A-kuet* - kimbia.

d. *A-bau* -fika.

e. *Tua*! –kufa!

### 4.2.2 Konsonanti

Lugha ya Kimaasai ina konsonanti ishirini kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo;

Jedwali la IPA la konsonanti (1989) kutoka Habwe j. na Karanja P. (2004: 37)

| | Midomo | Midomo -meno | Meno | Ufizi | Kaakaa -gumu | Kaakaa -laini | Kilimi | Koo | Kongo -meo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipasuo | p b | | | t d | | k g | | | |
| Nasali | m | | | n | ɲ/ | ŋ | | | |
| Kikwaruzo | | | | s | ʃ | | | | |
| Kipasuo-kwamizo | | | ð | | dʒ | | | | |
| Kimadende | | | | r | | | | | |
| Kitambaza | | | | l | | | | | |
| Nusuvokali | w | | | | j | | | | |

Konsonanti /b/, /d/, /j/(y) na /g/ hutamkwa kama zinavyotamkwa katika lugha ya Kiswahili na hupatikana katika maneno kama vile; *abor* (kuumiza), *adaa* (kula), *ajeyu* (kuvimba) na *airrag* (kulala).

Kutamkwa kwa konsonanti /p/, /t/, /tʃ/ na /k/ hutegemea muktadha. Zinapopatikana mwanzoni na mwishoni mwa shina, sauti hizi hutamkwa kama zinavyotamkwa katika lugha ya Kiswahili.

Mifano ni kama vile katika maneno *a-por* (tambaa), *toiyo* (kauka), *ol-chani* (mti) na *ol-kikwei* (mwiba). Kwa upande mwingine, sauti hizi zinapopatikana katika mazingira katikati ya irabu mbili, basi huwa zinapata sifa ya mghuno ambapo /p/ hutamkika kama /β/, /t/ kama dh na sauti /k/ hutamkika kama gh.

Kwa mfano katika maneno yafuatayo;

10. emanyata (kijiji) hutamkika kama e-manyadha

t > ð/ v - v

*enaiposha* (ziwa) hutamkika kama *e-naiβosha*

p > β/ v - v

*kokoo* (nyanya) hutamkwa kama *koghoo*

k > / ð / v - v

Sauti hizi zinapotanguliwa na nasali /m/ na /n/, hutamkika kama sauti pamwe za kipua kama katika lugha ya Kiingereza.

Kwa mfano,

11. *E-mpuruo* - moshi

*E-nterit* - mchanga

*E-nkaji* - nyumba

*E-ngoro* - hasira

Nasali /m/, /ŋ/ na /ɲ/ pia hutumika kwa namna moja na inavyotumika katika Kiswahili.

Kwa mfano,

12. *A-mayian* - kubariki

*A-ning'* - kusikia

*E-muny* – faru

Nasali /ŋ/ nayo hupatikana kwa wingi katika lugha ya Kimaasai na hutumika kwa namna moja na inavyotumika katika neno *ng'oa* la Kiswahili. Kwa mfano katika neno *eng'eno* (hekima), *eng'ues* (mnyama-mwitu) au *eng'ony* (mshipa).

Sauti /s/, /ʃ/ na /l/ pia hutamkwa kwa namna sawa na Kiingereza au Kiswahili, kwa mfano katika maneno *tisila* (chuja), *ʔoosho* (piga) na *i-lang'a* (mulika).

Sauti /r/ nayo yaweza kutokea mara moja au zikiwa mbili katika neno na zinapotokea zikiwa mbili huwa zinapoteza sifa ya mghuno. Kwa mfano, katika neno *in-kera* (watoto), sauti /r/ ina mguno, lakini katika neno *in-kerra (Kondoo)*, hizo /r/ mbili zinapoteza mghuno.

Viyeyusho /y/ na /w/ navyo pia hutamkwa kama katika lugha ya Kiswahili. Sauti hizi hupatikana katika maneno kama vile *ayeu* (kutaka), *ayooki* (kuamkia mapema), *ilewa* (wanaume), na *ewang'an* (mwangaza).

### 4.3 Mofolojia ya vitenzi vya lugha ya Kimaasai

Vitenzi vya lugha hii huchukua muundo unaotegemea viambishi vinavyofungiliwa katika mzizi. Hii inatokana na msingi kwamba, vitenzi ni mojawapo wa makundi wazi ya kisarufi na kama ilivyo katika lugha zingine, mashina ya vitenzi vya lugha ya kimaasai yana ule uwezo wa kuchukua viambishi kadha wa kadha vyenye kupanua au kubadilisha maana. Kimsingi viambishi ni mofimu au vipashio vidogo zaidi vyenye maana kisarufi visivyoweza kugawika zaidi bila kupoteza maana. Viambishi hivi vyaweza kufungiliwa katika mazingira ya awali au ya tamati katika kitenzi kutegemea lugha husika. Mofimu zifuatazo ziliweza kubainishwa kutoka katika vitenzi vya lugha ya Kimaasai;

Kibainishi (KB)
Nafsi (NF)
Wakati (WK)
Mzizi (MZ)
Mnyambliko (MN)
Kirejeshi nafsi (tenda au tendwa) (KNF)
Kiishio (KI)
Wingi (WI)
Rai (R)
Mofu Tupu (MT)
Jinsia (J)
Ukanusho (UK)
Shina (SH)

| -3 | -2 | -1 | 0 | +1 | +2 | +3 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kikanushi | Nafsi | Wakati | Mzizi | Mnyambuliko | Kiishio | |

Maana zinazowakilishwa na viambishi hivi ni kama vile:

Kielelezo cha neno *a-pej* – ku-choma

*13. E-tapejo* - alichoma

| Nafsi | wakati | Mzizi | Mnyambuliko | Kiishio |
|---|---|---|---|---|
| *E* | *ta* | *pej* | - | *o* |

*Etapejoko* – alichomea

| Nafsi | wakati | Mzizi | Mnyambuliko | Kiishio |
|---|---|---|---|---|
| *E* | *ta* | *pej* | *ok* | *o* |

*Etapejokinote* – walichomeleana/walichomeana.

| Nafsi | wakati | Mzizi | Mnyambuliko | Kiishio |
|---|---|---|---|---|
| *E* | *ta* | *pej* | *okinot* | *e* |

*Etapejokinoteki* – wali-o-chomeleana / wali-o-chomeana

| Nafsi | wakati | Mzizi | Mnyambuliko | Kiishio | Kirejeshi nafsi |
|---|---|---|---|---|---|
| E | ta | pej | okinot | e | ki |

*Viambishi vya kukanusha / vikanushi;*

Viambishi vya kukanusha huleta maana ya kupinga au kukana. Katika Kiswahili viambishi hivi ni kama vile *si-* (nafsi ya kwanza-umoja na wingi), *hu-*(nafsi ya pili-umoja na wingi) na *ha-*(nafsi ya tatu-umoja na wingi). Katika lugha ya Kimaasai, vikanushi ni *ma-* (nafsi ya kwanza-umoja na wingi.) *mi-* (nafsi ya pili-umoja na wingi) na *me-* (nafsi ya tatu - umoja na wingi). Kwa mfano;

14. *Mapejokini* - sichomewi

| Kikanushi | nafsi | wakati | Mzizi | Mnyambuliko | Kiishio |
|---|---|---|---|---|---|
| *M* | *a* | *Ø* | *pej* | *okin* | *i* |

*Mikipejokini* - huchomewi

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kikanushi | nafsi | wakati | Mzizi | Mnyambuliko | Kiishio |
| *M* | *i* | *ki* | *pej* | *okin* | *i* |

*Mepejokini* - hachomewi

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kikanushi | nafsi | wakati | Mzizi | Mnyambuliko | Kiishio |
| *M* | *e* | *Ø* | *pej* | *okin* | *i* |

*Viambishi nafsi*:

Huwakilisha mtenda, kitendaji, mtendewa au kitendewa na hupatikana katika mazingira ya awali. Viambishi vya nafsi ni kama vile /a/ - nafsi ya kwanza(umoja), /ki/ -nafsi ya kwanza (wingi), /i/ - nafsi ya pili (umoja na wingi) na /e/-nafsi ya tatu (umoja na wingi). Viambishi hivi ndivyo hutangulia vitenzi na kwa hivyo ni viambishi awali.

Mifano;

| | *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|---|
| Nafsi ya kwanza | */a/ (Kiswahili –ni-).* | */ki/ (kiswahili tu-).* |
| Nafsi ya pili | /i/ (Kiswahili u-). | /i/ (kiswahili m-). |
| Nafsi ya tatu | /e/ (Kiswahili a-). | /e/ (kiswahili wa-). |

15a. *Nafsi ya kwanza* :

| *umoja* | *wingi* |
|---|---|
| *A-shom-o* - nimeenda. | *Ki-shom-o* - tumeenda. |
| NF-MZ-KI | NF-MZ-KI |
| a > ki/ awali | |

b. *Nafsi ya pili;*

| umoja | wingi |
|---|---|
| *I-shom-o* - umeenda. | *I-shom-o* - mmeenda. |
| NF-MZ-KI | NF-MZ-KI |

Mabadiliko hapa yanahusu sifa ya kiarudhi ya mabadiliko ya toni. Katika *i-shomo* ya umoja irabu ya mzizi na ya tamati hutamkwa kwa toni ya chini ilihali katika *i-shomo* ya wingi irabu zile hutamkwa kwa toni ya juu. Toni ndio mofimu ya wingi.

Umoja

*I – s h o m o*

Chini Chini

Wingi

*I - s h o m o*

Chini Juu

Ufunguo:

Chini – Toni ya chini.

Juu – Toni ya juu.

c. *Nafsi ya tatu – umoja*

*E-shomo* – ameenda

katikati juu

*wingi*

*E-shomo* - wameenda

katikati chini

Kulingana na maelezo ya Chomsky na Halle katika kazi yao ya *Sound Pattern of English* (1968), wameelezea toni kama sifa inayoadhiri irabu pekee katika silabi zinapopatikana.

Mifano zaidi;

*A-te-mer-e* - ni-li-lew-a. *ki-te-mer-ate* - tu-li-lew-a

NF-WK-MZ-KI NF-WK-MZ-KI

(Kiishio *e* ni kirejeshi cha nafsi na katika wingi kiishio hiki hubadilisha umbo na kuwa *ate;* e > ate/ ........# *)*.

16a. *I-te-mer-e* - u-li-lew-a *i-te-mer-ate* - m-li-lew-a

NF-WK-MZ-KI NF-WK-MZ-KI

b. *E-te-mer-e* - a-li-lew-a. *E-te-mer-ate* - wa-li-lew-a.

NF-WK-MZ-KI NF-WK-MZ-KI

*Viambishi vya wakati:*

Huwakilisha wakati wa tukio na hupatikana katika mazingira ya awali au tamati. Katika lugha ya Kimaasai, viambishi vya wakati sio dhahiri katika vitenzi vingi na hudhihirika kimatumizi.

Kiambishi cha wakati uliopita huwa na alomofu tano zinazowakilishwa na maumbo *–ta-*, *-te-*, *-ti-*, *-to-*, na *-tu-* kwa kutegemea ulinganifu wa irabu iliopo katika shina la kitenzi.. Hata hivyo, mofimu hii hujitokeza tu katika vitenzi vya kundi I pekee (vile visivyokuwa na irabu *i* ikitangulia mzizi. Kiambishi tamati *–ita* au *–ito* huwakilisha wakati uliopo au kitendo kinachoendelea na hudhihirisha ulinganifu wa irabu na ile ya shina katika vitenzi husika katika kundi I na kundi II. Wakati ujao na hali mazoea haina kiambishi mahsusi na hudhihirika kipragmatiki. Mengi yatajadiliwa kuhusu vitenzi vya kundi I na Kundi II katika sura ya tano), ilihali nyakati zingine zote hudhirika kimatumizi. Mifano;

*Wakati uliopita:*

17a. A-***ta***-batat-e – ni-li-anguk-a.
NF-WK-MZ-KI

A-*te*-lej-a – ni-li-m-dangany-a.
NF-WK-MZ-KI

I-***ti***-mir-ish-e – u-li-shind-an-a .
NF-WK-MZ-MN-KI

***-to***-lop-e – u-li-tapik-a.
NF-WK-MZ-KI

b. E-*tu*-un-ishe – u-li-pand-a.
NF-WK-MZ-KI

*E-tu-puku-o* – a-li-tok-a.
NF-WK-MZ-KI

*Wakati uliopo:*

Kiambishi cha wakati uliopita hujitokeza katika mazingira ya tamati na hivyo kuchukua nafasi ya kiishio. Mifano;

c. A-batat-***ita*** – ni-na-angu-sh-a.
NF-MZ -WK NF-MZ-WK

A-lej-***ita*** – ni-na-dangany-a.

d. I-mir-*ita* – u-na-shind-a.
NF-MZ-WK

I-lop-***ita*** – u-na-tapik-ish-a.
NF-MŽ-WK

e. E-un-*ito* – a-na-pand-a. E-irrug-*ito* – a-na-inam-ish-a.

NF- -MZ-WK NF -MZ-WK

*Mzizi*:

Hii ni sehemu isiyobadilika ya kitenzi licha ya kitenzi hicho kunyambuliwa kwa namna tofauti. Pia ni sehemu inayobakia baada ya viambishi vyote vilivyokuwa vimeambishwa kuondolewa. Mzizi hasa ndio mhimili wa neno na hupatikana katikati ya viambishi vingine. Tazama mizizi katika mifano iliyotolewa hapo juu na mifano inayofuata.

*Viambishi vya mnyambuliko*:

Viambishi hivi ni maumbo yanayouakilisha mfanyiko wa unyambuaji. Viambishi hivi hubadilisha maana ya maneno au kuyatoa katika makundi yao ya kisarufi hadi makundi mengine. Katika lugha ya Kimaasai, kiambishi hiki chaweza kupatikana katika mazingira ya tamati isipokuwa mnyambuliko wa jinsi ya kutendesha unaopatikana katika mazingira ya awali. Mnyambuliko wa vitenzi ndicho kiini hasa cha kazi hii. Mengi kuhusu dhana hii ya unyambuaji na mnyambuliko umeelezewa katika sura ya pili. Pia, jinsi unavyojitokeza katika lugha ya Kimaasai imeelezewa katika sura ya tano.

*Viambishi viishio*:

Vitenzi sahili vya lugha ya Kimaasai vyenye kiambishi kibainishi *a-* (kisawe cha *ku-* cha kiswahili) havina kiishio kama lugha ya Kiswahili.

Viishio hupatikana katika mazingira ya tamati. Katika baadhi ya lugha kama vile Kiswahili, kiishio huwa hakina maana mahsusi, isipokuwa ni kijalizo tu cha silabi ya mwisho katika neno kinachorahisisha matamshi. Ni mfano wa kile Anderson (1992) anachokiita *empty morphs*.

Vitenzi sahili vya Kimaasai katika hali yake ya kimsingi havina kiishio isipokuwa tu viwe vinaashiria mwendo fulani, kumwelekea mzungumzaji au kuelekea mbali na mzungumzaji.. Viambishi muhimu ambavyo huambishwa katika vitenzi sahili vya lugha hii ni kama vile vinavyoashiria wingi, mwendo kuelekea mbali au kumwelekea mzungumzaji.

Vitenzi hivi huku vikitawaliwa na sheria za usilimisho na ulinganifu wa irabu vyaweza kuishia kwa mojowapo ya viishio *a- e-, i-, o-, u-* *-isho,-ishe, -ishote, -ishoyu, -u, -ua/uo, aa/oo, -aiyie/oiyie,* na *-ai/oi*. Katika vitenzi vilivyonyambuliwa, kiambishi cha minyambuliko huchukua nafasi ya kile kiishio. Mnyambuliko wa kutendesha hata hivyo hukaidi utaratibu huu kwa sababu ndio mnyambuliko pekee ambao hutokea katika mazingira ya awali.

Katika lugha hii, kile kinachovutia katika uchunguzi wa viishio hivi ni kuwa, katika vielezo vingi vya vitenzi sahili au vile vilivyonyambuliwa kuna ule mfumo wa ulinganifu wa irabu ya kile kiishio na ile ya mzizi. Hili pia litajadiliwa kwa kirefu katika sura ifuatayo.

### 4.4 Sintaksia ya Lugha ya Kimaasai

Sintaksia ni kiwango cha uchanganuzi wa kiisimu kinachojishughulisha na ule mpangilio wa vipashio vya kimaana katika neno au sentensi. Kipashio cha kimaana chaweza kuwa kiambishi au neno timilifu lisiloweza kugawika zaidi bila kupoteza maana. Miundo ya sentensi ni dhana ilio nje ya upeo wa utafiti huu ; lakini kwa sababu ya mifano michache iliotolewa kwa muktadha wa sentensi, ni muhimu kutaja kwamba, katika sentensi maneno ya lugha ya Kimaasai hufuata mifumo miwili ya mpangilio huku ikitegemea kama kauli ni tendi au ni tendewa;

*(i)Kauli tendi: Kitenzi – kiima – kiarifa:*

Mfumo huu hujitokeza katika sentensi za kauli tendi ambapo kiima ni mtu au kitu kinachotenda kitendo kinachohusika. Kwa mfano;

| | | |
|---|---|---|
| 18a. | *Einosita* Koileken endaa. | Koileken *anakula* chakula. |
| | *Kitenzi – kiima - kiarifa* | *kiima - kitenzi - kiarifa* |
| b. | *Etanapa.*yeyioo enkerai | Mama alimbeba mtoto |
| | *Kitenzi – kiima - kiarifa* | *kiima - kitenzi - kiarifa* |
| c. | *Eterewa* Lesaloi Engarri | Lesaloi *aliliendesha* gari. |
| | *Kitenzi – kiima - kiarifa* | *kiima - kitenzi - kiarifa* |

*(ii) Kauli tendewa: Kiima – kitenzi – kiarifa*

Mfumo huu hutumika katika sentensi za kauli tendwa ambapo kiima huathiriwa na kitenzi kinachohusika. Kwa mfano;

| | | |
|---|---|---|
| 19a. | Endaa *einosita* Koileken | Chakula *kinaliwa* na Koileken. |
| | *Kiima – kitenzi – kiarifa* | *Kiima – kitenzi – kiarifa* |
| b. | Enkerai *etanapa* yeyioo | Mtoto *alibebwa* na mama. |
| | *Kiima – kitenzi – kiarifa* | *Kiima – kitenzi – kiarifa* |
| c. | Engarri *eterewa* Lesaloi | Gari *liliendeshwa* na Lesaloi. |
| | *Kiima – kitenzi – kiarifa* | *Kiima – kitenzi – kiarifa* |

Katika kauli ya kutendwa kitenzi hubadilisha nafasi yake katika sentensi. Pia katika kauli hii maana ya kutendwa hudhihirika kiimatumizi kwa kuwa kitenzi hakibadilishi umbo. Katika utafiti huu popote ambapo mpangilio wa maneno ya Kimaasai haulingani na mpangilio wa tafsiri ya Kiswahili, maelezo yametolewa ili kupunguza utata.

Pia sentensi fupifupi zimetumiwa na vitenzi kuandikwa kwa herufi za mlazo katika Kimaasai na pia katika Kiswahili ili kumwezesha msomaji kuvibainisha kwa urahisi.

Lugha hii ina jumla ya minyambuliko minane. Minyambuliko hii inawakilishwa na mofimu zenye seti ya alomofu zinazokitofautisha kielezo kimoja na kingine kutegemea sifa mbalimbali za kimofosintaksia kama vile nafsi, wakati au hali.
Minyambuliko hii hutokea katika mazingira ya tamati isipokuwa mnyambuliko wa jinsi ya kutendesha unaojitokeza katika mazingira ya awali. Ufuatao ni muhtasari wa alomofu za kila mofimu ya mnyambuliko.

Mnyambuliko wa jinsi ala-tendea: *-ie, -ieki, -ishore* na *-ishoreki*.

Mnyambuliko wa jinsi ya kutendea / uhusika tendea: *–oki/-aki, -aka/-oko, -iki, -aa/-oo, -okito/-akita, -ikia/-ikita* na *–ikia.*

Mnyambuliko wa jinsi ya kutendesha: *-it-, -nt-, –i-, -m-* na *–n-.*

Mnyambuliko wa jinsi ya kutendwa/kutendewa: *-toi/-tai, -uni/i, -uoki/-uaki, -aki/-oki, -ikini/-akini/-okini -koki/-kaki, -oyioki/-ayioki, -ari/-ori* na *–uno.*

Mnyambuliko wa jinsi ya kutendana: *-a/o,-ote/ate, -ata/-oto, -kino/-kinono, -kinote/-unote, -uno* na *–kinoto.*

Mnyambuliko wa jinsi ya kutendeka – alomofu -e,*-ayu/-oyu/-noyu* na *-ate/-ote.*
Mnyambuliko zalishi: *–yu* na *-u.*

Mnyambuliko radidi hauna mofimu maalum bali huashiriwa na uradidi wa shina au mzizi. Vishio vya vitenzi sahili pamoja maumbo ya mofimu za mnyambuliko zimetolewa katika jedwali lililopo katika ukurasa wa 95.

Katika sura hii dhana ya kitenzi ilichunguzwa katika viwango vinne; kisauti (kifonolojia), kimaumbile (kimofolojia) kimaana (kisemantiki) na hatimaye kimazingira (kisintaksia). Ilidhihirika kwamba vitenzi vya Kimaasai hubadilika kimuundo kutegemea athari za sheria za kifonolojia zinazoibuka kutokana na ujirani wa baadhi ya sauti, kuambishwa kwa vipashio vya kimaana (viambishi) au kuwepo katika mazingira fulani katika sentensi. Sura ifuatayo ilimulika dhana ya minyambuliko mahsusi ya vitenzi kwa undani na maana zinazotokana na minyambuliko hii.

## SURA YA TANO

## MNYAMBULIKO WA VITENZI

### 5.1 Utangulizi,

Sura hii inahusu kubainisha mofimu mbalimbali za mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kimaasai na maana zinazoandamana na maumbo haya. Hii inatokana na msingi kwamba, vitenzi ni mojawapo ya makundi wazi ya kisarufi na kama katika lugha zingine, mashina ya vitenzi vya lugha ya kimaasai yana ule uwezo wa kuchukua viambishi kadha wa kadha vya kimaana. Viambishi hivi au mofimu hufuata sheria mbalimbali za kimofofonolojia kama vile uchopekaji, usimilishaji, ulinganifu wa irabu na udondoshaji ili kuzua maana na maumbo tofautitofauti. Ni katika sehemu hii hasa ambapo madhumuni ya utafiti huu yanatekelezwa.

### 5.2 Vitenzi sahili vya lugha ya Kimaasai

Vitenzi vya lugha ya Kimaasai vyaweza kugawanywa katika vikundi viwili vya kimofolojia. Jambo hili limetajwa na wataalam kama vile Tucker na Mpaayei (1955), Hollis (1905) na Mol (1978) ambapo wameyaita makundi haya kundi I na kundi II *( class I and class II)*. Kuingia kwa kitenzi katika kikundi I au kikundi II kunategemea kama shina linaanza kwa kiambishi awali i- au la.

Katika mifano hii, {*a-*} inayotangulia kitenzi ni kisawe cha {*ku-*} cha kiswahili. Kiambishi /a/ pia chaweza kutumika kama kiambishi cha nafsi ya kwanza umoja. Dhana ya viambishi vya nafsi na vya wakati imeelezewa katika sura ya nne.

| | *Kundi I* | *Kundi II* |
|---|---|---|
| 20. (a) | *A-pik* – ku-ing-iz-a | *A-ipik* – ku-tok-ez-a. |
| | KB-MZ | KB-MZ |
| (b) | *A-bor* – ku-tul-ia | *A-ibor* - kuwa –eupe |
| | KB-MZ | KB-MZ |
| (c) | *A-pur* – ku-iba | *A-ipur* – ku-ngurum-a |
| | KB-MZ | KB-MZ |

(c) *A-ruk* – ku-tung-a shanga    *A-iruk* – ku-amin-i

KB-MZ    KB-MZ

Kiambishi awali cha vitenzi vya kundi II ni /i/ funge mwanzoni mwa shina lenye irabu funge na /i/ wazi mwanzoni mwa shina lenye irabu wazi. Hii ni sheria ya ulinganifu wa irabu.

Kwa mfano,

i- funge    -i- wazi

21(a) *A-iting'* –ku-fik-a mwisho    *A-itiship* – ku-furah-ish-a

KB-MZ    KB-MZ

(b) *A-ilep-ie* – ku-inu-a    *A-ilep'* – ku-kwe-a

KB-MZ -KI    KB-MZ

*A-ipot* – ku-it-a    *A-iposh* - ku–vurug-a

KB-MZ    KB-MZ

*A-isur* – ku-fitin-i    *A-isuj* – ku-osh-a

KB-MZ    KB-MZ

Vitenzi vyenye irabu /a/ ya shina vyaweza kuchukua kiambishi awali /i/ ambacho chaweza kuwa funge au wazi. Hata hivyo /i/ iliyo wazi hutokea kwa wingi zaidi. Kwa mfano katika maneno yafuatayo;

22a. *A-inyang'* – ku-nunu-a kutoka kwa (/i/ wazi).

KB-MZ

b. *A-igany* – ku-jaz-a (/i/ funge)

KB-MZ

c. *A-imany-a* – ku-ap-a (/i/ wazi)

KB-MZ-KI

d. *A-im* – ku-pit-a (/i/ wazi)

KB-MZ

Tofauti ya viambishi tamati vya vitenzi vya kundi I na kundi II navyo hutegemea mambo kadha kama vile wakati, nafsi au mofimu ya mnyambuliko iliopo. Viambishi vya mnyambuliko hata hivyo havitegemei mgao huu. Vitenzi sahili katika makundi yote mawili huwa na kibainishi {a-} mwanzoni. Kiambishi {a-} ni kisawe cha kibainishi {*ku-*}katika vitenzi vya Kiswahili kama vile kusoma, kulia, kucheka na mengineyo. Kwa mfano;

Lugha ya Kimaasai huwa haitofautishi kati ya hali timilifu na wakati uliopita; dhana zote mbili hucukuliwa kama wakati uliopita.

23a. *A-dam-u* – ku-kumbuk-a

KB-MZ-KI

b. *A-ipung'* – ku-tok-a

KB-MZ

c. *A-lak* – ku-lip-a

KB-MZ

d. *A-irrag* – ku-lal-a

KB-MZ

f. *A-ok* – ku-nyw-a

KB-MZ

g. *A-ipot* – ku-it-a

KB-MZ

h. *A-dung* – ku-kat-a

KB-MZ

i. *A-iba* – ku-chuk-ia

KB-MZ

Dhana ya viambishi vya nafsi na vya wakati imeelezewa katika sehemu ya 4.3. Vitenzi sahili huchukua viambishi tamati kulingana na nyakati na nafsi mbalimbali kama itakavyobainika katika mifano ifuatayo.

*(i) Viishio –isho/-ishe/ishote*

Vitenzi sahili vyaweza kuchukua viambishi tamati *–isho/-ishe/ishote* ambavyo ni virejeshi vya nafsi katika wakati uliopo na hali rai. Mchakato uliopo ni uchopekaji tamati. Pia kuna uradidi wa silabi ya mwisho katika nafsi ya pili (wingi). Sheria ya kijumla inayoathiri vitenzi vyenye kiishio hiki ni;

*–isho/-ishe/ishote* / ---------#

Kwa mfano;

*Nafsi ya kwanza:*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 25a. *A-rany* : | *A-rany-isho* - | *Ki-rany-isho* - | *a-ta-rany-ishe* – | *ki-ta-rany-ishote* |
| | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF | NF-WK-MZ-KNF | NF-WK-MZ-KNF |
| Ku-imb-a : | na-imb-a | Twa-imb-a / tu-na-imb-a | ni-li-imb-a | tu-li-imb-a |

| | | |
|---|---|---|
| b. *A-rip* : | *A-rip-isho* | *Ki-rip-isho* |
| | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF |
| Ku-shon-a : | ni-na-shon-a – | Tu-na-shon-a / twa-shon-a |

Nafsi ya pili:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| c. *A-dung'* : | *I-dung'-isho*– | *Tu-dung'-isho!* | *Ki-dung'-isho* | *I-dung'-isho-sho* |
| | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF-WI |
| Ku-kat-a : | u-na-kat-a | kat-a! | tu-na-kat-a / | sisi hu-kat-a |

| | | | |
|---|---|---|---|
| d. *A-lej:* | *I-lej-isho-* | *Te-lej-isho!* | *i-lej-isho-sho* |
| | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF-WI |
| Ku-danyany-a : | u-na-dangany-a | dangany-a! | m-na-dangany-a/ mwa-dangany-a |

*Nafsi ya tatu:*

| | | | |
|---|---|---|---|
| e. *A-ked* : | *E-ked-isho* | *Me-ta-ked-isho!* | *E-ked-isho* |
| | NF-MZ-KNF | NF-R-MZ-KNF | NF-MZ-KNF |
| Ku-kwe-a : | a-na-kwe-a A-kwe-e! | Wa-na-kwe-a | |

(Tofauti kati ya *e-ked-isho* ya umoja na wingi ni ya kipragmatiki)

| | | | |
|---|---|---|---|
| f. *A-isul* : | *E-isul-isho* | *Me-isul-isho!* | *E-isul-isho* |
| | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF |
| Kupiga miluzi : | unapiga miluzi! | Apige miluzi | Wanapiga miluzi. |

(Tofauti kati ya *e-isul-isho* ya umoja na wingi ni ya kipragmatiki. Pia mofimu ya rai ni kapa).

*(ii) Kiishio –ishe / -ishote*

Kiambishi tamati /- ishe/ ni cha umoja na /–ishote/ ni cha wingi. Viishio hivi hutumika katika vitenzi sahili vya wakati uliopita. Kiambishi awali *–ta-,-te-, -ti-, -to- na -tu-* cha wakati uliopita huchopekwa baada ya kiambishi cha nafsi. Ulinganifu wa irabu hujitokeza ambapo irabu ya kiambishi hiki hutegemea irabu ya shina la kitenzi. Kwa mfano, vitenzi sahili vilivyotumika hapo juu vikiwa katika wakati uliopita hupata mabadiliko yafuatayo kwa kufuata sheria hii;

-ishe > -ishote / -------#

Nafsi ya kwanza:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 26a. | *A-rany :* | *a-ta-rany-ishe* | *ki-ta-rany-ishote* |
| | | NF-WK-MZ-KNF | NF-WK-MZ-KNF |
| | Ku-imb-a : | ni-li-imb-a | Tu-li-imb-a |

(pana usilimisho kati ya /a/ ya nafsi na /a/ ya kibainishi)

| | | | |
|---|---|---|---|
| b. | *A-rip :* | *a-ti-rip-ishe* | *ki-ti-rip-ishote* |
| | | NF-WK-MZ-KNF | NF-WK-MZ-KNF |
| | Ku-shon-a : | ni-li-shon-a | tu-li-shon-a |
| c. | *A-ure :* | *a-tu-ur-ishe* | *ki-tu-ur-ishote* |
| | | NF-WK-MZ-KNF | NF-WK-MZ-KNF |
| | Ku-ogop-a : | ni-li-ogop-a | tu-li-ogop-a. |
| d. | *Aisuj :* | *a-isuj-ishe* | *ki-suj-ishote* |
| | | NF-WK-MZ-KNF | NF-WK-MZ-KNF |
| | Ku-saf-ish-a: | ni-li-saf-ish-a | tu-li-saf-ish-a |

Nafsi ya pili:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 27a. | *A-dung':* | *i-tu-dung'-ishe* | *i-tu-dung'-ishote* |
| | | NF-WK-MZ-KNF | NF-WK-MZ-KNF |
| | Ku-kat-a: | u-li-kat-a | m-li-kat-a |
| b. | *A-lej:* | *i-te-lej-ishe* | *i-te-lej-ishote* |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | NF-WK-MZ-KNF | NF-WK-MZ-KNF |
| | Ku-danganya-a: | u-lidanganya-a | m-lidanganya-a |
| b. | *Amirr:* | *i-ti-mir-ishe* | *i-ti-mir-ishote* |
| | | NF-WK-MZ-KNF | NF-WK-MZ-KNF |
| | Ku-shind-a: | u-li-shind-a | m-li-shind-a |
| c. | *A-un:* | *i-tu-un-ishe* | *i-tu-un-ishote* |
| | | NF-WK-MZ-KNF | NF-WK-MZ-KNF |
| | Ku-pand-a: | u-li-pand-a | m-li-pand-a. |

Nafsi ya tatu:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 28a. | *A-ked:* | *e-ta-ked-ishe* | *e-ta-ked-ishote* |
| | | NF-WK-MZ-KNF | NF-WK-MZ-KNF |
| | Ku-pand-a: | a-me-panda | wa-me-pand-a |
| b. | *A-isul:* | *e-isul-ishe* | *e-isul-ishote* |
| | | NF-MZ-KN | NF-MZ-KNF |

Ku-pig-a miluzi: a-li-pig-a miluzi – wa-lipig-a miluzi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| c. | *A-rrip:* | *e-ti-rrip-ishe* | *e-ti-rrip-ishote* |
| | | NF-WK-MZ-KN | NF-WK-MZ-KNF |
| | Ku-lind-a: | a-li-lind-a | wa-li-lind-a |
| d. | *A-igerr:* | *e-iger-ishe* | *e-iger-ishote* |
| | | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF |
| | Ku-andik-a: | a-li-andik-a | wa-li-andik-a |

Katika vitenzi kadha, viishio hivi huleta maana ya kutendana.

Mifano hii hata hivyo ni michache sana hivi kwamba ni salama kuchukulia kwamba viishio hivi kimsingi ni vitenzi sahili vyenye maana ya hali ya kutenda.mifano ya vitenzi hivi vinavyopotoka kutoka katika kielelezo na kuchukua maana ya jinsi ya kutendeana au kutendana ni kama vile,

| | | |
|---|---|---|
| e. | *A-arr :* | *I-ta-ar-ishote* |
| | | NF-WK-MZ-KNF |
| | Ku-pig-a : | m-lipig-an-a / m-li-u-an-a |
| f. | *A-morr :* | *e-ta-mor-ishote* |
| | | NF-WK-MZ-KNF |
| | Ku-tukan-a : | wa-li-tukan-an-a. |

*(iii) Kiishio –ishoyu / ishoyuyu*

Kundi lingine la vitenzi sahili ni lile lenye kiambishi tamati */-ishoyu/* ambapo *–yu* ni kiwakilishi cha wakati ujao. Mofimu ya wakati ni kapa. Mchakato uliopo ni wa uchopekaji tamati na hufuata sheria hii:

-ishoyu / -------- #

Mifano;

*Nafsi ya kwanza:*

| | *Umoja* | *Wingi* |
|---|---|---|
| 29a. | *A-rany-ishoyu* | *Ki-rany-ishoyu* |
| | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF |
| | ni-taimb-a | tu-ta-imb-a. |
| b. | *A-lej-ishoyu* | *ki-lej-ishoyu* |
| | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF |
| | ni-ta-dangany-a | tu-ta-dangany-a. |
| c. | *A-lop-ishoyu* | *Ki-lop-ishoyu* |
| | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF |

ni-ta-tapik-a tu-ta-tapik-a.

*Nafsi ya pili:*

Katika nafsi ya pili wingi, dhana ya wingi huakilishwa na uradidi wa silabi ya mwisho ya kiishio kama ifuatavyo. Mofimu ya wakati hapa pia ni kapa.

| | | |
|---|---|---|
| 30a. | *Umoja* | *Wingi* |
| | *In-ger-ishoyu* | *In-ger-ishoyu-yu* |
| | NF- MZ-KN | NF- MZ-KNF-W |
| | u-ta-andik-a | tu-ta-andik-a |
| b. | *I-rany-ishoyu* | *I-rany-ishoyu-yu* |
| | NF- MZ-KNF | NF- MZ-KNF-W |
| | u-ta-imb-a | m-ta-imb-a. |
| c. | *I-isuj-ishoyu* | *I-suj-ishoyu-yu* |
| | NF- MZ-KNF | NF- MZ-KNF-W |
| | u-ta-safish-a | m-ta-osh-a. |

*Nafsi ya tatu:*

| | | |
|---|---|---|
| | *Umoja* | *Wingi* |
| 31a. | *E-lej-ishoyu* | *E-lej-ishoyu* |
| | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF |
| | a-ta-dangany-a | wa-ta-dangany-a |
| b. | *E-rany-ishoyu* | *E-rany-ishoyu* |
| | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF |
| | a-ta-imb-a. | wa-ta-imb-a. |
| c. | *E-lop-ishoyu* | *E-lop-ishoyu* |
| | NF-MZ-KNF | NF-MZ-KNF |

a-ta-tapik-a wa-ta-tapik-a

Katika vitenzi sahili kuna vitenzi ambavyo huashiria mwendo. Mwendo waweza kuwa unamwelekea mzungumzaji au unaelekea mbali na mzungumzaji. Tucker na Mpaayei (1955) na Hollis (1905) wanaziita hali hizi *'Motion Towards Form'* na *'Motion Away Form'*

*(a) Vitenzi vinavyoashiria mwendo kumwelekea mzungumzaji* huchukua viishio kadha wa kadha. Kwa mfano:

*(i) Kiambishi tamati /u/:*

Kiishio hiki huonyesha mwendo unaomwelekea mzungumzaji katika wakati ujao au hali rai.Katika hali rai, kuna uchopekaji awali wa mofimu ta, te ti to au tu kuwakilisha rai au amri inayotolewa. Uchopekaji huu hutii sheria ya ulinganifu wa irabu kulingana na irabu ya mzizi. Pia katika hali rai, mofimu ya nafsi ya pili huungana na nasali inayoteuliwa kulingana na mazingira ya kutamkwa kwa konsonanti inayoanzia mzizi.

Konsonanti za mdomo hunasalishwa kwa /m/, konsonanti ya ufizi hunasalishwa kwa /n/, zakaakaa gumu kwa sauti /ny/ ilihali za kaakaa laini hunasalishwa kwa sauti /ng'/. Pia mofimu *e* ya nafsi ya tatu hubadilika na kuwa *me* na huchopekwa mwanzoni mwa kitenzi. (kumbuka *a-* ni kibainishi kilicho kisawe cha *ku-* cha Kiswahili na pia ni mofimu ya nafsi ya kwanza umoja) Sheria ya kijumla inayojitokeza katika mifano ifuatayo ni; u / ------ #
Mifano;

*Nafsi ya kwanza*: Katika mifano hii, mofimu ya wakati ni kapa.

(Wakati > kapa)

32a. *A-dot* *a-dot-u* *ki-dot-u*

KB-MZ NF-MZ-KI NF-MZ-KI

ku-ng'o-a ni-ta-ng'o-a / mimi hu-ng'o-a tu-ta-ng'o-a / sisi hu-ng'o-a.

b. *a-ut-u* *ki-ut-u*

NF-MZ-KI NF-MZ-KI

ni-ta-ota / mimi hu-elek-ez-a Tu-ta-elek-ez-a / sisi hu-elek-ez-a

(upande huu). (upande huu).

*Nafsi ya pili:*

| | | | |
|---|---|---|---|
| c. | *a-purr* | *i-purr-u* | *I-purr-u-rru* |
| | KB-MZ | NF-MZ | NF-MZ-MT-KNF |
| | ku-iba | u-ta-iba /wewe hu-iba | m-ta-iba / nyinyi hu-ib-a. |

(Kumwelekea mzungumzaji Wakati > kapa)

| | | |
|---|---|---|
| d. | *Te-yet-u!* | *En-te-yet-u!* |
| | R-MZ-KI | NF-R-MZ-KI |
| | vuta upande huu! | Vuteni upande huu! |

(Mofimu ya nafsi imenasalishwa kwa *n* ya ufizi kwa ajili ya *t* ya ufizi inayoifuatia).

| | | |
|---|---|---|
| e. | *Ti-mir-u!* | *En- ti- mir-u!* |
| | R-MZ-KI | NF-R-MZ-KI |
| | fukuz-a upande huu! | Fukuz-e-ni upande huu! |

| | | |
|---|---|---|
| f. | *To-ning'-u!* | *En-to-ning'-u !* |
| | R-MZ-KI | NF-R-MZ-KI |
| | Siki-a ukielekea upande huu! | Siki-e-ni mkielekea upande huu. |

*Nafsi ya tatu:*

| | | |
|---|---|---|
| 33a. | *e-sot-u* | *Me-ta-sot-u!* |
| | NF-MZ-KI | NF-R-MZ-KI |
| | a-ta-kusany-a kuelekeza upande huu | A-kusany-e kuelekeza upande huu!/ |
| | (Wakati > kapa) | wa-kusany-e kuelekeza upande huu! |

| | | |
|---|---|---|
| b. | *e-ing'or-u* | *Me-ing'or-u!* |
| | NF-MZ-KI | R-MZ-KI |
| | a-ta-tafut-a akija. | a-tafut-e akija!/ wa-tafut-e wakija! |
| | (Wakati > kapa) | (wingi ni kapa) |

| | | |
|---|---|---|
| c. | *e-gel-u* | *me-te-gel-u!* |

| | |
|---|---|
| NF-MZ-KI | NF-R-MZ-KI |
| a-ta-chagu-a. | A-chagu-e!/ wa-chagu-e! |

(Kumwelekea mmzungumzaji, wakati > kapa, mofimu ya wingi ni kapa).

*(ii) Kiambishi tamati /ua/ au /-uo/:*

Kiishio hiki huashiria mwendo kumwelekea mzungumzaji katika wakati uliopita.

Katika wingi, viambishi */uo/* na */ua/* hubadilika na kuwa */-utuo/* na */-utua/* ambapo utendakazi wa sheria ya ulinganifu wa irabu hudhihirika. Viambishi vya wakati uliopita *ta, te, ti, to* na *tu* vinavyochopekwa katika mazingira ya awali huchukua irabu inayotamkwa katika mazingira sawa na ile ya mzizi. Mifano:

*Nafsi ya kwanza:*

$$\text{uo} > \text{utuo} \,/\, \text{----}\,\# \quad \begin{bmatrix} +\text{irabu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix}$$

| | | |
|---|---|---|
| 34a. | *A-ta-por-uo* | *Ki-ta-por-ut-uo .* |
| | NF-WK-MZ-KI | NF-WK-MZ-WI-KI |
| | Ni-li-tamb-aa nikija. | Tu-li-tamb-aa tukija |
| b. | *A-to-osh-uo.* | Ki-to-osh-utuo |
| | NF-WK-MZ-KI | NF-WK-MZ-KI |
| | Ni-li-elek-ez-a (mifugo) upande huu huu | Tu-li-elek-ez-a (mifugo) upande huu huu |

Mifano ifuatayo inaadhiriwa na sheria:

$$ua > utua \,/\, \text{------}\# \quad \begin{bmatrix} +\text{ irabu} \\ +\text{mbele} \end{bmatrix}$$

| | | |
|---|---|---|
| c. | *E-ipang'-ua* | E-ipang'-ut-ua |
| | NF-MZ-KI | NF-MZ-WI-KI |
| | A-li-tok-a kuelekea upande huu. | Wa-li-tok-a kuelekea upande huu |

(Wakati > kapa)

d. *A-ing'or-ua* *Ki-ng'or-ut-ua*

NF-MZ-KI NF-MZ-WI-KI

Ni-li-ta-fut-a. Tu-li-ta-fut-a

Katika mfano huu kitendo kinamwelekea mzungumzaji, wakati ni kapa na pana usilimisho kati ya *u* ya *king'oru* na ile ya *utua*.

*(b) Vitenzi vinavyoashiria mwendo mbali na mzungumzaji:*

Vitenzi vya umbo hili pia huchukua viambishi tamati kadha. Kwa mfano;

*(i) Kiambishi tamati /-aa/ au /-oo/ cha wakati ujao au mazoea.*

Kiambishi hiki huchopekwa katika mazingira ya tamati na hufuata sheria ya ulinganifu wa irabu na hutumika katika nafsi zote. Kwa mifano;

Sheria oo / ----- # [+ irabu, + nyuma]

35a. *A-ng'or-oo* eremet *Ki-ng'or-oo* iremeta

NF- MZ-KI NF- MZ-KI

Ni-ta-rush-a / Mimi hurusha. Tu-ta-rush-a/ Sisi hu-rush-a.

b. *A-osh-oo* *Ki-osh-oo*

NF- MZ-KI NF- MZ-KI

Ni-ta-fukuz-a mbali / tu-ta-fukuz-a mbali/

Mimi hu-fukuz-a mbali. sisi hu-fukuz-a mbali.

Mifano ifuatayo inatawaliwa na sheria hii;

Sheria (aa / ------ #) [+ irabu, + mbele]

c. *A-yiat-aa*

NF- MZ-KI

Ni-ta-burut-a mbali/ Mimi hu-burut-a mbali.

d. *I-mirr-aa*
NF- MZ-KI
U-ta-wa-fukuz-a/ wewe hu-wa-fukuz-a / m-ta-wa-fukuz-a.

e. *E-yiat-aa*
NF- MZ-KI
A-ta-burut-a/ Wao hu-burut-a.

(ii) */-ayie/ au /-oyie/*

Wakati mwingine, vitenzi sahili vinavyoashiria mwendo mbali na mnenaji huchukua viambishi tamati */-ayie/ au /-oyie/* kwa kufuata sheria ya ulinganifu wa irabu katika wakati uliopita na katika nafsi zote. Sheria za kijumla zinazotenda kazi ni;

(i) ayie / ----- # $\begin{bmatrix} + \text{irabu} \\ + \text{mbele} \end{bmatrix}$

(ii) oyie / ----- # $\begin{bmatrix} + \text{irabu} \\ + \text{nyuma} \end{bmatrix}$

| | | |
|---|---|---|
| 37a. | *A-te-lej-ayie* pee *e-lo*<br>NF- WK- MZ-KI<br>Ni-li-m-danganya-a ili a-end-e. | *A-te-rew-aiyie* inkishu<br>NF-MZ NF- WK-MZ-KI<br>Ni-li-wa-pelek-a ng'ombe. |
| b. | *I-ta-ng'or-oyie* eremet.<br>NF- WK-MZ-KI<br>U-li-rush-a mkuki. | *I-rrag-ayie* Narok.<br>NF-MZ-KI<br>U-li-lal-a Narok ukienda. (wakati > kapa) |
| c. | *E-ta-nang-aiye* isoito<br><br>NF- WK-MZ-KI<br>A-li-rush-a mawe (mbali). | *E-ta-bol-oyie* inkineji.<br><br>NF- WK-MZ-KI<br>A-li-fung-ua zizi mbuzi (waende). |

(ii) */-oitie/ au /-aitie/.*

Katika hali ya wingi, kiambishi tamati /-oyie/ au /-ayie/ hubadilika na kuwa */-oitie/ au /-aitie/*. Vilevile kwa kufuata sheria ya ulinganifu wa irabu ambapo irabu ya kiishio hupatikana katika mazingira sawa na ile ya mzizi. Kwa mintarafu hii katika mifano ifuatayo, sheria zinazodhihirika ni hizi;

(i) aiye > aitie / ----- # [+ irabu, + mbele]

(ii) oiyie > oitie / ----- # [+ irabu, + nyuma, + uviringaji]

Kwa mfano;

| | | |
|---|---|---|
| 38a. | *A-te-lej-aiye* pee elo - | *Ki-te-lej-aitie* pee epuo |
| | NF- WK-MZ-KI | NF-WK-MZ-W |
| | Ni-li-m-dangany-a ili aende – | Tu-li-wa-dangany-a ili waende. |
| b. | *E-ti-mir-aiye* ildiein - | *E-ti-mir-aitie* ildiein. |
| | NF-WK-MZ-KI | NF-WK-MZ-W |
| | A-li-wa-fukuz-a mbwa– | Wa-li-wa-fukuz-a mbwa. |
| c. | *A-tu-tur-oiye* empopok - | *Ki-tu-tur-oitie* impopoki. |
| | NF- WK-MZ-KI | NF-WK-MZ-W |
| | Ni-li-zik-a mzoga | Tu-li-zik-a mizoga. |
| d. | *I-ta-ngor-oiye* eremet - | *I-ta-ng'or-oitie* iremeta |
| | NF- WK-MZ-KI | NF-WK-MZ-W |
| | U-li-rush-a mkuki | M-li-rush-a mikuki. |

Popote ambapo konsonanti hudondoshwa, sauti /y/ huchopekwa huku ikifuatwa na kutanguliwa na irabu. Kwa mfano katika neno *a-dol* (kuona) tunapata maneno yafuatayo;

39a. *A-d-uaaya* – ni-na-mw-on-a (akienda) / mimi humwona (akienda).

NF-MZ-KI

b. *A-to-d-uaayie*

NF-WK-MZ-KI

ni-li-mw-on-a (akienda).

Sheria inayojitokeza ni l > y / v – v.

Pia kutoka katika neno *a-dek* (kulaani) tunapata maneno yafuatayo;

c. *E-d-iaaya*

NF-MZ-KI

A-na-m-laan-i (akienda) / hu-m-laan-i (akienda).

d. *E-te-d-iaaye*

NF-WK-MZ-KI

A-li-m-laan-i (akienda).

Mfano mwingine ni wa kitenzi *a-buak* kimaanishacho ku-payuka ambacho huzua vitenzi vifuatavyo;

e. *A-b-uaaya*

NF-MZ-KI

Ni-na-payuk-a (nikienda) / Mimi hu-payuk-a (nikienda).

f. *A-to-b-uaayie*

NF-WK-MZ-KI

Ni-li-payuk-a (nikienda).

Sheria itendayo kazi hapa ni k > y / v – v ambapo sauti /k/ hubadilika na kuwa /y/ katika mazingira ya vokali mbili.

Katika neno *a- idak* linalomaanisha 'kuangamia' konsonanti /k/ hudondoshwa na badala yake konsonanti /y/ kati ya irabu mbili huchopekwa kama ifuatavyo:

g. *A-idak* (ku-angam-ia) – *a-idaay-a* (ku-angam-ia na ku-tokom-ea kabisa)

NF-MZ NF-MZ-KI

g. *In-day-ie* - (u-me-angam-ia kabisa) *k > y / v –v,* {*i*} ambayo ni mofimu ya nafsi imenasalishwa.

NF-MZ-KI

(iv) *Kiambishi tamati /-ai/ au /-oi:*

Baadhi ya vitenzi sahili vinavyoashiria mwendo mbali na mzungumzaji huchukua kiambishi tamati /-ai/ au /-oi/ katika hali rai. Vitenzi hivi vina kiambishi awali kinachowakilisha muungano wa nafsi na rai kinachotegemea mzizi wa kitenzi kinachohusika. Mofimu hii ni matokeo ya utendakazi wa sheria tofautitofauti kama vile unasalishaji awali wa vipasuo na vikwaruzo vinavyoanzia mzizi, ulinganifu wa irabu na uleksia usioelezeka kwa sheria yoyote ya kiisimu.

*Unasalishaji* unaathiri vitenzi vya kundi II ambapo sauti *i* ya shina hubadilika na kuwa nasali ya eneo mnampotakiwa kipasuo au kikwaruzo kinachoanzia mziziau eneo lillilo jirani. Kwa mfano katika maneno yafuatayo;

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 40a. *In-chop-oi!* | *Im-buk-oi!* | b. | *Im-pot-oi!)* | *Im-pa-ai!* |
| R-MZ-KI | R-MZ-KI | | R-MZ-KI | R-MZ-KI |
| Va-a (ukienda)! | Mwag-a! | | It-a (ukienda) | Tum-a! |

*Ulinganifu wa irabu* nao unadhihirika kati ya irabu ya mzizi na ile ya kiishio na kutii sheria ifuatayo;

*oi* / ..........# [+ Irabu, + nyuma]

Kwa mfano:

| | | |
|---|---|---|
| 41a. *Tu-tur-oi* | b. | *To-osh-oi!* |
| R-MZ-KI | | R-MZ-KI |
| zik-a chini mbali! | | Wapelek-e! (mifugo) mbali |

| | | | |
|---|---|---|---|
| c. | *To-du-ai!* | d. | *Te-rew-ai!* |
| | NF-MZ-KI | | R-MZ-KI |
| | Angali-a! | | pelek-a! (mifugo) mbali |

*a* inayotumika katika *toduai* ni ya nyuma na vitendo vinaelekea mbali na mnenaji.

Kuna vitenzi vichache vinavyopatikana katika umbo hili ambavyo haviashirii mwendo wowote ule, kwa mfano:

| 42a. | b. | c. | d. | e. |
|---|---|---|---|---|
| *A-or-u* | *A-ạny-u* | *A-i-u* | *A-inyang'-u* | *A-ibir-u* |
| KB-MZ-KI | R-MZ-KI | R-MZ-KI | R-MZ-KI | R-MZ-KI |
| u-nyang'anya. | ku-ngoj-a. | ku-za-a. | ku-nunu-a | ku-avy-a |

Pia neno *Aoru* humaanisha kufagia kumwelekea mzungumzaji; Ufuatao ni muhtasari wa mifano ya jozi za vitenzi vinavyoonyesha mwendo kumwelekea mzungumzaji na vinavyoonyesha mwendo mbali na mzungumzaji na sheria zinazotenda kazi.

| *Mwendo kumwelekea mzungumzaji* | | *Mwendo mbali na mzungumzaji* |
|---|---|---|
| 43. *Te-re-u!* – fukuza (upande huu)! | | *Terewai!* - fukuza (upande huu)! |
| R-MZ-KI | u > ai / ----- # | R-MZ-KI |
| b. *Ta-nap-u!* – Beb-a (mzigo) huku! | | *Ta-nap-ai!* – beb-a mzigo (mbali)! |
| R-MZ-KI | u > ai / ------ # | R-MZ-KI |
| c. *Tu-ut-u!* – Elekez-a! (upande huu). | | *Tu-ut-ai* – elekez-a! (mbali) |
| R-MZ-KI | u > ai / ------ # | R-MZ-KI |
| d. *Tu-shuk-u!* - Rudisha! | | Tu-shuk-oi! – rudisha mbali! |
| R-MZ-KI | u > oi / ------ # | R-MZ-KI |
| e. *Me-ta-ng'or-u!* – Arushe huku! | | *Me-ta-ng'or-oi!* – arushe! |
| NF-R-MZ-KI | u > oi / ------ # | NF-R-MZ-KI |

f. *A-te-dek-ua* – Nilimlaani akija huku - *A-te-d-iayie* – nimemlaani (akienda).

NF-WK-MZ-KI NF- WK-MZ-KI

| | |
|---|---|
| e > ia / -y<br>k > y / v - v<br>ua > ie / y- | + irabu<br><br>+mbele |


g. *I-irrag-ua* – Ulilala (ukija). *I-irrag-ayie* – Ulilala (akienda).

NF-MZ KI ua > ayie [+ irabu, + mbele]

h. *I-to-ror-ua* – Ulikanyanga (ukija) *I-to-roru-ayie* – Umekanyanga (ukienda).

NF-WK-MZ-KI NF-WK-MZ-KI

ua > oyie + nyuma [+ irabu, + uviringaji]




i. *E-tu-dung'-uo* – A-li-kat-a (akija). *E-tu-dung'-oiyie* – a-li-kat-ili-a mbali.

NF-WK-MZ-KI NF-WK-MZ-KI

uo > oiyie + nyuma [+ irabu, + uviringaji]

j. *E-to-osh-uo* – A-li-wa-fukuz-a mifugo. *E-to-osh-oiyie* – A-li-wa-fukuz-a mifugo (mbali).

NF-WK-MZ-KI NF-WK-MZ-KI

uo > oiyie [+ irabu, + nyuma, + uviringaji]

k. *A-to-omon-uo* – Ni-li-sal-i (nikija). *A-to-omon-oyie* – Ni-li-sal-i (nikienda).

NF-WK-MZ-KI NF-WK-MZ-KI

$$uo > oiyie \begin{bmatrix} + \text{irabu} \\ + \text{nyuma} \\ + \text{uviringaji} \end{bmatrix}$$

**5.3 Hali tofauti za mnyambuliko wa vitenzi.**

Lugha ya Kimaasai ina minyambuliko minane ya vitenzi, huku kila mnyambuliko ukiwa na seti ya mofimu kadha wa kadha zinazotegemea hali, wakati wa kitendo au nafsi. Hii ni kumaanisha ya kwamba minyambuliko mingi katika lugha hii inaashiriwa na seti za alomofu na wala sio mofimu moja.

**5.3.1 Mnyambuliko ala tendea (Applied au instrumental form)**

Umbo hili la kitenzi huzingatia kitu, mtu au chombo kinachotumiwa kutendea au kutendwa kwa jambo. Mnyambuliko ala tendea unaashiriwa na mofimu yenye alomofu nne; *-ie, -ieki, ishore* na *–ishoreki* zinazo ambishwa kwa mchakato wa uchopekaji tamati. Mnyambuliko huu haupo katika lugha ya Kiswahili na hudhihirika kutegemea muktadha wa matumizi.

(i) Kiishio {-ie}: Kiishio hiki hutamkwa upesi hivi kwamba husikika kama ni /-ye/ na hupatikana katika nyakati zote. Mnyambuliko huu unahusu uchopekaji tamati na kwa hivyo ni matokeo ya sheria hii;

ie / ------ #

Mifano;

*Nafsi ya kwanza:* Katika baadhi ya mifano ifuatayo mofimu ya wakati ni kapa.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 44a. | *A-dung'-ie* | *ki-dung'-ie* | *a-tu-dung-ie* | *ki-tu-dung'-ie* |
| | NF-MZ-MN N | F-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN |
| | nitakata kwa | tutakatia kwa | nilikata kwa | tutakata kwa. |
| b. | *A-rik-ie* | *ki-rik-ie* | *a-to-rik-ie* | *ki-to-rik-ie* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN |
| | nitaongoza kwa | tutaongoza kwa | niliongoza kwa | tutaongoza kwa . |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| c. | *A-kut-ie* | *ki-kut-ie* | *a-tu-kut-ie* | *ki-tu-kut-ie* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN |
| | nitafuta kwa | tutafuta kwa | ilifuta kwa | tulifuta kwa. |

*Nafsi ya pili:*

Katika lugha ya Kimaasai, kitenzi chaweza kuwa katika wakati uliopo, ujao au mazoea ikiwa ni mzizi wenye kiambishi nafsi awali na kiambishi tamati cha mnyambuliko. Katika hali hizi, wingi huwakilishwa na toni ya juu katika kiishio lakini katika othografia huwa hamna mabadiliko yoyote. Kwa wazungumzaji wa lugha hii, dhana ya wingi hudhihirika kiimatumizi. Umbo hili katika nafsi ya pili wingi huhusu uradidi wa silabi ya mwisho ya kiishio. Kiambishi cha nafsi hakibadiliki. Kwa mfano;

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 45a. | *I-gil-ie* | *i-gil-ielie* | *i-ti-gil-ie* | *i-ti-gil-ie* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN |
| | utavunja kwa | mtavunja kwa | ulivunja kwa | mlivunja kwa. |
| b. | *I-dany-ie* | *i-dany-ienyie* | *i-ta-dany-ie* | *i-ta-dany-ie* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN |
| | utatoboa kwa | mtatoboa kwa | ulitoboa kwa | mtatoboa kwa |
| c. | *I-shet-ie* | *i-shet-ie* | *i-te-shet-ie* | *i-te-shet-ie* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN |
| | Utajenga kwa | mtajenga kwa | ulijenga kwa | mlijenga kwa |

Nafsi ya tatu:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| d. | *E-pal-ie* | *e-pal-ie* | *e-ta-pal-ie* | *e-ta-pal-ie* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN |
| | Ataacha kwa | wataacha kwa | aliacha kwa | waliacha kwa |
| e. | *E-oshie* | *e-oshie* | *e-to-osh-ie* | *e-to-osh-ie* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN |
| | atapiga kwa | watapiga kwa | alipiga kwa | walipiga kwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| f. | *E-ning'-ie* | *e-ning'-ie* | *e-to-ning'-ie* | *eto-ning'-ie* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN |
| | Anasikia kwa | wanasikia kwa | atasikia kwa | watasikia kwa |

Mnyambuliko huu katika hali rai nafsi ya pili, vitenzi vya kundi II (vyenye irabu i mwanzoni mwa mzizi) hudhihirisha mfanyiko wa usilimishaji wa vipua na utamkaji dufu kati ya mofimu ya nafsi na sauti inayoanza mzizi.

Katika mfanyiko huu sauti /i/ hudondoshwa na nasali huchopekwa kati ya mofimu ya nafsi na kile kipasuo au kikwaruzo cha kwanza katika mzizi. Jambo hili huibua konsonanti ambatano mwanzoni mwa vitenzi hivi kama vile *mb, mp, nd,* ŋg, *ŋk* na *nych*. Katika mifano ifuatayo itabainika kuwa sauti inayonasalishwa lazima iwe imetamkwa katika mazingira moja na nasali inayohusika. Katika hali kama hii, sauti ya nasali huwa kama kipashio cha kurahisisha na kuharakisha matamshi; jambo lililo la kimsingi katika tamko la rai au amri. (Hali rai haijitokezi katika nafsi ya kwanza, huwa sio kawaida mtu kujirai au kujiamrisha mwenyewe).

Mifano:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 46a. | | b. | |
| *Im-bung-ie!* | *em- bung-ie!* | *Im-pung-ie!* | *em-pung-ie!* |
| R-MZ-MN | R-MZ-MN | R-MZ-MN | R-MZ-MN |
| Shikia! / shika kwa | shikieni kwa! | Tokea / toka kwa | tokeeni toka kwa |
| c. | | d. | |
| *In-chop-ie!* | *en-chop-ie!* | *In-dong'ie!* | *en-dong'ie!* |
| R-MZ-MN | R-MZ-MN | R-MZ-MN | R-MZ-MN |
| Valia! | valieni! | Twangia! / twanga kwa | twangeni kwa |
| e. | | f. | |
| *In- ken-ie!* | *en-ken-ie!* | *In-gany-ie!* | *en- gany-ie!* |
| R-MZ-MN | R-MZ-MN | R-MZ-MN | R-MZ-MN |
| Funga kwa | fungeni kwa | Jazia / jaza kwa | jazani kwa |

Katika nafsi ya tatu hali rai, mnyambuliko huu wa ala-tendea unahusu unasalishaji awali wa mofimu hio ya nafsi kwa nasali /m/ lakini irabu /i/ ya mzizi haidondoshwi. Kwa mfano, vitenzi vilivyotumiwa hapo juu huwa hivi;

g.

| *Me-ibung-ie!* | *Me-ipung-ie!* | *Me-ishop-ie!* | *Me-idong-ie!* |
|---|---|---|---|
| R-MZ-MN | R-MZ-MN | R-MZ-MN | R- MZ-MN |
| washike kwa | watoke kwa | wajivike kwa | watwange kwa |

h.

*(ii)* *Kiishio {–ieki}:*

Kiishio kingine cha mnyambuliko wa ala tendea ni /-ieki/ kinachopatikana katika nyakati zote na ambacho pia huzingatia kifaa kinachotumiwa katika kutendwa kwa jambo. Katika wakati uliopo, ujao na hali mazoea, mofimu ya wakati ni kapa na hudhihirika kiimatumizi. Katika wakati uliopita kiambishi tamati /-ieki/ hutumika pamoja na kiambishi awali *ta, te, ti, to* na *tu* cha wakati uliopita.Viambishi hivi huwa na irabu inayotamkiwa mazingira sawa na ile iliyopo katika shina. Hata hivyo kuna vitenzi vichache ambavyo havihitaji kuchukua kiambishi hiki cha wakati uliopita katika mnyambuliko wowote ule. Mifano ya maneno haya ni; *a-irrag* (ku-lala) – *i-rrag-a* (u-li-lala), a-iken (ku-funga) – *in-ken-o* (ulifunga), a-el (kupaka) – i-el-a (ulipaka) na mengineyo. Kwa mfano,

*Wakati uliopita:*

47a.

| *a-to-osh-ieki* | *ki-to-osh-ieki* | *e-to-osh-ieki* |
|---|---|---|
| NF-WK-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN | NF- WK-MZ-MN |
| Nilipigwa kwa | ulipigwa kwa | alipigwa kwa |

Katika wakati uliopo, ujao na hali mazoea *mo*fimu ya wakati ni kapa. Kwa mfano;

b.

| *a-osh-ieki* | *ki-osh-ieki* | *e-osh-ieki* |
|---|---|---|
| NF- MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| ninapigwa kwa / | unapigwa kwa/ | anapigwa kwa / mtapigwa kwa / |
| nitapigwa kwa | utapigwa kwa | atapigwa kwa / tutapigwa kwa |

(iii) *Kiambishi tamati {ishore}:*

Kiishio hiki ni matokeo ya uchopekaji tamati na hutumika katika nyakati zote na nafsi zote. Hata hivyo, kama itakavyodhihirika katika baadhi ya vitenzi mofimu ya wakati haiashiriwi na mofimu yoyote ila huthibitika tu kipragmatiki.

Katika nafsi ya pili wingi, wakati uliopo, ujao na hali mazoea, silabi ya mwisho /re/ ya kiishio hiki hukaririwa ili kuwakilisha zile nafsi zinazotenda kile kitendo. Ulinganifu wa irabu hudhihirika katika vitenzi vingi. Sheria ya kijumla inayoathiri kiishio hiki ni;

ishore / ----- #

Kwa mfano;

*Nafsi ya kwanza;*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 48a. | *A-dung'-ishore* | *A-tu-dung'-ishore* | *Ki-dung'-ishore* | *Ki-tu-dung'ishore* |
| | NF- MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF- MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| | Ni-na-kat-a kwa / | ni-li-kata kwa | tu-nakata kwa / | tu-li-kata kwa |
| | mimi hu-kata kwa | | sisi hu-kata kwa | |

*Nafsi ya pili:*

| | | | |
|---|---|---|---|
| b. | *I-yeng'-ishore* | *I-te-yeng'-ishore* | *I-yeng'-ishore-re* |
| | NF- MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-MZ-MN-WI |
| | u-na-chinja kwa / | u-li-chinj-a kwa / | m-na-chinj-a kwa / |
| | m-ta-chinj-a kwa | m-li-chinj-a kwa | m-ta-chinj-a kwa |

*Nafsi ya tatu:*

| | | |
|---|---|---|
| c. | *E-dam-ishore* | *E-ta-dam-ishore* |
| | NF- MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| | anakumbuka kwa / | a-li-fikir-i-a kwa/ |
| | wanakumbuka kwa | wa-li-fikir-i-a kwa |
| d. | *E-barn-ishore* | *E-ta-barn-ishore* |
| | NF- MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| | ananyoa kwa/ | a-li-nyo-a kwa / |
| | wa-ta-nyo-a kwa | wa-li-nyo-a kwa |

Katika mnyambuliko huu mnyambuliko wa jinsi ya ala tendea ikiwa nafsi zinazotenda jambo ni nyingi, basi kiambishi *ishore* kinapata kiambishi kingine *ki* cha wingi mwishoni na kuwa /–*ishoreki*/. Kwa hivyo Kiishio hiki hutumika kuelezea kitu au vitu vinavyotumiwa na nafsi ya tatu katika wingi kutendea jambo katika nyakati zote na pia katika hali mazoea. Ni mfano mwingine wa uchopekaji katika mazingira ya tamati. Sheria ya kijumla inayoathiri vitenzi vyenye kiishio hiki ni;

Ishore-ki / ------ #

Kimaasai ni lugha nyambulishi kwa kiwango fulani. Jambo hili linadhihirishwa katika mifano ifwatayo ambapo neno moja linasimamia dhana ambazo katika Kiswahili husimamiwa na maneno mawili. Kwa mfano;

Wakati uliopita:

| | | |
|---|---|---|
| 49a. | *E-tu-dung'-ishore-ki* | *E-ta-ar-ishore-ki* |
| | NF-WK-MZ-MN-WI | NF-WK-MZ-MN-WI |
| | -li-tum-iw-a ku-kat-i-a | -li-tum-iw-a kupigia |
| b. | *E-ta-mayian-ishore-ki* | *E-ta-barn-ishore-ki* |
| | NF-WK-MZ-MN-WI | NF-WK-MZ-MN-WI |
| | -li-tum-iw-a ku-barik-i-a | -li-tum-iw-a ku-nyol-e-a |

Katika vitenzi vingine vyenye kiishio hiki, uchopekaji awali wa kiambishi cha wakati uliopita *ta, te, ti, to,* na *tu* hauhitajiki. Wakati uliopita hudhihirika kiimuktadha. Katika hali kama hii, kitenzi husika kinatumika kiipragmatiki kuelezea matukio ya wakati uliopita, uliopo, ujao na hata mazoea. Sheria ya kijumla inayoadhiri vitenzi hivi ni;

-ishoreki / ------#

*Wakati uliopita, uliopo ujao na mazoea:*

Mifano:

50a.

*E-iger-ishore-ki*

NF-MZ-MN-WI

-li-tum-iw-a ku-andik-i-a/ -na-tum-iw-a ku-andik-i-a/ ta-tum-iw-a ku-andik-i-a/ hu-tum-iw-a ku-andik-a

b.

*E-isuj-ishore-ki-*

NF-MZ-MN-WI

-li-tum-iw-a ku-osh-e-a/ -na-tum-iw-a ku-osh-e-a/ -ta-tum-iw-a ku-osh-e-a/ -hu-tum-iw-a ku-osh-e-a.

c.

*E-ibon-ishore-ki*

NF-MZ-MN-WI

-li-tum-iw-a ku-fany-i-a uganga- -na-tum-iw-a ku-fany-i-a uganga

/-ta-tumiw-a ku-fany-i-a uganga- -hu-tum-iw-a ku-fanyia uganga

**5.3.2 Mnyambuliko wa jinsi ya kutendea / uhusika tendea (The dative form)**

Wazo kuu katika mnyambuliko huu ni "kitendo" kwa niaba au kwa ajili ya mwingine. Mnyambuliko huu pia unaashiriwa na mofimu yenye alomofu kadha wa kadha ambazo kwa kiwango kikubwa zinategemea wakati wa kitendo kutendeka na idadi ya nafsi zinazohusika.

(i) Viishio { *oko / okito*} na {*aka /akita*}:

Kiishio *-oko* ni umoja ilihali *-okito* ni wingi wake. Pia *-aka* ni umoja na *-akita* ni wingi wake.

Katika wingi *-oko* hubadilika kuwa -okito na *-aka* hubadilika kuwa *-akita* kwa kufuata sheria ya ulinganifu wa irabu katika nafsi zote na katika wakati uliopita. Kiambishi *–ta* au *–to* kinachochopekwa mwishoni ni kirejeshi cha kitendewa. Kwa jumla, viishio hivi hufuata sheria hizi;

*Umoja*: oko / ----- #

*Umoja*: oka / ----- #

*Wingi:* okito / ----- #

Wingi: okita / ----- #

*Mabadiliko kutoka umoja hadi wingi:*

oko > okito / ----- # $\begin{bmatrix} +\text{irabu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix}$

aka > akita / ----- # $\begin{bmatrix} +\text{irabu} \\ +\text{mbele} \end{bmatrix}$

51a.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | A-ta-ar-aka | ki-ta-ar-ikita | A-ta-pal-aka | ki-ta-pal-akita |
| | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| | ni-li-pig-il-ia | tu-li-pig-ili-a | ni-li-ach-i-a | u-li-ach-i-a |
| b. | I-to-omon-oko | i-to-omon-okito | I-to-osh-oko | i-to-osh-okito |
| | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| | u-li-omb-e-a | m-li-omb-e-a | u-li-pig-i-a | m-li-pig-i-a |

Vitenzi vifuatavyo ni vya kundi II visivyohitaji kuchopekwa kiambishi awali *ta, te, ti, to* au *tu* vya wakati; *wakati* > Ø, Wingi > Ø.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| c. | *E-ipang'-aka* | *e-ipang'-akita* | *E-ilep-aka* | *e-ilep-akita* |
| | NF- MZ-MN | NF- MZ-MN | NF- MZ-MN | NF- MZ-MN |
| | a-li-tok-e-a | wa-li-tok-e-a | a-li-pand-i-a | wa-li-pand-i-a |

*(ii) Kiambishi { -ikia - ikitia}:*

Katika baadhi ya vitenzi mnyambuliko wa hali ya kutendea pia huwakilishwa na kiambishi *-ikia - ikitia*. –ikia ni umoja na ikitia ni wingi wake na chochopekwa katika mazingira ya tamati. Kiambishi hiki pia hutumika katika nafsi zote na katika wakati uliopita pekee. Sheria za kimsingi zinazotawala katika vitenzi vyenye umbo hili ni:

Umoja: *ikia* / ------ #

Wingi: *ikitia* / ----- #

Mabadiliko kutoka umoja hadi wingi: ikia > ikitia / ----- #

Mifano:

52a.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| *A-te-en-ikia* | *Ki-te-en-ikitia* |
| NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| Ni-li-fung-ĩ-a | tu-li-fung-i-a. |

b.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| *I-to-pon-ikia* | *I-to-pon-ikitia* |
| NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| U-li-ongez-e-a | M-li-ongez-e-a |

c.

| | |
|---|---|
| *E-te-en-ika* | *E-te-en-ikitia* |
| NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| A-me-fung-i-a | wa-me-fung-i-a |

d.

| | |
|---|---|
| *I-te-bel-ikia* | *i-te-bel-ikitia* |
| NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| u-li-vunj-i-a | m-li-vunj-i-a |

(iii) Kiishio {*-iki*}

Hii ni mofimu nyingine ya hali ya kutendea ambayo hujitokeza katika wakati uliopo, ujao na hali mazoea. Mchakato uliopo ni wa uchopekaji tamati na kwa hivyo sheria iliopo ni *iki* / ------- # katika umoja na pia katika wingi. Kwa mfano;

53a.

| | |
|---|---|
| *A-ite-en-iki* | *Ki-nte-en-iki* |
| NF-MT-MZ-MN | NF-MT-MZ-MN |

(*ite* na *nte* ni mofimu tupu, *iki* ni mnyambuliko tendea)

| | |
|---|---|
| Na-singiz-i-a/ni-ta-singiż-i-a/ mimi hu-singiz-i-a | Twa-singiz-i-a/tu-ta-singiz-i-a/sisi hu-singiz-i-a. |

b.

| | |
|---|---|
| *A-en-iki* | *Ki-en-iki* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| Na-fung-i-a/ni-ta-fung-i-a/mimi hu-fung-i-a | twa-fung-i-a/tu-ta-fung-ia/sisi hu-fung-i-a. |

Katika nafsi ya pili mofimu ya wingi inawakilishwa na uradidi wa silabi ya mwisho kama ifuatavyo.

c.

| | |
|---|---|
| *I-nte-en-iki* | *I-nte-en-iki-ki* |
| NF-MT-MZ-MN | NF-MT-MZ-MN |
| u-na-singiz-i-a/u-ta-singiz-i-a/wewehu-singiz-i-a | m-na-singiz-i-a m-ta-singiz-i-a/ nyinyi hu-singiz-i-a. |

d.

| | |
|---|---|
| *I-yen-iki* | *I-yen-ikiki* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| U-na-fung-i-a/u-ta-fung-i-a/ wewe hu-fung-i-a | m-na-fung-i-a - m-ta-fung-i-a/ m-ta-fung-i-a. |

e.

| | |
|---|---|
| *I-ton-iki* | *I-ton-ikiki* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| U-na-ka-a/u-ta-ka-a/wewe hu-ka-a ku-ngoj-e-a | m-na-ka-a/m-ta-ka-a wewe hu-ka-a ku-ngoj-e-a. |

Katika nafsi ya tatu mabadiliko kutoka umoja hadi wingi ni ya kileksia na hayaashiriwi na mabadiliko yoyote ya umbo. Wakati > Ø

f.

| | |
|---|---|
| *E-iten-iki* | *E-iten-iki* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| A-na-singiz-i-a/a-ta-singiz-i-a/yeye hu-singiz-i-a | wa-na-singiz-i-a/wa-ta-singiz-i-a/ wao hu-singiz-i-a. |

g.

| | |
|---|---|
| *E-en-iki* | *E-en-iki* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| a-na-fung-i-a/a-ta-fung-i-a/ yeye hu-fung-i-a | wa-na-fung-i-a w/ a-ta-fung-ia. wao m-ta-fung-i-a. |

h.

| | |
|---|---|
| *E-pet-iki* | *E-pet-iki* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| A-na-lal-i-a/a-ta-lal-i-a/yeye hu-lal-i-a | wa-na-lal-i-a/ /wa-ta-lal-i-a/ waohu-lal-i-a. |

Kiishio *-iki* pia hutumika katika hali rai. Kama ilivyotajwa hapo awali sio kawaida mtu kujirai mwenyewe, labda awe na nafsi zingine pamoja naye ambapo mofimu ya nafsi ya kwanza wingi *ki* hubadilika kileksia na kuwa *ma*.

Katika nafsi ya pili umoja na wingi hali rai inahusu unasalishaji tamati (*post-nasalisation*) wa mofimu ya nafsi ilihali katika nafsi ya tatu mofimu ya nafsi hubadilika kutoka *e* na kuwa *me* katika umojá na pia katika wingi. Pia katika nafsi zote, kiambishi {*ta*}. {*te*, {*to*} na {*tu*} huchopekwa huku irabu zikilingana kuwakilisha rai. Mifano;

Nafsi ya kwanza;

| | | | |
|---|---|---|---|
| 54a. | *Ma-te-en-iki!* | *Ma-te-pet-iki!* | *Ma-to-pon-iki!* |
| | NF-R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN |
| | Tu-fung-i-e! | Tu-lal-i-e! | Tu-ongez-e-e! |

Nafsi ya pili;

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| b. | *Te-en-iki!* | *En-te-en-iki!* | *Te-pet-iki!* | *En-te-pet-iki!* |
| | NF-R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN | R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN |
| | Fung-i-a! | Fung-ie-ni! | Lal-i-a! | Lal-ie-ni! |

Nafsi ya tatu;

| | | | |
|---|---|---|---|
| c. | *Me-te-en-iki!* | *Me-te-pet-iki!* | *Me-to-ton-iki!* |
| | NF-R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN |
| | A-fung-i-e! / Wa-fung-i-e! | A-lal-i-e / wa-lal-i-e! | A-keti a-ngoj-e-e! / Wa-ket-i wa-ngoj-e-e! |

*(iv) Kiishio {–aki / -oki}:*

Kiishio kingine cha mnyambuliko huu wa jinsi ya kutendea ni *–aki / -oki* ambacho hutumika katika wakati uliopo, ujao na pia hali mazoea. Huu ni mfano mwingine wa uchopekaji tamati unaotii sheria ya ulinganifu wa irabu na hutumika katika nafsi zote. Sheria ya kijumla inayotawala vitenzi vyenye umbo hili ni;

$$\text{aki} \; / \; \text{------} \; \# \begin{bmatrix} + \text{irabu} \\ + \text{mbele} \end{bmatrix}$$

$$\text{oki} \; / \; \text{------} \; \# \begin{bmatrix} + \text{irabu} \\ + \text{nyuma} \end{bmatrix}$$

| | | |
|---|---|---|
| 55a. | *A-ilep-aki*<br>NF-MZ-MN<br>Ninapandia/<br>mimi hupandia | *ki-lep-aki (Wakati > Ø)*<br>NF-MZ-MN<br>Tunapandia /<br>tutapandia/sisi hupandia. |
| b. | *A-osh-oki*<br>NF-MZ-MN<br>Ninapigia/nitapigia/mimi hupigia | *ki-osh-oki*<br>NF-MZ-MN<br>Tunapigia /tutapigia/sisi hupigia. |
| c. | *E-ilep-aki*<br>NF-MZ-MN<br>A-na-pand-i-a/a-ta-pand-i-a/yeye hu-pand-i-a | *E-ilep-aki*<br>NF-MZ-MN<br>Wa-na-pand-i-a/<br>wa-ta-pand-i-a/wao hu-<br>pand-i-a. |
| d. | *E-osh-oki*<br>NF-MZ-MN<br>A-na-pig-i-a/ a-ta- pig-i-a<br>/ yeye hu-pig-i-a | *E-osh-oki*<br>NF-MZ-MN<br>Wa-na-pig-i-a/wa-ta-pig-<br>i-a / wao hu-pig-i-a. |

Kama ilivyotajwa hapo awali wingi katika nafsi ya pili unahusu uradidi wa silabi ya mwisho. Kwa mfano; *Wakati* > Ø

e.

| | |
|---|---|
| *-lep-aki* | *I-lep-aki-ki* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN-WI |
| U-na-pand-i-a/u-ta-pand-i-a/wewe hu-pand-i-a | M-na-pand-i-a/m-ta-pand-i-a. nyinyi hu-pand-i-a. |

f.

| | |
|---|---|
| *I-osh-oki* | *I-osh-oki-ki* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN-WI |
| U-na-pig-i-a/u-ta-pig-i-a/wewe hu-pig-i-a | M-na-pig-i-a/m-ta-pig-i-a/nyinyi hu-pig-ia |

g.

| | |
|---|---|
| *I-wang'-aki* | *I-wang-aki-ki* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN-WI |
| U-na-ondok-e-a/m-ta-ondok-e-a | M-na-ondok-e-amta-ondok-e-a |

Kiishio –aki /-oki pia hutumika katika hali rai ambapo mofimu ya nafsi hudondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na mofimu ya rai inayotegemea nafsi inayoamrishwa. Mifano;

*Nafsi ya kwanza;*

Kama ilivyotajwa hapo awali, huwa sio kawaida mtu kujiamrisha au kujirai mwenyewe labda awe na nafsi zingine pamaja naye. Kwa mintarafu hii basi rai katika nafsi ya kwanza hujitokeza tu katika wingi kama ifuatavyo;

| 57a. | b. | c. |
|---|---|---|
| *Ma-ilep-aki!* | *Ma-to-osh-oki!* | *Ma-iwang'-aki!* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-R-MZ-MN |
| Tu-pand-i-e! | Tu-pig-i-e! | Tu-ondok-e-e! |

*Nafsi ya pili;*

Katika vitenzi vya kundi I, mofimu ya nafsi hunasalishwa na kiambishi *ta, te, ti, to* au *tu* huchopekwa ili kuwakilisha rai. Katika baadhi ya vitenzi vya kundi II, mofimu za umbo hufuata utaratibu wa kawaida katika umoja na katika wingi ilihali katika vitenzi vingine kuna udondoshi au unasalishaji wa mofimu ya nafsi.

*Kundi I*

| 58a. | | b. | |
|---|---|---|---|
| *To-osh-oki!* | *En-to-osh-oki!* | *Te-lej-aki!* | *En-te-lej-aki!* |
| R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN | R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN |
| Pigi-a! | pigi-e-ni! | Dangany-i-a! | Dangany-i-eni! |

| b. | | c. | |
|---|---|---|---|
| *To-omon-oki!* | *En-to-omon-oki!* | *Ta-ar-aki* | *En-ta-ar-aki* |
| R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN | R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN |
| Omb-e-a! | Omb-e-eni! | Pig-ili-a | pig-ili-eni |

Katika vitenzi vya kundi II hakuna uchopekaji wa mofimu *ta, te, ti,* to *na tu* ya wakati.

| d. | | e. | |
|---|---|---|---|
| *I-lep-aki!* | *E-lep-aki!* | *Im-pot-oki!* | *Em-pot-oki!* |
| R-MZ-MN | R-MZ-MN | R-MZ-MN | R-MZ-MN |
| Pand-i-a! | Pand-i-eni! | It-i-a! | It-i-eni! |

| f. | | g. | |
|---|---|---|---|
| *Im-pung'-oki!* | *Em-pung'-oki!* | *Im-bun'g-aki* | *Em-bung'-aki* |
| R-MZ-MN | R-MZ-MN | R-MZ-MN | R-MZ-MN |
| Tok-e-a! | Tok-e-eni! | Shik-i-a | Shik-i-eni |

Katika *Nafsi ya tatu* hali rai, kiambishi cha nafsi *e* hubadilika na kuwa *me* ili kuwakilisha dhana ya rai na pia nafsi inayoraiwa. Kiambishi huakilisha umoja na pia wingi umoja na pia katika wingi. Kiambishi awali *-to-* cha rai kimechopekwa. Mofimu ya wakati ni kapa:

Mifano:

59. a. b.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *Me-to-osh-oki!* | *Me-iwang'-aki!* | *Me-ta-pej-oki!* | *Me-te-lej-aki!* |
| NF-R-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN |
| A-pig-i-e! / | A-ondok-e-e! / | A-chom-ee! / | A-dangany-i-e! / |
| Wa-pig-i-e! | Wa-ondok-e-e! | Wa-chom-e-e! | Wa-dangany-i-e! |

Mofimu yá rai Katika kitenzi *Me-iwang'-aki* ni kapa.

*(v) Kiishio {–aa / -oo};*

Hii ni mofimu nyingine ya mnyambuliko wa jinsi ya kutendea inayofuata sheria ya ulinganifu wa irabu na huelezea dhana ya kutendea jambo kuelekea mbali na mnenaji. Kiishio hiki hutumika katika wakati uliopo, ujao na hali mazoea. Sheria za kijumla zinazotawala vitenzi vyenye umbo hili ni;

aa / ------- # [+ irabu, + mbele]

*/-oitie/ au /-aitie/.*

oo / ------- # [+ irabu, + nyuma]

Mifano;

Mofimu ya wakati hapa ni kapa na hutokea katika nafsi zote. Kwa mfano;

*Nafsi ya kwanza*

60. a. b.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-pal-aa* | *Ki-pal-aa* | *A-itoip-oo* | *Kin-toip-oo* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| Ni-na-ach-i-a | Tu-na-ach-i-a | Ni-na-funik-i-a | tu-na-funik-i-a |

*Nafsi ya pili*

c. d.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-tur-oo* | *Ki-tur-oo* | *A-suj-aa* | *ki-suj-aa* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| Ni-na-chimb-i-a | Tu-na-chimb-i-a | Ni-na-fuat-i-a | Tu-na-fuat-i-a |

*Nafsi ya tatu;*

| e. | | f. | |
|---|---|---|---|
| E-*pal-aa* | E-*pal-aa* | *E-itoip-oo* | *E-itoip-oo* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| A-na-ach-i-a | Wa-na-ach-i-a | A-na-funik-i-a | Wa-na-funik-i-a |

### 5.3.3 Mnyambuliko wa jinsi ya kutendesha

Dhima kuu ya mnyambuliko huu ni kusababisha mtu au kitu kutenda kitendo katika kitenzi. Umbo hili ni mojawapo ya maumbo yanayotatanisha zaidi katika lugha ya Kimaasai kwa kuwa ndio mnyambuliko wa pekee unaotambulishwa na viambishi awali katika idadi kubwa ya vitenzi. Viambishi awali hivi ni, *-it, -nt-, i, imp-, imb-, inch-* na *ink-*. Kuna mifano michache hata hivyo, ambayo licha ya kuwa na viambishi awali pia hupata viambishi tamati mahsusi kama itakavyoelezewa baadaye.

*Kiambishi awali {-it}:*

Hutumika katika nyakati zote na katika nafsi ya kwanza umoja na nafsi ya tatu umoja na pia wingi. Kwa sababu ya kuwako kwa irabu /i/ katika kiambishi hiki vitenzi vyote hupata muundo wa vitenzi vya kundi II. Pia kuna uchopekaji wa kile Anderson (1992) anachokiita mofu-tupu (*empty morphs)* inayosimamiwa na irabu inayolingana na ile ya shina. Vitenzi vya umbo hili vilivyo katika wakati uliopo hupata viambishi tamati /-ita/ au /-ito/ huku ikitegemea kama irabu ya shina ni ya mbele au ya nyuma; /-ita/ ni ya vitenzi vyenye irabu za mbele na /-ito ni ya vitenzi vyenye irabu za nyuma. Sheria inayotendakazi ni; (it / # ------)
*Wakati* > Ø
Kwa mfano;

*Nafsi ya kwanza;*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 61a. | *A-it-u-jut-o /* | *A-it-u-jut-ito* | *A-it-u-jut* |
| | NF-MN-MT-MZ-KI | NF-MN-MT-MZ-KI | NF-MN-MT-MZ |
| | nilipangusisha / | ninapangusisha | nitapangusisha / mimi hu-pangusisha. |
| b. | *A-it-o-osh-o* | *A-it-o-osh-ito* | *A-it-o-osh* |
| | NF-MN-MT-MZ-KI | NF-MN-MT-MZ-KI | NF-MN-MT-MZ |

ni-li-pig-ish-a. ninapigisha nitapigisha/mimi hupigisha

*Nafsi ya tatu;*

| | | | |
|---|---|---|---|
| c. | *E-it-a-l-aa.* | *E-it-a-lak-ita* | *E-it-a-lak* |
| | NF-MN-MT-MZ-KI | NF-MN-MT-MZ-WK | NF-MN-MT-MZ |
| | a-li-lip-iz-a/ | a-na-lip-iz-a | a-ta-lip-iz-a / |
| | wa-li-lip-iz-a / | wa-li-lip-iz-a. | yeye /wao hu-lip-iz-a/ |
| | | | wa-ta-lip-iz-a |

| | | | |
|---|---|---|---|
| d. | *E-it-o-t-io* | *E-it-ot-ito* | *E-it-oti* |
| | NF-MN-MT-MZ-KI | NF-MN-MT-MZ-KI | NF-MN-MT-MZ |
| | a-li-l-ish-a | analisha | atalisha |
| | wa-li-l-ish-a. | wanalisha | yeye/wao hulisha |

*(ii) Mofimu {–nt};*

Mnyambuliko wa jinsi ya kutendesha pia huwakilishwa na kiambishi awali *-nt* katika nafsi ya kwanza na ya pili wingi nyakati zote, na hali rai. Hapa pia, sifa ya kiarudhi ya toni inapata umuhimu wa kimofemiki hasa pale kitenzi hubadilisha maana bila ya kubadilika umbo.

Katika baadhi ya vitenzi vyenye nafsi ya kwanza wingi, wakati uliopita kiishio tamati *-itia* ambacho ni kirejeshi cha nafsi, ilihali *-utua* hutumika kuelezea kitendo kinachomwelekea msemaji. Katika wakati uliopo umoja, kiishio tamati *–ita* au *-ito* ni mofimu ya wakati uliopo na hufuata sheria ya ulinganifu wa irabu. Katika wingi hata hivyo, silabi ya mwisho katika *–ita* na *–ito* hukaririwa kuwa *-itata* au *–itoto* ili kuashiria wingi. Kishio hiki sio cha mnyambuliko bali ni cha kuashiria mwendo mbali au kumwelekea mzungumzaji. Sheria inayotawala alomofu *-nt* ya kutendesha ni;

*-nt* / # -------

Tazama vielelezo hivi;

62a.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *I-**nt**-a-lam-a* | *I-**nt**-a-lam-a!* | *I-nt-a-lam* | *I-nt-a-lam-ita* |
| NF-MN-MT-MZ-KI | NF-MN-MT-MZ-KI | NF-MN-MT-MZ | NF-MN-MT-MZ-KI |
| u-li-ondo-*sh*-a / | Ondo-sh-a ! | u-ta-ondo-sh-a | u-na-ondo-sh-a |

| | | | |
|---|---|---|---|
| *Ki-**nt**-a-lam-aitie* | *Ki-**nt**-a-lam-ita* | *Ki-**nt**-a-lam* | *I-nt-a-lam-itata* |
| NF-MN-MT-MZ-KI | NF-MN-MT-MZ-WK | NF-MN-MT-MZ | NF-MN-MT-MZ-KI |
| tu-li-ondo-*sh*-a | tu-na-ondo-*sh*-a | tu-ta-ondo-*sh*-a | m-na-ondo-sh-a mbali |

(Mabadiliko ya kimaana huashiriwa na mabadiliko ya toni)

| | | | |
|---|---|---|---|
| b. | *Ki-nt-a-lak-utua* | *Ki-nt-a-lak-ita* | *Ki-nt-a-lak* |
| | NF-MN-MT-MZ-KI | NF-MN-MT-MZ-WK | NF-MN-MT-MZ |
| | tu-li-lip-iz-a. | tu-na-lip-iz- a. | tu-ta-lip-iz-a |
| c. | *I-nt-a-l-aa* | *I-nt-a-l-aa!* | *I-nt-a-lak* |
| | NF-MN-MT-MZ-KI | NF-MN-MT-MZ-KI | NF-MN-MT-MZ |
| | u-li-lip-iz-a / m-li-lip-iz-a. | Li-piz-a! | u-ta-lip-iz-a. |

(Mabadiliko ya kimaana huashiriwa na mabadiliko ya toni)

*(iii) Kiambishi awali {–i}:*

Katika baadhi ya vitenzi mofimu inayoashiria hali ya kutendesha ni kiambishi awali *–i-* katika nafsi ya kwanza umoja na ya tatu katika nyakati zote. Katika nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili umoja na wingi, maana ya hali ya kutendesha huashiriwa na irabu awali *i* baada ya mofimu ya nafsi.

i / # ------

Mifano;

(i) Mofimu {i}:

63a.

| | |
|---|---|
| *A-**i**-bung-ie* | *E-**i**-bung-ie* |
| NF-MN-MZ-KI | NF-MN-MZ-KI |
| ni-li-shik-ish-a / ni-ta-shik-ish-a | a-ta-shik-ish-a/ yeye hu-shik-ish-a. |

b.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-i-shop-oko* | *A-i-shop-oki* | *E-i-shop-oko* | *E-i-shop-oki* |
| NF-MN-MZ-WK | NF-MN-MZ-WK | NF-MN-MZ- WK | NF-MN-MZ- WK |
| ni-li-va-lish-a. | ni-ta-va-lish-a / mimi hu-va-lish-a. | a-li-va-lish-a. | a-ta-va-lish-a / yeye hu-va-lish-a. |

c.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-i-dik-o* | *A-i-dik-ito* | *A-i-dik* | *E-i-dik-o* |
| NF-MN-MZ-KI | NF-MN-MZ-WK | NF-MN-MZ | NF-MN-MZ-KI |
| ni-li-ungan-ish-a. | ni-na-ungan-ish-a. | ni-ta-ungan-ish-a / mimi hu-ungan-ish-a. | a-li-ungan-ish-a. |

(iv) Unasalishaji wa Konsonanti inayoanza shina;

Mnyambuliko wa jinsi ya kutendesha pia huashiriwa na unasalishaji wa konsonanti inayoanza shina.

Mfanyiko huu unaadhiri tu vitenzi vya kundi II ambapo irabu *i* inayotangulia mizizi inadondoshwa huku kipasuo au kikwaruzo kinachofuatia kikinasalishwa. Utaratibu ni kwamba, nasali inayotumika sharti itoke katika mazingira moja na konsonanti inayonasalishwa; nasali za mdomo hunasalisha konsonanti za mdomo, za ufizi hunasalisha za ufizi, nasali ya kaakaa ngumu hunasalisha konsonanti za kaakaa ngumu ilihali ya kaakaa laini hunasalisha konsonanti ya kaakaa laini. Sheria inayodhihirika katika vielelzo vifwatavyo ni;

+ nasali / # -------

Mifano;

*Nasali {m}*

$$i > m \left[\begin{array}{l} + \text{konsonanti} \\ + \text{mdomo} \end{array}\right]$$

64a.

*I-m-bung'-ie*

NF-MN-MZ-KI

Shik-ish-a! /

u-li-shik-ish-a

| b. | *I-m-posh-a* | *I-m-posh* | *I-m-posh-ita* | *I-m-posh-ie* |
|---|---|---|---|---|
| | NF-MN-MZ-KI | NF-MN-MZ | NF-MN-MZ-WK | NF- MN-MZ-KI |
| | Tik-is-a! / | u-ta-tik-is-a / | u-na-tik-is-a. | u-li-tik-is-a kwa |
| | u-li-tik-is-a. | wewe hutikisa | | (*-ie* ni kwa) |
| | (wakati uliopita ni kapa.) | | | |

*Nasali* {*ń*}
Unasalishaji kwa kutumia nasali *n;*

i > n [+ konsonanti, + kaakaa lain]

| c. | I-n-chop-oko. | I-n-chop-oki! |
|---|---|---|
| | NF-MN-MZ-KI | NF-MN-MZ-KI |
| | u-li-val-ish-a. | Va-lish-a! |

Sauti *n* katika *inchopoki* na *inchopoko* hutamkwa kama *ny*. Maana katika *inchopoki* hubainika kwa kubadilika kwa toni.

| d. | *I-n-dik* | *I-n-dik-o*! | *I-n-dik-ito* |
|---|---|---|---|
| | NF-MN-MZ | NF-MN-MZ-KI | NF-MN-MZ-WK |
| | u-ta-ungan-ish-a / | Ungan-ish-a! / | u-na-ungan-ish-a. |
| | wewe hu-ungan-ish-a. | u-li-ungan-ish-a. | |

(Tofauti ya kimaana hapa hubainika kwa kubadilika kwa toni).

**5.3.4 Mnyambuliko wa jinsi ya kutendwa na kutendewa (passive form).**

Umbo hili huonyesha kitendo kilichofanywa au kufanyiwa mtu au kitu. Mnyambuliko huu huashiriwa na mofu za tamati tofautitofauti katika nyakati tofauti na hali tofauti. Mofimu ya mnyambuliko huu ina alomofu nane ambazo hugawika katika makundi matatu kama ifuatavyo kulingana na wakati wa kutendwa kwa kitenzi. Baadhi ya alomofu hizi hujitokeza katika jozi na kudhihirisha ulinganifu wa irabu uliopo. iishio *-uaki* no *–uoki* hueleza vitenzi vinavyoonyesha mwendo kumwelekea mzungumzaji.

*Wakati uliopita:*

Katika wakati uliopita mnyambuliko huu una alomofu tano;

- *-uaki / -ouki.*
- *-ayioki / -oyioki.*
- *-aki / -oki.*
- *-kaki /-koki*
- *-no.*

Mifano;

*(i) Kiambishi tamati {–uaki / -uoki/ -ayoki / -oyoki}:*

Viishio hivi hudhihirisha ulinganifu wa irabu ambapo huchukua irabu inayolingana na ile iliyopo katika mzizi wa kitenzi. Maumbo haya hudokeza dhana ya mwendo unaomwelekea mzungumzaji au unaoelekea mbali na mzungumzaji ingawa mofimu ya mwendo ni kapa.

Kama ilivyodhihirika katika mnyambuliko wa jinsi ya kutedesha, vilevile katika mnyambuliko huu baadhi ya vitenzi vina uchopekaji wa mofimu tupu *i* au *n* kabla au baada ya mofimu ya wakati uliopita *ta, te, ti, to* au *tu*. Umbo *–auki / -uoki* huelezea vitenzi vya jinsi ya kutendwa vinavyomwelekea mzungumzaji. Katika vitenzi vinavyoonyesha mwendo mbali na mzungumzaji *-uaki* hubadilika na kuwa *–ayoki* ilihali *–uoki* huwa *–oyoki;*. Sheria zilizopo ni;

uaki / ------- # [+ irabu, +mbele]

uoki / ------- # [± irabu, ±nyuma]

uaki > ayoki / ------- # [+ irabu, +mbele]

uoki > oyoki -------- # [+ irabu, + uyuma, + uviringaji]

| | |
|---|---|
| *Kumwelekea mzungumzaji.* | *kueleka mbali na mzungumzaji.* |

65a.

| | |
|---|---|
| *A-i-to-bir-uaki* | *A-i-to-bir-ayoki* |
| NF-MT-WK-MZ-MN | NF-MT-WK-MZ-MN |
| ni-li-tend-wa / ni-li-tend -ew-a vizuri | ni-li-tend-w-a / ni-li-tend-ew-a vizuri |
| nkija | nikienda |

b.

| | |
|---|---|
| *E-ta-bol-uoki* | *E-ta-bol-oyoki* |
| NF-WK- MZ-MN | NF-WK- MZ-MN |
| a-li-fung-uliw-a akija | alifunguliwa akienda |

(ii) Kiishio {aki/ oki};

Katika wakati uliopita baadhi ya vitenzi katika mnyambuliko tendwa/tendewa huchukua viambishi /-aki/ au /-oki/ huku mfanyiko wa ulinganifu wa irabu ukidhihirika. Sheria zidhihirikazo ni;

aki / -------- # [+ irabu, + mbele]

oki / ------- # [+ irabu, + nyuma]

Mifano:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 66a. | *A-to-osh-oki* | *Ki-to-osh-oki* | *E-to-osh-oki* |
| | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ- MN | NF-WK-MZ-MN |
| | ni-li-pig-w-a. | u-li-pig-w-a. | a-li-pig-w-a. |
| b. | *A-te-lej-aki* | *Ki-te-lej-aki* | *E-te-lej-aki* |
| | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| | ni-li-dangany-w-a. | u-li-dangany-w-a. | a-li-dangany-w-a |

(iii) Kiishio {-koki/-kaki};

Vitenzi vingine vya navyo huchukua viambishi tamati *-koki* au *-kaki* vya hali ya *tendewa/tendewa* katika wakati uliopita pia vikidhihirisha ulingaifu wa irabu. Umbo hili huwa limetokana na-lile lililojadiliwa hapo awali la *-aki* na *–oki* la hali ya tendwa. Umbo hili halisababishi kudondoshwa kwa kiishio cha shina. Ugeuzaji umbo hapa hufuata sheriahizi kama inavyodhihirishwa na vielelezo vifuatavyo;

aki > kaki / -------------- # [+ irabu, + mbele]

oki > koki / ------------ # [+ irabu, + nyuma]

67a.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-iger-oki* | *A-iger-o-koki* | *A-ta-pal-aki* | *a-ta-pal-a-kaki* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MT-MN | NF-WK MN | NF-WK-MZ- MT-MN |
| ni-li-andik-w-a. | ni-li-andik-iw-a. | ni-li-ach-w-a. | ni-li-ach-iliw-a |

b.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *Ki-nger-oki* | *Ki-nger-o-koki* | *Ki-te-lej-aki* | *Ki-te-lej-a-kaki* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MT-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-MZ-MT-MN |
| u-li-andik-w-a. | u-li-andik-iw-a. | u-li-dangany-w-a | u-li-dangany-iw-a |

c.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *E-tu-buk-w-oki* | *E-tu-buk-o-koki* | *E-ibung-aki* | *E-ibung-a-kaki* |
| NF-WK-MZ-MT-MN | NF-WK-MZ-MT-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MT-MN |
| -li-mwag-w-a | a-li-mwag-iliw-a. | a-li-shik-w-a | a-li-shik-iw-a |

*(iv) Kiishio {uno}*

Umbo lingine linalowakilisha jinsi ya kutendwa ni kiambishi tamati *–uno* ambacho kando na kuelezea dhana ya kutendwa katika wakati uliopita pia husizitiza au hukariri kitendo. Kwa mfano;

| | | | |
|---|---|---|---|
| 68a. | *A-rik-uno* | *I-rik-uno* | *E-rik-uno* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | ni-ii-let-w-a / | u-li-let-w-a / | a-li-let-w-a / |
| | ni-me-o-lew-a kikweli | u-me-o-lew-a kikweli | a-me-o-lew-a kikweli |
| b. | *A-i-uno* | *I-i-uno* | *Ke-i -uno* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| | ni-li-za-liw-a hasa. | u-li-za-liw-a / hasa. | a-li-za-liw-a hasa. |
| c. | *E-shet-uno* | *E-iger-uno* | *E-yer-uno* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| | i-me-jeng-w-a sawasawa. | i-lia-ndik-w-a sawasawa. | -li-pik-w-a vilivyo. |

(v) Itoi /itai

Katika wakati uliopo mnyambuliko tendwa au tendewa huashiriwa na kiambishi kimoja pekee ambacho ni kiambishi tamati -itoi au –itai. Kiambishi hiki hutawaliwa na sheria ya ulinganifu wa irabu hivi kwamba, ikiwa irabu ya awali au ya shina ni ya mbele nayo ile ya mnyambuliko inakuwa ya mbele. Ikiwa ni ya nyuma, ile ya mnyambuliko nayo inakuwa ya nyuma.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 69a. | *A-osh-itoi* | *Ki-dung-itoi* | *E-iger-itoi* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| | Ni-na-pig-w-a. | ni-na-kat-w-a | Ki-na-andik-w-a |
| b: | *A-pal-itai* | *Ki-mir-itai* | *E-iba-itai* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| | Ni-na-ach-w-a | u-na-fukuz-w-a | a-na-chuk-iw-a. |

*(vi) Kiishio {-ari/-ori}:*

Viishio tamati *-ari* au *-ori* huwakilisha mnyambuliko wa jinsi ya kutendwa/tendewa katika wakati ujao, mazoea na pia hali rai. Viambishi hivi pia hutii sheria ya ulinganifu wa irabu hivi;

ari / ——— # [+ irabu, +mbele]

Hapa dhana ya wakati na mwendo unaoelekea mbali na mzungumzaji ni kapa. Tazama vielelezo vifuatavyo;

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 70a. | *A-rik-ori* | *Ki-rik-ori* | *E-rik-ori* | *Me-to-rik-ori!* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-R-MZ-MN |
| | ni-ta-ongoz-w-a . | u-ta-ongoz-w-a . | hu-ongoz-w-a. | A-ongoz-w-e! |
| b. | *A-mir-ari* | *Ki-mir-ari* | *E-mir-ari* | *Me-ti-mir-ari!* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-R-MZ-MN |
| | ni-ta-fukuz-w-a | u-ta-fukuz-w-a | a-ta-fukuz-w-a | Afukuzwe! |
| c. | *A-rrum-ori* | *Ki-rrum-ori* | *E-rrum-ori* | *Me-tu-rrum-ori!* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-R-MZ-MN |
| | Ni-ta-sukum-wa | u-ta-sukum-wa | -ta-sukum-w-a | a-sukum-w-e! |
| d. | *A-ibung-ari* | *Ki-mbung-ari* | *E-ibung'-ari* | |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | |
| | ni-ta-shik-iliw-a | u-ta-shik-iliw-a | a-ta-shik-iliw-a | |

*(vii) Kiishio {-uni}*

Mnyambuliko tendwa/tendewa pia waweza kuwa na viambishi tamati au *-i* katika wakati ujao, hali mazoea na pia katika hali rai ambapo sheria ifuatayo hufanya kazi:

uni / ______ #

Vitenzi vyenye umbo *–uni* huashiria mwendo wa kumwelekea mzungumzaji ingawa dhana ya wakati ni kapa. Kwa mfano;

80a.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-asuj-uni* | *Ki-suj-uni* | *E-suj-uni* | *Ma-a-tu-suj-uni!* |
| NF-WT-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MT-R-MZ-MN |
| ni-ta-fuat-w-a / | u-ta-fuat-w-a / | A-ta-fuat-w-a | ni-fuat-w-e! |
| mimi hu-fuat-w-a. | wewe hu-fuat-w-a. | yeye hu-fuat-w-a. | |

b.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-wap-uni* | *Ki-wap-uni* | *E-wap-uni* | *Me-ta-wap-uni!* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-R-MZ-MN |
| ni-ta-vut-w-a / | u-ta-vut-w-a / | -ta-vut-w- a / | A-vut-w-e upesi! / |
| mimi hu-vut-w-a. | wewe u-ta-vut-w-a. | hu-vut-w-a. | I-vut-w-e upesi! |

c.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-ibung'-uni* | *Ki-mbung'-uni* | *Eibung-uni* | *Me-ibung-uni!* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF -MZ-MN |
| Ni-ta-shik-iliw-a | u-ta-shik-iliw-a | a-ta-shik-iliw-a | A-shik-iliw-e! |

Hapa mofimu ya rai ni kapa.

*(viii) Kiambishi tamati {–akini, -okini* au *-ikini}*

Viishio hivi huashiria mnyambuliko wa hali ya kutendewa katika hali mazoea. Uteuzi wa viishio hivi hutegemea irabu inayomalizia shina la kitenzi husika. Sheria zinazotawala kiishio hiki ni;

akini / -------- #
okini / -------- #
ikini / -------- #

*Mifano;*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 81. | *A-iger-okini* | *Ki-nger-okini* | *Ei-ger-okini* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| | Ni-ta-andik-iw-a / | U-ta-andik-iw-a | a-ta-andik-iw-a / |
| | mimi ni-ta-andik-iw-a. | wewe hu-andik-iwa. | yeye hu-andik-iw-a. |

Sauti *i* katika kingerokini ambacho ni kitenzi cha kundi II hubadilika na kuwa *n* kwa sababu konsonanti inayoifuatia ni *g* ya kaakaa laini.

$$i > n \left[\begin{array}{l} +\text{ konsonanti} \\ +\text{ kaakaa laini} \end{array}\right]$$

| | | | |
|---|---|---|---|
| 82a. | *A-osh-okini* | *Ki-osh-okini* | *E-osh-okini* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| | ni-ta-pig-iw-a / | u-ta-pig-iw-a / | a-ta-pig-iw-a / |
| | mimi hu-pig-iw-a. | wewe hu-pig-iw-a. | yeye hu-pig-iw-a. |
| b. | *A-mir-akini* | *Ki-mir-akini* | *E-mir-akini* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| | ni-ta-uz-iw-a / | u-ta-uz-iw-a / | a-ta-uz-iw-a / |
| | mimi hu-uz-iw-a. | wewe u-ta-uz-iw-a. | yeye a-ta-uz-iw-a. |
| c. | *A-dung'-okini* | *Ki-dung'-okini* | *E-dung'-okini* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| | ni-ta-kat-iw-a / | u-ta-kat-iw-a / | a-ta-kat- iw-a / |
| | mimi hu-kat-iw-a. | wewe hu-kat-iw-a. | yeye hu-kat-iw-a. |
| d. | *A-en-ikini* | *Ki-en-ikini* | *E-en-ikini* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| | ni-ta-fung-iw-a / | u-ta-fung-iw-a / | a-ta-fung-iw-a / |
| | mimi hu-fung-iw-a. | wewe hu-fung-iw-a. | yeye hu-fung-i-a. |

### 5.3.5 Mnyambuliko wa jinsi ya kutendana/ kutendeana

Lodhi (2002) anauita mnyambuliko huu *'associative / reciprocal form'*. Mnyambuliko huu humaanisha vitu viwili au zaidi hutendana au hutendeana jambo. Kwa mintarafu hii myambuliko huu hushirikisha watu au vitu zaidi ya kimoja. Mnyambuliko huu pia huwakilishwa na viambishi tamati kadha kutegemea nyakati na hali tofauti.

*(i) Kiishio {-kinote au –unote};*

Kiishio hiki hudhihirisha ule ukamilifu wa kutekelezeana jambo/ kitendo katika wakati uliopita. Uteuzi wa *–kinote* au *–unote* katika kitenzi chochote kile ni wa kileksia na haufuati utaratibu wowote wa kifonemiki. Katika baadhi ya vitenzi kiishio cha shina hakidondoshwi kabla ya kuambishwa umbo hili la mnyambuliko. Sheria za kijumla zinazotawala kiishio hiki ni;

kinote / -------- #

unote / -------- #

Mifano;

| | | | |
|---|---|---|---|
| 83a. | *Ki-ta-pal-a-kinote* | *I-ta-pal-a-kinote* | *E-ta-pal-a-kinote* |
| | NF-WK-MZ-MT-MN | NF-WK-MZ-MT-MN | NF-WK-MZ-MT-MN |
| | tu-li-sameh-ean-a / tu-li-ach-ani-a. | m-li-sameh-ean-a. | wa-li-sameh-ean-a. |
| b. | *Ki-mba-y-unote* | *I-mba-y-unote* | *E-iba-y-unote* |
| | NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-MZ-MT-MN |
| | tu-li-chuk-ian-a. | m-li-chuk-ian-a. | wa-li-chuk-ian-a. |
| c. | *Ki-tu-rrum-o-kinote* | *I-tu-rrum-o-kinote* | *E-tu-rrum-o-kinote* |
| | NF-WK-MZ-MT-MN | NF-WK-MZ-MT-MN | NF-WK-MZ-MT-MN |
| | tu-li-sukum-ian-a. | m-li-sukum-ian-a. | wa-li-sukum-ian-a. |
| d. | *Ki-to-nyorr-unote* | *I-to-nyorr-unote* | *E-to-nyorr-unote* |
| | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| | tu-li-pend-an-a. | m-li-pend-an-a. | wa-li-pend-an-a. |

*(ii)Kiishio {–kino/ uno};*

Katika wakati ujao kiishio *–kinote* au *–unote* hupoteza viambishi *–ta, -te, -ti, -to, -tu* na kubadilika kuwa *-kino* au *–uno*. Katika nafsi ya pili silabi ya mwisho –no hurudiwa ili kurejelea nafsi zunazotendana. Katika nafsi ya pili wingi, mofimu ya wingi hudhirika kwa uradidi wa silabi ya mwisho *–no*. Katika hali hii, maana ya wakati hudhihirika kiipragmatiki. Uteuzi kati ya *-kino* na *-unote* pia ni wa kileksia. Sheria zitendazo kazi ili kusababisha mabadiliko haya ni:

*kinote > kino* / ------- #

*unote > uno* / ------- #

Mifano:

***Kiishio –kino;***

84a.

*Ki-pal-a-kino* *I-pal-a-kino-no* *E-pal-a-kino*

| | | |
|---|---|---|
| NF- MZ- MT-MN | NF- MZ- MT-MN-WI | NF- MZ- MT-MN |
| tu-ta-ach-ian-a / | m-ta-ach-ian-a / | wa-ta-ach-ian-a / |
| tu-ta-sameh-ean-a. | m-ta-sameh-ean-a. | wa-ta-sameh-ean-a. |

b.

| | | |
|---|---|---|
| *Ki-gor-o-kino* | *I-gor-o-kino-no* | *E-gor-o-kino* |
| NF- MZ- MT-MN | NF- MZ- MT-MN-WI | NF- MZ- MT-MN |
| tu-ta-kasirik-ian-a. | m-ta-kasirik-ian-a. | wa-ta-kasirik-ian-a. |

c.

| | | |
|---|---|---|
| *Ki-ng'ur-a-kino* | *I-ng'ur-a-kino-no* | *E-ing'ur-a-kino* |
| NF- MZ- MT-MN | NF- MZ- MT-MN-WI | NF- MZ- MT-MN |
| tu-ta-tafut-ian-a. | m-ta-tafut-an-a. | wa-tat-afut-an-a. |

***Kiishio –uno:***

85a.

| | | |
|---|---|---|
| *Ki-mbay-uno* | *I-mbay-uno-no* | *E-iba-y-uno* |
| NF- MZ- MN | NF- MZ- MT-MN-WI | NF- MZ- MT-MN |
| tu-ta-chuk-ian-a. | m-ta-chuk-ian-a. | wa-ta-chuk-ian-a |

b.

| | | |
|---|---|---|
| *Ki-nyorr-uno* | *I-nyorr-uno-no* | *E-nyorr-uno* |
| NF- MZ- MN | NF- MZ- MN-WI | NF- MZ- MN |
| tu-ta-pend-an-a. | m-ta-pend-an-a. | wa-ta-pend-an-a. |

c.

| | | |
|---|---|---|
| *Ki-rrum-uno* | *I-rrum-uno-no* | *E-rrum-uno* |
| NF- MZ- MN | NF- MZ- MN-WI | NF- MZ- MN |
| tu-ta-sukum-an-a. | m-ta-sukum-an-a. | wa-ta-sukum-an-a. |

*(iii) Kiambishi tamati {–ote* au *–ate}:*

Hii ni alomofu nyingine ya mofimu ya jinsi ya kutendana/ kutendeana katika wakati uliopita na hujitokeza katika vitenzi ambavyo huelezea hali ya watu wawili au zaidi kuelekezana kitendo. Alomofu hii hutii sheria ya ulinganifu wa irabu hivi:

$$ote \,/\, \text{------} \,\#\, \begin{bmatrix} +\text{irabu} \\ +\text{nyuma} \end{bmatrix}$$

$$ate \,/\, \text{------} \,\#\, \begin{bmatrix} +\text{irabu} \\ +\text{mbele} \end{bmatrix}$$

Mifano;

86a.

| | | |
|---|---|---|
| *Ki-ta-paash-ate* | *I-ta-paash-ate* | *E-ta-paash-ate* |
| NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| tu-li-pish-an-a / | m-li-pish-an-a / | wa-li-pish-an-a / |
| tu-li-pit-an-a. | m-li-pit-ana. | wa-li-pit-an-a. |

b.

| | | |
|---|---|---|
| *Ki-tu-ng'ua-r-ote* | *I-tu-ng'ua-r-ote* | *E-tu-ng'ua-r-ote* |
| NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| tu-li-teng-an-a / | m-li-teng-an-a / | wa-li-teng-an-a |
| tu-li-ach-an-a. | m-li-ach-an-a. | wa-li-ach-an-a. |

c.

| | | |
|---|---|---|
| *Ki-ta-ar-ate* | *I-ta-ar-ate* | *E-ta-ar-ate* |
| NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| tu-li-pig-an-a. | m-li-pig-an-a. | wa-li-pig-an-a. |

d.

| | | |
|---|---|---|
| *Ki-to-or-ote* | *I-to-or-ote* | *E-to-or-ote* |
| NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| tu-li-gaw-an-a / | m-li-gaw-an-a / | wa-li-gaw-an-a / wa-li-ach-an-a. |

tu-li-ach-an-a/

tu-li-ach-an-a

*Wakati uliopo na hali mazoea:*

(iii) Kiambishi tamati {–a / -o};

Uteuzi wa kiishio hiki cha hali ya kutendana ni wa kileksia na haudhihirishi sheria yoyote ya kifonemiki. Katika nafsi ya pili silabi ya mwisho inarudiwa ili kurejelea nafsi tenda.

87a.

| | | |
|---|---|---|
| *Ki-uri-a* | *I-ur-ia-ria* | *E-uri-a* |
| NF- MZ- MN | NF-MZ-MN-WI | NF-MZ-MN |
| tu-na-ogop-an-a / | M-na-ogop-an-a / | wa-na-ogop-an-a / |
| sisi hu-ogop-an-a. | nyinyi hu-ogop-an-a. | wao hu-ogop-an-a. |

Kuna uradidi wa silabi ya mwisho kuashiria wingi katika nafsi ya pili.

b.

| | | |
|---|---|---|
| *Ki-mba-r-o* | *I-m-ba-r-o-ro* | *E-iba-r-o* |
| NF-MZ-MT-MN | NF-MZ-MT-MN-WI | NF-MZ-MT-MN |
| tu-na-chuk-ian-a / | m-na-chuk-ian-a / | wa-na-chuk-ian-a / |
| sisi hu-chuk-ian-a. | nyinyi m-na-chuk-ian-a. | wao wa-na-chuk-ian-a. |

c.

| | | |
|---|---|---|
| *Ki-ar-a* | *I-ar-a-ra* | *E-ar-a* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ- MN-WI | NF-MZ-MN |
| tu-na-pig-an-a / | m-na-pig-an-a / | wa-na-pig-an-a./ |
| sisi hu-pig-an-a. | nyinyi hu-pig-an-a | wao hu-pig-an-a |

d.

| | | |
|---|---|---|
| *Ki-orr-o* | *I-orr-o-rro* | *E-orr-o* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ- MN-WI | NF-MZ-MN |
| tu-na-ng'ang'an-i-a / | m-na-ng'ang'an-i-a/ | wa-na-ng'ang'an-i-a / |
| sisi hu-ng'ang'an-i-a. | nyinyi hu-ng'ang'an-i-a. | wao hu-ng'ang'an-i-a. |

*(v) Kiambishi tamati {-ata / -oto} vya hali rai.*

Uteuzi wa kiishio hiki cha hali ya kutendana pia ni wa kileksia na haudhihirishi sheria yoyote ya kifonemiki. Kwa mfano;

| 88a. | | b. | |
|---|---|---|---|
| *Ma-iba-r-oto!* | *E-mba-r-ŏto!* | *Ma-iger-oto!* | *E-ngẹr-oto!* |
| NF-MZ-MT-MN | NF-MZ-MT-MN | NF-MZ- MN | NF-MZ- MN |
| Tu-chuk-ian-e! | Chuk-ian-eni! | Tu-andik-an-eni! | Andik-an-eni! |

Nasali *m* ya mdomo inachopekwa katika mazingira kati ya *e* na *b*, *n* inachopekwa katika mazingira kati ya e na g. Ni mfano wa usilimisho wa vipuạ.

| c. | | d. | |
|---|---|---|---|
| Ma-tu-mut-ata! | E-ntu-mut-ata! | Ma-ta-pal-ata! | E-n-ta-pal-ata! |
| NF-R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN |
| Tu-angam-izan-eni! | Angam-izan-eni! | Tu-ach-an-e! | Ach-an-eni! |

| e. | | f. | |
|---|---|---|---|
| *Ma-not-oto!* | *E-not-oto!* | *Ma-ta-ar-ata!* | *E-nta-ar-ata!* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN | NF-R-MZ-MN | NF-R-MZ-MN |
| Tukut-an-e! | Kuṭ-an-eni! | Tu-pig-an-e! | Pig-an-eni! |

### 5.3.6 Mnyambuliko wa jinsi ya kutendeka.

Mnyambuliko huu humaanisha hali ya kuwezekana au kutowezekana kufanyika kwa jambo. Mnyambuliko huu huzingatia kitendo kinachotendeka na kupuuza mtendaji na kitendewa. Mnyambuliko huu huashiriwa na maumbo tofauti yanayotegemea sifa za kimofosintaksia za idadi na wakati. Kwa mfano;

*Wakati uliopita:*

Katika wakati uliopita mnyambuliko huu huashiriwa na kiishio tamati {*-e*} katika umoja na {*-ate*} au {*-ote*} katika wingi. Umbo hili hupatikana katika vitenzi michache sana. Sifa nyingine muhimu ni kuwa kiishio hiki hudhihirisha ulinganifu wa irabuiliopo kwenye mnyambuliko na ile iliopo kwenye mzizi. Sheria zinazotawala maumbo haya ni;

e / -------- #

ate / -------- # [+ irabu, + mbele]

ote / -------- # [+ irabu, ± nyuma]

| | | | |
|---|---|---|---|
| 89a. | A-ti-gil-e | I-ti-gil-e | E-ti-gil-e |
| | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| | ni-li-vunj-ik-a. | u-li-vunj-ik-a. | a-me-vunj-ik-a. |
| b. | *Ki-ti-gil-at-e* | *I-ti-gil-at-e* | *E-ti-gil-at-e* |
| | NF-WK-MZ-WI-MN | NF-WK-MZ-WI-MN | NF-WK-MZ-WI-MN tu- |
| | li-vunj-ik-a | m-li-vunj-ik-a. | wa-me-vunj-ik-a. |
| c. | *A-ti-sip-e* | *I-ti-sip-e* | *E-ti-sip-e* |
| | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN | NF-WK-MZ-MN |
| | ni-li-lain-ik-a | ulilainika | alilainika |
| d. | *Ki-ti-sip-at-e* | *I-ti-sip-at-e* | *E-ti-sip-at-e* |
| | NF-WK-MZ-WI-MN | NF-WK-MZ-WI-MN | NF-WK-MZ-WI-MN |
| | tu-li-lain-ik-a. | m-li-lain-ik-a | wa-li-lain-ik-a |

***Kiishio {ayu, oyu / noyu};***

Katika wakati ujao, mazoea na hali rai kiambishi cha mnyambuliko wa jinsi ya kutendeka huchukua umbo *-ayu -oyu* au *-noyu*. Uteuzi hapa unategemea irabu inayomalizia shina la kitenzi. Kwa mfano, *-ayu* hutumika kwenye vitenzi vinavyoishia kwa irabu *a* ilihali *-oyu* hutumika katika vitenzi vinavyoishia na irabu *o* iloihali *-noyu* hupatikana kwenye vitenzi vinavyoishia irabu *u*. Ni kwa mintarafu hii basi maneno kama vile *imbung'a* huwa *I-mbung'-ayu* (shikika), toosho huwa *tooshoyu*, na inyang'u huwa *i-nyang'-u-noyu.* Ulinganifu wa irabu unadhihirika hapa nahivyo kudhihirisha sheria hizi;

ayu / -------- # [+ irabu, + mbele].

oyu / -------- # $\begin{bmatrix} + \text{irab} \\ + \text{nyuma} \end{bmatrix}$

noyu / ------- # $\begin{bmatrix} + \text{irabu} \\ + \text{nyuma} \end{bmatrix}$

Mifano:

Kiishio {-ayu};

Kiishio hiki hupatikana katika vitenzi vyenye irabu ya mbele katika mzizi. Kwa mfano;

90a. I-mbelekeny-a -Pindua

*E-ibelekeny-ayu* *Me-ibelekeny-ayu*

NF-MZ-MN UK-MZ-MN

ta-pindu-lik-a. ha-i-pindu-lik-i.

(*i* > *m* huchopekwa kwa sababu ya sauti *b* ya mdomo)

b. Te-yer-a - Pika

*E-yer-ayu* *Me-yer-ayu*

NF-MZ-MN UK-MZ-MN

-ta-pik-ik-a. ha-ki-pik-ik-i.

c. Ta-r-a - piga

*E-ar-ayu* *Me-ar-ayu*

NF-MZ-MN NF-MZ-MN

- ta-pig-ik-a. ha-i-pig-ik-i.

d. Ta-rany-a - imba

*E-rany-ayu* *Me-rany-ayu*

NF-MZ-MN UK-MZ-MN

-ta-imb-ik-a. ha-i-imbik-i.

*Alomofu {-oyu}:*

Kiishio hiki hupatikana katika vitenzi vinavyoishia na irabu *o*. Kwa mfano;

92a.

| | |
|---|---|
| To-bol-o - fung-u-a | |
| *E-bol-oyu* | *me-bol-oyu* |
| NF-MZ-MN | NF-MZ-MN |
| Ta-fung-ulik-a | ha-i-fung-ulik-i |

| | | |
|---|---|---|
| b. | *To-osh-o* - Piga | |
| | *e-osh-oyu* | *me-osh-oyu* |
| | NF-MZ-MN | UK-MZ-MN |
| | Ta-pig-ika | ha-i-pig-iki |

*Alomofu {–noyu}:*

Alomofu hii hupatikana katika vitenzi vya jinsi ya kutendeka vinavyoashiria mwendo kumwelekea mzungumzaji na vinavyoishia na irabu *u*.

| | | |
|---|---|---|
| 92a. | *Ti-gil-u* - Vunja | |
| | *Ke-gil-u-noyu.* | *Me-gil-u-noyu* |
| | NF-MZ-MT-MN | UK-MZ-MT-MN |
| | ta-vunj-ik-a | ha-i-vunj-ik-i. |
| b. | *Te-shet-u* - Jenga | |
| | *Ke-shet-u-noyu* | *Me-shut-u-noyu* |
| | NF-MZ-MT-MN | UK-MZ-MT-MN |
| | -ta-chom-ok-a | ha-i-chom-ok-i. |
| c. | *Ta-nap-u* - beba | |
| | *E-nap-u-noyu* | *Me-nap-u-noyu* |
| | NF-MZ-MT-MN | UK-MZ-MT-MN |
| | -ta-beb-ek-a | ha-i-beb-ek-i. |

Kama ilivyo kawaida ya vielelezo vinavyotokana na mfanyiko wa unyambuaji, mofimu *-ayu* na *-oyu* wakati mwingine huranda na kukiuka mfumo wa kisemantiki hivi kwamba hazielezei jinsi ya kutendeka, badala yake hujitokeza katika vitenzi sahili vya hali rai. Kwa mfano;

| | | |
|---|---|---|
| 93a. *E-suj-ayu!* | *Ti-gir-ayu!* | *To-oj-oyu!* |
| NF-MZ-MN | R-MZ-MN | R-MZ-MN |
| Og-eni! | Nyamaz-a! | Jikune! |
| b. *Te-mer-ayu!* | *Ma-itirring'-ayu!* | *Ta-raposh-oyu!* |
| R-MZ-MN | NF-MZ-MN | R-MZ-MN |
| Lew-a! | Tu-tuli-e! | Shib-a! |

**5.3.7 Mnyambuliko zalishi / geuzi**

Mnyambuliko huu huelezea mfanyiko wa kubadilika, kugeuka au kuingia katika hali fulani. Sifa nyingine ya kimsingi ya mnyambuliko huu ni kuwa licha ya kubadilisha maana ya neno, pia una uwezo wa kukibadilisha kikundi cha kisarufi cha lile neno, kwa mfano kukibadilisha kitenzi kiwe kivumishi au nomino.

Katika lugha ya Kiswahili mnyambuliko huu huwa na kiambishi awali {-pa} katika maneno k.v ogopa, nenepa, au lapa. Maneno haya yaweza kuzalishwa hivi:

94. *Ogop-a – wog-a, mwog-a, mwog-of-u*
*Nenep-a – nen-e, u-nen-e, m-nen-e*
*Lap-a – l-a, m-l-afi, u-l-afi* (lodhi 2002 :18)

Katika lugha ya Kimaasai, mnyambuliko huu huwakilishwa na kiambishi *u* au *yu* katika wakati ujao na hali mazoea. Katika mnyambuliko geuzi vitenzi vyaweza kubakia kuwa vitenzi au vibadilike kuwa nomino na vivumishi. Uundaji wa nomino unahusu kuchopekwa kwa mofimu za jinsia. Jinsi kike huwakilishwa na mofimu *e* au *en* ulihali uume huwakilishwa na *o* au *ol*. Katika mifano ifuatayo, itadhihirika kuwa irabu katika mofimu ya jinsia inasilimisha irabu za shina kwa sheria ya ulinganifu wa irabu. Kwa kufuata mantiki alioielezea Lodhi (2002) (tazama ukurasa wa 7), ugeuzaji au uzalishaji hujitokeza hivi katika lugha ya Kimaasai;

95a.

| | | |
|---|---|---|
| *A-mu-o-yu* | *Ol-omuoi* | *En-amuoi* |
| KB-MZ-MT-MN | J-SH | J-SH |

| | | |
|---|---|---|
| kuwa mgonjwa. | Mwanamume mgonjwa. | Mwanamke mgonjwa. |

b.

| | | |
|---|---|---|
| *A-sas-u* | *O-sas* | *E-sas* |
| KB-MZ-MT-MN | J-SH | J-SH |
| kukonda. | Mwanamume mkonde. | Mwanamke mkonde. |

c.

| | | |
|---|---|---|
| *A-ado-r-u* | *Ol-oodo* | *En-aado* |
| KB-MZ-MT-MN | J-SH | J-SH |
| kuwa mrefu. | Mwanamume mrefu. | Mwanamke mrefu. |

(katika hali sahili ya kitenzi, sauti *r* huchopekwa kuvunja mkururo wa irabu mwishoni. Ni mofimu tupu).

96a.

| | | |
|---|---|---|
| *A-do-r-u* | *Ol-odo* | *En-ado* |
| KB-MZ-MT-MN | J-SH | J-SH |
| kuwa mwekundu. | Mwanamume mwekundu. | Mwanamke mwekundu. |

b.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-ng'u-o-yu* | *E-ng'uan* | *O-long'u* | *E-nangu* |
| KB-MZ-MT-MN | J-SH | J-SH | J-SH |
| ku-nuk-a. | Uvundo | mume anayenuka. | Mwanamke anayenuka. |

c.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-mu-o-yu.* | *E-muoy-an* | *Ol-tamuoy-ai* | *En-tamuoy-ai* |
| KB-MZ-MT-MN | J-SH | J-SH | J-SH |
| kuwa mgonjwa | ugonjwa. | mwanamume mngonjwa. | mwanamke mgonjwa. |

d.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-sas-u* | *E-saso* | *O-sas* | *E-sas* |
| KB-MZ-MN | J-SH | J-SH | J-SH |

| | | | |
|---|---|---|---|
| ku-kond-a | ukonde | mwanamume mkonde. | mwanamke mkonde. |

e.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-iropi-ju* | *En-kirobi* | *Ol-kirobi.* | *En-airobi* |
| KB-MZ- MN | J-SH | J-SH | J-SH |
| kuwa baridi | baridi. | homa ya baridi | mahali au kitu baridi. |

*p* ya mzizi hubadilika kuwa *b* kufuata sheria p > b / ----- # / v – v.

f.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-nana-u* | *E-nanai* | *Ol-onana* | *En-anana* |
| KB-MZ- MN | J-SH | J-SH | J-SH |
| kuwa –ororo / laini. | wororo. | mwanamume mwororo. | mwanamke mwororo. |

g.

| | | | |
|---|---|---|---|
| *A-do-r-u* | *En-doron* | *Ol-odo* | *En-ado* |
| KB-MZ- MT-MN | J-SH | J-SH | J-SH |
| kuwa -ekundu. | wekundu. | mwanamume mwekundu. | mwanamke mwekundu |

Katika vitenzi *olodo*, na *enado*, irabu za mofimu ya jinsia imeathiri irabu za shina na mpangilio wake. Ni mfano wa mfanyiko wa usupuli kiasi au *partial supletion*.

h.

| | |
|---|---|
| *A-ado-r-u* | *En-k-adori* |
| KB-MZ-MT-MN | J-MT-SH |
| kuwa mrefu | urefu |

i.

*Ol-oodo* - mwanamume mrefu.
J-SH
*En-aado* – mwanamke mrefu.
J-SH

} Irabu za mofimu ya jinsia imeathiri irabu ya mzizi kwa mfanyiko wa uirabunganishaji (*dipthongization*).

### 5.3.8 Mnyambuliko radidi (reduplication).

Kama ilivyo katika lugha za kibantu uradidi una mifano mingi katika lugha ya Kimaasai. Umbo hili hutumiwa kuunda kitenzi vya kujirudiarudia kwa lengo la kukariri ukali / nguvu ya kitendo au ule uduni wake na pia kuelezea kitendo kinachotendeka kwa mazoea.

Hakuna kiambishi mahsusi kinachouakilisha isipokuwa uradidi wa shina au mzizi. Sheria za uradidi ni za kileksia huku vitenzi vikidhihirisha upekee katika kutekeleza mfanyiko huu.

Katika baadhi ya vitenzi, uradidi huhusu urudiaji wa mzizi mzima au sehemu yake na pengine irabu ya kuunganisha ikichopekwa katikati ya mizizi ile. Katika vitenzi vingine, uradidi unahusu udondoshaji wa silabi kadha. Kwa mfano;

*Vitenzi vinavyokariri nguvu au ukali wa kitendo:*

Baadhi ya vitenzi vinavyodhihirisha nguvu au ukali wa kitendo ni kama vile:

| | | |
|---|---|---|
| 97a. | *A-ning'* | *A-inining* |
| | KB-MZ | KB-MZ |
| | ku-sikia | ku-sik-iliz-a kwa makini |

Hapa kitenzi kimebadilika kutoka umbo la kitenzi cha kundi I na kuwa kitenzi chenye umbo la kundi II kwa kupata irabu awali ya shina.

| | | |
|---|---|---|
| b. | *A-ded* | *A-ded-e* |
| | KB -MZ | KB -MZ-MN |
| | ku-bomoa | ku-bomoa kwa fujo / nguvu. |

Msizitizo hapa huakilishwaishwa na uradidi wa irabu *e* ya mzizi.

| | | |
|---|---|---|
| c. | *A-ijul-u-jul* | *A-ijul-ul* |
| | KB-MZ-MT-MN | KB-MZ-MN |
| | Ku-inam-ish-a (bila kupindua). | Ku-pind-u-a (kabisa kiwe juu chini). |

Katika *aijulul* /u/ inachopekwa kuunganisha mizizi miwili nayo huku *i* ikidondoshwa katika mzizi wa pili. Katika *aijulujul* sauti /u/ ya kuunganisha na /j/ ya mzizi wa pili inadondoshwa.

d.

| | |
|---|---|
| *A-bol* | *A-bol-bol* |
| KB-MZ | KB-MZ-MN |
| kumushika ng'ombe mdomo bila shida. | kung'ang'ana kumshika ngombe mdomo kwa mikono yote miwili lau kwa shida. |

Huu ni mfano wa uradidi wa mzizi mzima.

*Vitenzi vinavyodunisha kitendo:* Vitenzi hivi huonyesha ule udhaifu wa kitendo. Kwa mfano;

| | | |
|---|---|---|
| 98a. | *A-tur-isho* | *A-tur-u-tur-isho* |
| | KB-MZ-MN | KB-MZ-MT-MN-KI |
| | ku-lima. | kulimalima ovyo ovyo bila makini wala bidii. |
| b. | *A-lot-u* | *A-lot-u-lot-u* |
| | KB-MZ-KI | KB-MZ-MT-MN-KI |
| | ku-kuja. | kukujakuja (polepole bila haraka). |
| c. | *A-woj-o* | *A-woj-i-woj-o* |
| | KB-MZ-KI | KB-MZ-MT-MN-KI |
| | ku-jikuna kwa nguvu. | Ku-jikunakuna (kidogo hapa na pale). |

Vitenzi vingine vya uradidi huonyesha hali ya mazoea au vitendo vinavyotendeka mara kwa mara. Kwa mfano;

| | | |
|---|---|---|
| d. | *A-morr* | *A-morr-i-morr* |
| | KB-MZ-KI | KB-MZ-MT-MN-KI |
| | ku-tukana. | ku-tukanatukana (kila mara). |
| e. | *A-arr* | *A-arr-i-arr* |
| | KB -MZ | KB-MZ-MT-MN-KI |
| | ku-chapa. | Ku-chapachapa kila mara. |

f. *A-lej* *A-lej-i-lej*

KB-MZ KB-MZ-MT-MN

ku-danganya. kudanganyadanganya kila mara.

Kuna vitenzi vichache ambavyo licha ya kuwa na umbo la uradidi huwa haviashirii nguvu au uduni wa kitendo bali hali sahili tu ya kitenzi. Sehemu iliorudiwa huwa ni mofimu moja isiogawika zaidi. Kwa mfano;

99a. *A-ipangipang*

NF-MZ

ku-hema kwa nguvu kwa sababu ya uchofu au ugonjwa.

b. *A-ineneng*

NF-MZ

ku-pima uzito.

c. *A-ilepilep*

NF-MZ

ku-piga kelele au kupayuka.

d. *A-ilejilej*

NF-MZ

ku-bembeleza kama mtoto / kutuliza.

*A-ilejilej* ni neno la kundi II kwa kuwa lina irabu awali *i* katika mzizi na halina uhusiano na neno *a-lej* la kundi I lililoelezewa hapo juu.

# SURA YA SITA
# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.1 Utangulizi

Sehemu hii ina sehemu mbili; sehemu ya kwanza ni muhtasari wa matokeo ya uchanganuzi uliofanywa wa mofimu zā mnyambuliko katika vitenzi vyá lugha ya Kimaasai. Sehemu ya pili nayo imejihusisha na hitimisho na mapendekezo ambapo mtafiti ameelezea maswala tata yanayoibuka katika utafiti huu na mapendekezo ya tafiti zingine zenye ukuruba na kazi hii.

## 6.2 Muhtasari

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni matatu; kwanza kutambulisha muundo wa vitenzi vya lugha ya Kimaasai kifonolojia na kimofolojia. Pili, kubainisha mofimu za mnyambuliko iliyopo katika vitenzi hivi na tatu kutambulisha 'maana na maumbo yanayotokana na minyambuliko hiyo. Madhumuni ya kwanza yalitekelezwa katika sura ya nne ambapo maelezo ya fonolojia ya Kimaasai na mofolojia ya vitenzi vya lugha hii yalitolewa kwa kifupi. Madhumuni ya pili na ya tatu yaliweza kutekelezwa katika sura ya tano na yafuatayo yakadhihirika;

(i) Kwamba vitenzi sahili vya lugha ya Kimaasai vyaweza kuishia kwa mojawapo wa viishio vifuatavyo; *a, e, i, o, u, -isho,-ishe, -ishote, -ishoyu, -u, -ua/uo, aa/oo, -aiyie/oiyie,* na *-ai/oi* huku vingi vikitawaliwa na sheria ya ulinganifu wa irabu na sifa za kimofosintaksia kama vile nafsi, wakati, ukanushaji au rai.

(ii) Kwamba lugha hii ina jumla ya minyambuliko minane ya vitenzi. Minyambuliko hii inawakilishwa na mofimu zenye seti ya alomofu zinazokitofautisha kielezo kimoja na kingine kutegemea sifa mbalimbali za kimofosintaksia kama vile nafsi, wakati au hali. Minyambuliko hii hutokea katika mazingira ya tamati isipokuwa mnyambuliko wa jinsi ya kutendesha unaojitokeza katika mazingira ya awali. Ufuataο ni muhtasari wa mofimu za unyambuaji wa vitenzi na alomofu za kila mnyambuliko.

Mnyambuliko wa jinsi ala-tendea: {*-ie*}, {-ieki}, {*-ishore*} na {*–ishoreki*}.

Mnyambuliko wa jinsi ya kutendea / uhusika tendea: {*–oki/-aki*, { *-aka/-oko*, {*-iki*, {*aa/-oo*}, {*okito/-akita*}na {*ikia/-ikita*}.

Mnyambuliko wa jinsi ya kutendesha: {*-it-*}, {*-nt-*, {*i*}, {*-m*} na {*n*}.

Mnyambuliko wa jinsi ya kutendwa/kutendewa: {*toi/tai*}, {*uni/i*}, {*-uoki*/-uaki}, {*-aki/-oki*}, {*-ikini/-akini/-okini*}, {*-koki/*-kak}i, {*-oyioki/-ayioki*}, {*-ari/*-or}i na {*–uno*}.

Mnyambuliko wa jinsi ya kutendana: {*-a/o*}, {*-ote/ate*}, {*-ata/-ōto*}, {*-kino/-kinote/-unote*}, {*uno*} na {*–kinoto*}.

Mnyambuliko wa jinsi ya kutendeka – alomofu -e, {*-ayu/-oyu/ -noyu*} na {*ate/-ote*}.

Mnyambuliko zalishi: {*yu*} na {*u*}.

Mnyambuliko radidi hauna mofimu maalum bali huashiriwa na uradidi wa shina au mzizi.

Jedwali hili linatoa muhtasari wa mnyambuliko wa vitenzi vya lugha hii:

| SAH | AL-EA | UH- EA | ESH | W/EW | AN | EK | GEUZI | RADIDI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| -a | -ie | -aka/-oko | -it- | -uoki/-uaki | -kinote/ -unote | -e/-ate/- ote | -yu | - |
| -e | -ieki | -akita/- okito | -nt- | -ayoki/- oyoki | -kino/ -uno | -Ayu/ -oyu | -u | - |
| -i | -ishore | -ikia/-ikita | -i- | -aki/-oki | -ate/ote | -noyu | | - |
| -o | -ishoreki | -iki | -m- | -kaki/ -koki | -a/-o | | | - |
| -u | | -aki/-oki | -n- | -uno | -ata/oto | | | - |
| -ishe/ - ishote | | -aa/-oo | | -toi/-tai | | | | - |
| -ua/-uo | | | | -ikini/-akini | | | | - |
| -aa/-oo | | | | -ari/-ori | | | | - |
| -aiye/-oiye | | | | -uni | | | | - |
| -isho | | | | | | | | - |
| -tie/-oitie | | | | | | | | - |
| -ai | | | | | | | | - |
| -ai/oi | | | | | | | | |
| -ishoyu | | | | | | | | - |

**Ufunguo**:

SAH: Sahili

AL-EA: Ala-tedea

UH-EA: Uhusika- tendea

ESH: Tendesha

W/EW: Tendewa

AN: Tendana

EK: Tendeka

GEUZI: Geuzi/zalishi

RADIDI: Uradidi

### 6.3 Mapendekezo

Kwa sababu ya utafiti huu kuzingatia mofimu katika vitenzi zaidi, kuna haja ya kuvitafiti vitenzi katika mazingira ya maneno mengine katika tungo, yaani kuchunguza dhana ya vitenzi kwa mwelekeo unaozingatia neno na wala sio mofimu kama kipashio cha kimsingi cha kisarufi. Unyambuaji ni mfanyiko mojawapo tu unaoathiri vitenzi. Kuna haja ya tafiti zingine za kina za kuchunguza jinsi mifanyiko mingine kama vile uambatanishaji na uambishaji inavyoathiri vitenzi vya lugha hii. Utafiti huu umeshughulikia Kimaasai cha eneo la Suswa, Mosiro na Ilkerin-Loita wilayani Narok; Hii ni lahaja mojawapo inayozungumzwa na Wamaasai. Kuna haja ya utafiti mwingine utakaochunguza tofauti za kimofofonemiki zilizopo kati ya lahaja za lugha hii.

### 6.4 Hitimisho

Swala la mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kimaasai ni tatizi. Licha ya kuwepo kwa kaida za ulinganifu wa vokali, udondoshaji na uchopekaji zinazoibua vielezo vyenye usare, mabadiliko yasiotarajiwa hutokea. Kwa mfano, kuna vitenzi vyenye umbo la jinsi ya kutendeka lakini kimsingi ni vya jinsi ya kutenda. Kwa mfano, maneno *i-rur-ayu* (lala), *i-suj-ayu* (oga), *ta-man-ayu* (chelewa) na mengineyo. Pia kuna maneno kama*a-ineneng* (kupima uzito) na *il-ejilej-a* (bembeleza) ambayo yanadhihirisha mnyambuliko wa kutendatenda lakini kimsingi ni vitenzi sahili. Mnyambuliko wa jinsi ya kutendesha huwakilishwa na viambishi awali katika baadhi ya vitenzi na viambishi tamati katika vitenzi vingine.

Hata hivyo, vitenzi vinavyokiuka sheria za minyambuliko ni vichache sana katika msamiati wa lugha hii na havitoshi kubatilisha mfumo na usare unaodhihirika katika unyambuaji wa vitenzi vya lugha ya Kimaasai.

Tatizo lingine lipo katika hali ya vitenzi vya lugha ya kimaasai kubadilisha viambishi vya mnyambuliko kulingana na nafsi, nyakati na hali tofauti. Jambo hili linasababisha kuzuka kwa vielelezo vingi vya alomofu za mnyambuliko fulani. Jambo hili laweza kumtatiza mgeni wa lugha hii. Utata huu umepunguzwa kwa kuandamanisha mifano na tafsiri za lugha ya Kiswahili. Tatizo lingine hutokea pale ambapo umbo moja hubeba maana zaidi ya moja. Katika hali kama hii, maana hudhihirika kipragmatiki (kimatumizi) kwa kuzingatia maneno mengine yaliyo jirani ya kitenzi husika au kwa kuzingatia sifa ya kiarudhi ya toni.

Kazi hii imechunguza mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kimaasai kimofolojia (kimuundo) na kisemantiki (kimaana) kwa kufuata mwelekeo unaozingatia mofimu kama kipashio cha kimsingi cha kisarufi. Kwa sababu hii basi, umejikita zaidi katika kuchunguza muundo wa kitenzi kinapoathiriwa na mfanyiko wa unyambuaji au kuwepo kwa kategoria mbalimbali za kimofosintaksia kama vile wakati, nafsi, urejeleaji au rai. Hata hivyo kama asemavyo Anderson (1992) kuwa mofolojia ni mfumo wa mahusiano kutoka viwango mbalimbali vya uchanganuzi wa lugha kama vile fonolojia, sintaksia na pragmatiki, maswala ya mofofonemiki, mofosintaksia na leksia yameibuka na kuelezewa pale ilipobidi.

## MAREJELEO


Adams, V. (1973) *An Introduction to Modern English Word-Formation*, London, Longmans.

Anderson, S. (1992) *A-Amorphous Morphology*, Cambridge, Cambridge University Press.

Aronoff, M. (1979) *Word Formation in Generative Grammar*. Cambridge, Cambridge University Press.

Aswani, F. O. B. (2001) *Uswahilishaji Kifonolojia wa Maneno Mkopo Yenye Asili ya Kiingereza Katika Kiswahili Sanifu*. Ph. D Thesis, Njoro, Egerton University.

Ashton, E, O. (1944) *Swahili Grammer (including Intonation)*. London, Longmans.

Bakari, M. (1982) *The Morphophonology of Kenyan Swahili dialects*, PH. D Thesis, Nairobi, University of Nairobi.

Barker, C. (1978) *Introduction to Generative Syntax*, New Jersey, Eagle Wood Cliffs.

Bauer, L, (1983) *Introducing Morphology*, Edinburgh, Edinburgh University Press.

Boudewyn, A., (1933) *Kazi ya Sarufi ya Kiswahili*, Albertville, Procure des peres Blances

Bloomfield, G. W. (1931) *Sarufi ya Kiswahili*, London, The Sheldon Press.

Bloomfield, L. (1933) *Language*, New York, Holt.

Chai, J. F. (2002), *Language Use In a Medical Setting: Reconciling Explanatory models of Illness in the Diagnostic Interview Among the Giriama of Kenya*. Unpublished Ph.D Thesis, Colchester, University of Essex, UK.

Chomsky, N. (1957) *Syntactic Structures*. The Hague, Mouton.

Chomsky, N. and Halle, M., (1968) *The Sound pattern of English*, New York, Harper and Row.

Church Missionary Society, (1971) *Maasai Basic Course*, Nairobi, C.M.S.; Language.

Doke, C. (1943) *Outline Grammar of Bantu*, Johannesburg, University of Witwatersrand.

Dressler, W, U., (1990) *Contemporary Morphology*, Berlin, Mouton De gruyter.

Eglin, L. and Betty A. (1975) 60 *Lessons in Maasai with Tests*, Kajiado, CMS.

Erhardt, J. (1857) *Vocabulary of the Engutuk Ooloikop as Spoken by the Maasai Tribes in East Africa*, Wertenburge, CMS.

Greenburg, J. (1963) *Universals of Language*, Cambridge, MIT Press.

Habwe j. na Karanja P., (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*, Nairobi, Phoenix publishers.

Harris, S. (1951) *Structural Linguistics*, Chicago, Chicago University Press.

Hockett, C. (1958) *A Course in Modern Linguistics*, New York, Macmillan.

Holis., A, C. (1905) The Maasai: *Their Language and Folklore*, Clarendon Press, Oxford.

Holsti, R. (Ed) (1968) *"Content Analysis"* In Nachmias. E., *Handbook of Social Psychology*,

New Jersey, Gardener and Eliots Ltd.

Johnson, F. (1939) *A standard Swahili-English Dictionary*, London, Oxford University Press.

Kapinga, C. (1983) *Sarufi Maumbo ya Lugha ya Kiswahili Sanifu*, Dar-esalaam, TUKI.

Kiparsky, P. *"Word Formation and the Lexicon"* In: Ingemann, F. (ed) (1983) *Proceed ings of the 1982 Mid-American Linguistics Conference*, Kansas, University of Kansas.

Kipury. N. (1984) *Oral Literature of the Maasai*, Nairobi, Kenya Literature Bureau.

Krapf, L. (1854) *Engutuk Ooloikop*, Tubingen, Ludwig Fried Fues Press.

Lass, R. (1984) *Phonology*, Cambridge, Cambridge University Press.

Lodhi, A. (2002) *"Verbal Extensions in Swahili and Nyamwezi"* www.google.com.

Lyons, J. (1968*) Introduction to Theoretical Linguistic* Cambridge, Cambridge University press.

Malmkjaer, K. (1991) *The Linguistics Encyclopedia*, London, Routledge.

Marantz A. 1988), *"Clitics; Morphological Merger and the Mapping to Phonological Structure"*, In Hammonds and Chomsky (eds), (*Language and the Mind*, Oxford, Oxford University Press.

Marchand, H. (1969) *The Categories And Types of Present-Day English Word-Formation,* Munich, C, Beck.

Mathews, P., (1974) *Morphology*, Cambridge, Cambridge University Press.

Mbaabu, I. (1985) *Sarufi ya Kiswahili,* Nairobi, Kenya Publishing and Book Company.

Meinhorf, C. (1904) *Linguistc Studies in East Afrika:* Hamburg, Mittuilungen des Semminars fur Orientalische Sprachen.

Miehe, G. (1989) *Verbal Extentions in Swahili and Neihgbouring Languages.* Windhoek, Logos.

Mol, F. (1979) *Maa – A Dictionary of the Maasai language and Folkore : English – Maasai,* Marketing and Publishing.

Nachmias, F. (1992) *Research Methods in the Social sciences*, Munich Arrowsmith Ltd.

Nida, E. (1994) *Morphology: The Descriptive Analysis of Words*, University of Ann Arbor, Michigan Press.

Polome, E. (1967) *Swahili Language handbook*, Washington, Centre For Applied Linguistics.

Radford, A. (1988) *Transformational Grammar* Cambridge; CUP

Robins R. H. (1989) *General Linguistics; an Introductory survey*, London, Longman.

Sankan, S, S. (1979) *Ntepen Olmaasae*, Nairobi, Kenya literature Bureau.

Scalise, S. (1988) *Inflection and Derivation*, Dorrecht, Floris.

Shafter, R. (1955) *Twelve Lessons in Maasai: A Simple Introduction to Learning Maasai*, Nairobi, Eagle Press.

Schiffrin, D. (1994) *Approaches to Discourse*, New York, Blackwell Publishers.

Spencer, A. (1991) *Morphological Theory*, Oxford, Blackwell Publisher.

Tucker, A. and Mpaayei, T., (1954) *A Maasai Grammar With Vocabulary*, London, Longmans.

Tuki, (1981) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Nairobi, OUP.

Tuki, (1990), *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, Dar es salaam, TUKI.

Tuki, (2000) *English-Swahili Dictionary*, Dar es Salaam, TUKI.

GERTON UNIVERSITY LIBR